**25 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 25 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*- KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jumanne Sagini.

Katibu.

**25 APRILI, 2024**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*- KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aje kwa ajili ya maswali kutoka kwenu, lakini leo ataanza na taarifa kwa sababu kanuni zetu zinaruhusu yeye kutoa taarifa ya jambo linaloweza kuwa limetokea na anataka kulitolea taarifa hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kushiriki Kikao hiki cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu tukiwa buheri wa afya.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, zimetoa fursa ya uwepo wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kwa siku ya Alhamisi. Vilevile Kanuni ya 44(4) imeruhusu Waziri Mkuu kutumia kipindi cha maswali ya papo kwa papo kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Aprili, 2024 wakati nikihitimisha Hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, nilieleza kwa uchache kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na athari zinazotokea hapa nchini. Kutokana na unyeti wa suala hili nimeona ni vyema nitumie kipindi cha leo kutoa taarifa kuhusu mwenendo wa matukio ya hali ya hewa, athari zake na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani inaendelea kuongezeka kila mwaka na athari zake zinaendelea kuwa kubwa. Tathmini ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani, inaonyesha kuwa wastani wa ongezeko la joto kwa mwaka 2023 ulifikia nyuzijoto 1.4 kwa kipimo cha *celsius* na

kuvunja rekodi ya kuwa mwaka wa joto kubwa zaidi katika historia ya dunia. Kwa upande wa Tanzania wastani wa ongezeko la joto mwaka 2023 ulifikia nyuzijoto moja kwa kutumia kipimo cha *celsius* ambapo pia ulivunja rekodi kwa kuwa mwaka wenye joto kubwa zaidi katika historia yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yamesababisha kuongezeka kwa mvua ambazo zimeleta athari katika maeneo mbalimbali duniani. Tumeshuhudia pia nchi mbalimbali zikipata mafuriko hasa katika maeneo ambayo yalizoeleka kutokuwa na mvua kabisa au mvua chache. Mathalani hivi karibuni tumeshuhudia baadhi ya nchi za Afrika, Asia na maeneo mengine kupitia vyombo mbalimbali vya habari zikikumbwa na mafuriko makubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini taarifa za tathmini kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* zimeendelea kuonesha mwelekeo wa kuongezeka kwa kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo matukio ya mvua kubwa, upepo mkali na athari zake katika sekta zote za kiuchumi na kijamii. Taarifa ya Utabiri wa Hali ya Hewa ilibainisha kuwepo kwa mvua kubwa kuanzia mwezi Oktoba, 2023 hadi Mwezi Mei, 2024, katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla utabiri wa mvua ulionesha uwepo wa mvua za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya nchi zikiambatana na matukio ya mvua kubwa zilizochagizwa na uwepo wa *El-Nino*. Kwa kawaida *El-Nino* huambatana na ongezeko kubwa la mvua katika maeneo mengi nchini na hata kusababisha mafuriko. Tathmini ya mvua kwa misimu yote inaonesha kuwa maeneo mengi yatapata mvua za juu ya wastani zikiambata na matukio ya hali mbaya ya hewa hususan matukio ya mvua kubwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la joto duniani limesababisha uwepo wa *El-Nino* ambayo imeambatana na mvua kubwa zilizosababisha mafuriko hapa nchini kwetu. Mwezi Oktoba hadi Desemba, 2023, kulikuwa na ongezeko kubwa la mvua ambapo jumla ya milimita 534.5 zilipimwa ikilinganishwa na milimita 227.2

kwa mwaka 2022, ikiwa ni ongezeko la 135%. Vilevile ongezeko hilo la mvua kubwa limeshuhudiwa katika kipindi cha mwezi Januari, hadi Aprili, 2024 na utabiri wa hali ya hewa unaonesha kuwa mvua za masika zitaendelea hadi mwezi Mei, 2024.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayoendelea hapa nchini na duniani kote, kuna umuhimu wa kuimarisha uwezo wa nchi yetu katika masuala ya utabiri wa hali ya hewa ili kuwezesha hatua za kuchukuliwa kwa wakati na hivyo kuepuka na kupunguza maafa yanayoweza kujitokeza. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Hali ya Hewa nchini ikiwemo kufunga miundombinu ya kisasa ya hali ya hewa ambayo kwa sasa inaendelea kutoa utabiri. Mafunzo kwa watumishi yameimarishwa kwa kuzingatia vigezo vya kitaifa na kimataifa na kuweka mifumo wezeshi ya usambazaji wa taarifa ya hali ya hewa pamoja na kuimarisha mifumo ya uhakiki kwa ubora wa huduma zinazotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa miundombinu uliofanyika unajumuisha ununuzi wa rada za hali ya hewa ambapo rada mbili zinakamilishwa kufungwa katika Mikoa ya Kigoma na Mbeya. Vilevile rada nyingine mbili zinatarajiwa kufungwa Mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro ifikapo mwishoni mwa mwaka 2024. Uwekezaji huu umesaidia kuongeza ufanisi na usahihi wa utabiri wa hali ya hewa hapa nchini. Hatua hii itaifanya Tanzania kuwa na rada saba ambapo ni kiwango kikubwa cha rada katika nchi za Afrika Mashariki na Kati. Kutokana na jitihada hizo sasa Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi za mwanzoni kabisa kufanikisha kupata Cheti cha Ubora wa Kimataifa katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwenye Sekta ya Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafaniko hayo, Tanzania imeweza kuzisaidia nchi nyingine za Afrika na nje ya Afrika katika masuala ya uanzishaji na utekelezaji wa mifumo ya utoaji huduma bora za hali ya hewa katika viwango vinavyotambulika kimataifa.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa uwekezaji mkubwa alioufanya katika Sekta ya Hali ya Hewa na kuijengea uwezo nchi yetu na kuifanya kuwa kinara Afrika na nje ya Afrika katika masuala ya utabiri wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie athari za mvua zinazoendelea. Mvua kubwa za *El-Nino* zinazoambatana na upepo mkali, mafuriko na maporomoko ya udongo katika maeneo mbalimbali nchini zimesababisha athari kubwa. Athari hizo ni pamoja na vifo, uharibifu wa mazao, makazi, mali za wananchi, miundombinu kama vile barabara, madaraja na reli. Kutokana na athari hizo, zaidi ya kaya 51,000 za watu 200,000 waliathirika ambapo watu 155 walipoteza maisha na watu wapatao 236 walijeruhiwa na nyumba zaidi ya 10,000 ziliathiriwa kwa kiwango tofauti.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyoathirika ni miundombinu ya shule, zahanati, nyumba za ibada, barabara, madaraja, mifugo na mashamba yenye mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yaliyoathirika mmepata kuyatembelea na kujionea hali halisi na hivi karibuni mimi pamoja na Mawaziri nane wa kisekta pamoja na Makatibu Wakuu nane wa kisekta walitembelea maeneo ya Mlimba, Ifakara na Malinyi Mkoani Morogoro na kule Rufiji na Kibiti Mkoani Pwani. Natumia fursa hii kuwasilisha salamu za pole za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwajulisha kuhusu misaada inayotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru sana wadau mbalimbali nchini ambao wamekuwa mstari wa mbele kuungana na Serikali kuwasaidia Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga. Natumia fursa hii kuendelea kuwasihi Watanzania wenzangu kuungana na Serikali kuwasaidia wananchi wenzetu wanaopatwa na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yaliyoathirika nchini ni pamoja na Rufiji na Kibiti, Mkoani Pwani; Malinyi, Mlimba, Kilosa,

Manispaa ya Morogoro na Ifakara, Mkoani Morogoro; Ilala, Kinondoni, Ubungo, Kigamboni na Temeke, Mkoani Dar es Salaam; Same, Hai na Moshi, Mkoani Kilimanjaro; Mbarali, Kyela na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mkoani Mbeya; Manispaa ya Kigoma Ujiji na Kakonko, Mkoani Kigoma; Iringa Vijijini, Mkoani Iringa; Manispaa ya Tabora, Mkoani Tabora; Bahi, Mkoani Dodoma; Lindi Manispaa, Kilwa, Liwale na Nachingwea, Mkoani Lindi; Masasi, Mkoani Mtwara; pamoja na Arusha Jiji, Monduli na Karatu, Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni Muleba na Bukoba Manispaa, Mkoani Kagera; Manispaa ya Shinyanga, Mkoani Shinyanga; Geita Mji, Nyangwale na Chato, Mkoani Geita; Mbozi na Momba, Mkoani Songwe; Nkasi, Sumbawanga na Kalambo, Mkoani Rukwa; pamoja na Hanang, Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine nitumie fursa hii kutoa pole kwa ndugu zetu walioathirika na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha hapa nchini na nitoe rai kwa wananchi wote kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha hapa nchini. Nawasihi sana wananchi kuwa na subira kipindi wanapoona maji mengi yanapita hususan barabarani ili kuepuka ajali zinazoweza kusomba magari na kuangukia kwenye mashimo na kupoteza maisha ya abiria au waendesha vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukumbusha kuwa uratibu na usimamizi wa maafa nchini unazingatia Sheria na Kanuni za Usimamizi wa Maafa zilizopo ambapo maafa yanashughulikiwa katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa kupitia Kamati za Usimamizi wa Maafa. Kamati hizo zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na.6 ya Mwaka 2022. Naendelea kuzikumbusha Kamati hizo kuwa tayari wakati wote kuchukua hatua endapo dharura hizo zitajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali maafa hushughulikiwa katika ngazi za Wilaya, Mikoa na Taifa kulingana na ukubwa wa maafa husika. Utaratibu uliopo unatoa fursa ya ngazi ya chini kutoa taarifa kwa ngazi ya juu endapo maafa hayo

yaliyojitokeza yanazidi uwezo wa ngazi husika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kulingana na ukubwa wa maafa hayo. Hivyo, nasisitiza Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi zote kuendelea kuweka mipango madhubuti na kutekeleza majukumu ya usimamizi wa maafa katika ngazi zao.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kutokana na maafa yaliyotokea nchini. Serikali kupitia Kamati ya Usimamizi na Maafa na wadau imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuzuia, kukabiliana na kurejesha hali. Hatua hizo zinajumuisha utoaji wa elimu kwa jamii ya kujikinga na kuchukua tahadhari na hasa wanaoishi mabondeni kukabiliana na maafa na kurejesha miundombinu iliyoharibika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoa misaada ya kibinadamu ikiwemo chakula, vifaa vya ujenzi, vifaa vya malazi na vifaa vya usafi. Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa na misaada kutoka Serikalini na wadau kama vile uokoaji, vyakula, mahema, madawa na marekebisho ya miundombinu ya utoaji huduma zinaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kikamilifu na inaendelea kuchukua hatua stahiki ili kuzuia na kupunguza makali ya majanga sambamba na kurejesha hali katika maeneo mbalimbali yaliyoathirika. Ikumbukwe kuwa katika kuchukua tahadhari za mvua hizi, Serikali iliandaa Mpango wa Taarifa ya Dharura ya Kuzuia na Kukabiliana na Maafa ya *El-Nino* kwa kipindi cha Septemba, 2023 mpaka Juni, 2024, sambamba na kuandaa mipango ya dharura katika mikoa 14 iliyokuwa katika hatari ya kuathiriwa na mvua kubwa kutokana na uwepo wa *El-Nino*.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mipango hii yanafanyika pamoja na utoaji wa mafunzo ya kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa Mikoa ikijumuisha mikoa iliyokuwa katika hatari ya kukumbwa na maafa kutokana na uwepo wa *El-Nino*. Maandalizi haya yamesaidia sana mikoa na sekta nyingine kuchukua hatua stahiki za kuzuia na kupunguza madhara pamoja na kujiandaa na kukabiliana na maafa yaliyosababishwa na mvua kubwa za *El-Nino* katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa baadhi ya shule zimeathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha hapa nchini, Wakurugenzi wa halmashauri pamoja na wamiliki wa shule zilizoathirika watekeleze maelekezo ya Serikali kulingana na athari zilizopo katika maeneo yao ili shule hizo zianze kutumika kwa wanafunzi kuingia madarasani na kusoma.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya tarehe 15 Aprili, 2024, kwa kuwa athari tunazozishuhudia sasa zinatokana na uharibifu wa mazingira ambao kimsingi unasababishwa na ukataji wa miti ovyo kwa matumizi ya nishati, kilimo kisichokuwa endelevu kinachofanyika kwa kukata miti na kuchoma mashamba ikiwa ni njia ya kurahisisha maandalizi ya shamba. Sababu nyingine ni ufugaji holela usiozingatia uwezo wa eneo la malisho ambao umesababisha mifugo kuharibu ardhi na maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tunao wajibu wa kutunza mazingira yetu ili kuepuka athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira ambazo zimekuwa na athari kubwa kwa nchi yetu. Hivyo natumia fursa hii kuwasihi Watanzania wenzangu tuwe mstari wa mbele katika kuhifadhi mazingira yetu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha taarifa yangu nitumie nafasi hii kusisitiza masuala yafuatayo:-

(a) Taasisi za Serikali ziendelee kujizatiti kukabiliana na maafa kwa kushirikiana na wadau kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Madhara ya *El-Nino* pamoja na mipango ya kisekta ili kuzuia na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza;

(b) Kamati za Maafa za Wilaya na Mikoa ziendelee kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa tahadhari kwa wananchi na kusaidia wananchi kwa wakati pindi maafa yanapojitokeza;

(c) Nawasihi wananchi wafuatilie taarifa za utabiri wa hali ya hewa ambazo zinatolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa na

kuzingatia maelekezo yanayotolewa na viongozi katika maeneo yao ikiwemo kuhama maeneo ya bondeni na kuhamia maeneo yaliyo salama, kulima mazao yanayopendekezwa ili yaweze kuiva haraka;

(d) Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata, Mitaa na Vijiji wasimamie ipasavyo usafi katika maeneo yao na kudhibiti utupaji taka ovyo unaosababisha kuziba kwa mitaro badala ya kusubiri usafi unaofanyika kila jumamosi ya mwisho wa mwezi;

(e) Kwa kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa na athari kubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi, hivyo viongozi wa ngazi zote washirikiane na wananchi kudhibiti uharibifu wa mazingira katika maeneo yao;

(f) Kwa kuwa Serikali imetoa maelekezo ya kufunga shule zilizoathiriwa na mafuriko, halmashauri na wamiliki wa shule hizo waweke utaratibu wa kufidia muda wa vipindi ili kukamilisha kalenda ya muhula kama ilivyopangwa;

(g) Wamiliki wa shule na madereva wa mabasi yanayotoa huduma za usafiri kwa wanafunzi wajiridhishe kuhusu njia wanazopita ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wanaobebwa katika vyombo hivyo vya usafiri;

(h) Wazazi, walezi na jamii ya Watanzania kwa ujumla tushiriki kikamilifu katika kuhakikisha usalama wa wanafunzi wanapokwenda na kurudi shuleni wakati wote, hususani katika kipindi hiki cha mvua nyingi;

(i) Wakala wa Barabara *(TANROADS)*, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA), TAZARA* na Shirika la Reli nchini mfanye tathmini ya barabara na njia za reli zilizoathirika na mafuriko kwenye maeneo mbalimbali yaliyoathirika na kuweka mpango wa kukarabati haraka ili kurejesha mawasiliano. Aidha, wabainishe maeneo yaliyopitiwa na mkondo wa maji kote na kuweka alama za tahadhari;

(j) Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, iendelee kutoa tahadhari kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara wakati wa mvua;

(k) Kamati za maafa katika ngazi za vijiji, wilaya na mikoa zisimamie kikamilifu ugawaji wa misaada inayotolewa kwa waathirika wa mafuriko na kuhakikisha kuwa misaada hiyo inawafikia walengwa tu;

(l) Viongozi wa Serikali kuanzia ngazi ya vijiji wahamasishe na kuelimisha wananchi wanaoishi mabondeni, kuhamia maeneo yaliyo salama ili kuepusha maafa wakati wa mafuriko na kuhakikisha wanatenga maeneo salama yanayotumika na wananchi watakapohamia kutoka mabondeni;

(m) Mamlaka za mipango miji kote nchini, zisimamie kikamilifu mipango ya miji ya halmashauri na kudhibiti ujenzi holela unaozuia njia za maji. Aidha, mipango ya matumizi bora ya ardhi iandaliwe katika maeneo yote ya vijiji na kusimamiwa ipasavyo; na

(n) Wizara ya Afya itoe elimu ya afya ya jamii ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko pamoja na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa tiba unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kipekee nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kujitoa kwenu kwa hali na mali katika kipindi hiki cha maafa. Tumewashuhudia mikoani kwenye maeneo yenu mkitumia muda wenu na mali zenu kwa ajili ya kuwafariji wananchi walioathirika na maafa katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru wadau wengine wakiwemo wafanyabiashara, taasisi za dini, vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla ambao wamekuwa mstari wa mbele kuwasaidia waathirika wa maafa. Tunawashukuru sana, tundelee kuwa na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru Jeshi la Akiba, Mgambo, *Red Cross* pamoja na majeshi yetu kwa kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba wananchi wanaokolewa na wanasimamiwa usalama wao mahali walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la udhibiti wa majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa ni mtambuka, natoa wito kwa mamlaka zote zinazohusika kushirikiana katika kuzuia na kupunguza athari zinazotokana na majanga hayo. Kwa upande mwingine nawasihi Watanzania wenzangu kuchukua tahadhari katika kipindi hiki ili kuepuka majanga yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Zipo dakika chache kama Mbunge ana swali kuhusu taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimewaona Waheshimiwa Wabunge watatu; Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, *TMA* imekuwa ikijitahidi sana kutoa taarifa sahihi kuhusu uwepo wa mvua kubwa nchini kwetu na Serikali ina vyombo vyake vingi vya kujua kwamba mvua inanyesha kubwa sehemu gani. Sasa, badala ya kuacha utashi wa mzazi aseme nimpeleke mtoto wangu shule au nisimpeleke, kwa nini zile mamlaka zetu kule chini zisiwe zinatoa taarifa kwamba leo Mtwara kuna mvua kubwa, watoto wote wasiende shuleni ili kuepusha maafa ambayo yanatokea na yanawakumba watoto wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwamba, Serikali yetu imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye mfumo wa utoaji taarifa ya hali ya hewa kila siku hapa nchini. Taarifa hizi ambazo zinatokana na mitambo na wataalam walioko kwenye

sekta zinatakiwa zizingatiwe pia na mamlaka zote mpaka kule vijiji. Kwa hiyo ni jukumu la mamlaka zetu ambazo pia ni Kamati za Maafa kutoa taarifa za hali ya hewa ili kuepusha maafa hayo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa maelekezo hapa kwa halmashauri zote nchini na mikoa kwa kupitia wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, wahakikishe kuwa wanajenga utamaduni wa kutoa mawasiliano wakati wote pindi wanapopata taarifa za hali ya hewa. Kama taarifa ya hali ya hewa hiyo inaweza kuwa mbaya kwenye eneo hilo, basi ni wajibu wa Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado narudia tena kuwasihi na kuwataka Wakuu wa Mikoa kufuatilia mwenendo wa hali ya hewa hasa kipindi hiki ambacho kinaonesha kwamba mvua zitaendelea kuwa kubwa mpaka mwezi Mei, waweze kujua, je, kwenye mkoa wao hali ya hewa ikoje na waweze kutumia njia hiyo kuweza kutoa taarifa kwa wananchi wao kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza viongozi wetu walioko mikoani kuhakikisha kwamba wanatoa taarifa hizi mara kwa mara na ndio wajibu wao ili kuweza kuokoa hali hii ambayo watu wengine walikuwa hawapati taarifa huku mamlaka zetu za Serikali zikiwa ziko pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nalichukua hili kwa ajili ya kuendelea kuliimarisha zaidi kwenye kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kuwa nyingi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**SPIKA:** Washa kisemeo.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Waheshimiwa Mawaziri ambao walitutembelea wakati tulipopata maafa.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa aliyotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakutaja katika taarifa Mkoa mzima wa Morogoro ambao pia ulikumbwa na mafuriko, ikiwemo Wilaya ya Mvomero, Morogoro *DC* ambayo mimi natoka na Ulanga. Kwa mfano kwenye jimbo langu zaidi ya nyumba 300 na kitu zimevunjika na mashamba. Sasa swali, ni je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na mafuriko haya ambayo yanatokea kila mwaka hasa katika Mkoa wa Morogoro, katika suala la kuchimba mabwawa ili kuweza kupunguza kasi ya mito ambayo iko mingi katika Mkoa wa Morogoro na kuendelea kuleta maafa kwa wananchi wetu na Serikali kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Kalogeris, Mbunge wa Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakiri kwamba tumesahau kuiweka Ulanga, lakini Ulanga pamoja na Malinyi ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimeathirika. Kote huko Kamati zetu za Maafa za Wilaya na Mkoa pamoja na hawa Waheshimiwa Mawaziri Nane na Makatibu Wakuu wote wamepita kule na wameona hiyo hali. Pia nimepata nafasi, nimepita maeneo hayo kutoka kule Mlimba, nimekuja Ifakara Mjini. Nilipokuwa naenda Malinyi nilipitia Ulanga kuona hali hiyo. Hakika hali siyo shwari sana kwa sababu eneo lote limejaa maji; na bado nikapita juu ya Mto Rufiji mpaka Rufiji kwenye kuona hali hiyo na ujaaji wa maji. Ni kweli kwamba maeneo hayo yamepata athari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba bonde hili tunalitumia vizuri na hasa kwa

kuelekeza maji kwenye maeneo yanayoweza kuleta manufaa kwa wananchi. Tayari Wizara zetu mbili, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zimeshaandaa mpango wa kuchimba mabwawa, yatakayoweza kukusanya maji haya kwa matumizi mbalimbali ikiwemo moja, umwagiliaji na mbili, kutakuwa na uvuvi mdogo mdogo kwa maeneo hayo yenye mabwawa pamoja na kunyweshea mifugo yetu. Tayari wataalamu wako Ifakara kuona maeneo sahihi ya kuchimba mabwawa hayo ili kuchepusha maji kutoka kwenye ule Mfereji Mkubwa wa Rufiji na kupeleka kwenye mabwawa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati huu pia unaendelea mpaka uelekeo wa Mto Wami, ambako huko nako pia kupitia mfereji ule tunachimba Bwawa kubwa sana la Kidunda kwa ajili ya matumizi ya maji ambayo yataingia Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na mpango huu mpaka Bonde la Mto Rufiji, Maeneo ya Rufiji yenyewe nako pia tumeshatenga fedha kwa ajili ya kuchimba mabwawa ili tuelekeze maji yetu katika maeneo hayo, tuyahifadhi halafu tutakuwa tunayatumia kulingana na mahitaji kwenye maeneo yote matatu ya kilimo, mifugo pamoja na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna hii hii tutaendelea na mabonde yote. Bonde la Mto Ruvuma tutafanya kazi hiyo; kule eneo la Nyasa tutafanya jambo hilo na Wizara zetu zimeendelea kuongezewa bajeti na wataendelea na kazi hiyo kadiri tunavyopata fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na napenda pia kutumia nafasi hii kupongeza jitihada za Serikali katika masuala mazima ya hali ya hewa. Kwa kweli taarifa zinazotolewa zimekuwa na usahihi wa hali ya juu na zinatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nchi yetu pamoja na ushiriki wa uhifadhi na mazingira, lakini pia Mheshimiwa Rais wetu amekuwa mshiriki wa Mikutano ya Kimataifa ya Mazingira. Mara zote ameyasihi mataifa makubwa ambayo kwa kiasi kikubwa yana mchango mkubwa katika mabadiliko ya tabianchi, kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia nchi hizi ambazo zinaendelea ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya ushawishi wake, mataifa makubwa kupitia Umoja wa Mataifa walikubaliana kuanzisha Mfuko wa Fidia unaitwa *Loss and Damage Fund*, kwa ajili ya kuzisaidia nchi zinazoendelea pale ambapo zinakuwa zimepata athari kama hizi zinazoendelea za mafuriko kama matokeo ya tabianchi.  Je, Serikali iko tayari kuunda kikosi kazi ambacho kitahusisha wataalam kutoka vyuo vya elimu ya juu, sekta binafsi na *NGOs* na wataalamu kutoka Serikalini ili kuona kwa namna gani sisi tunapata fedha hizo ili ziweze kutusaidia kukabiliana na athari ambazo zimetokana na mabadiliko haya ya tabianchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chumi, Mbunge wa Mufindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu imekuwa inashiriki mikutano mingi na pia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshiriki mikutano mingi, pia Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango ambaye ndiye mwenye ofisi yenye dhamana ya mazingira ameshiriki mikutano hii. Serikali tumeihakikishia dunia kwamba na sisi tuko kwenye mchakato na mpango unaoweza kudhibiti uharibifu wa mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuunda chombo, tayari Wizara ya Mazingira ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayo timu ambayo inafanya kazi wakati wote pamoja na Idara ya Mazingira kuhakikisha kuwa inakuwa na mipango ya sasa endelevu ambayo itawezesha Serikali yetu kutambua na kubaini maeneo ambayo yanahitaji kuimarishwa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

Pia tathmini na tafiti mbalimbali zimekuwa zinafanyika ili ziweze kutuongoza Serikali katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpango huu unaoendelea ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni endelevu kwa sababu tunahitaji kuelimisha umma na tunaona ghasia za mabadiliko ya tabianchi zinazojitokeza kwenye maeneo yao. Lengo hapa ni kupitia tafiti hizo zinazofanywa na kikosi kazi hicho ambacho tayari kimeshaundwa, tutaona mahitaji zaidi ili tuongeze vikosi kazi kulingana na mahitaji yenyewe. Lengo ni kufikia hatua nzuri ili Taifa letu tuwe kwanye nafasi ya kuhifadhi mazingira na kuepusha majanga yanayoweza kujitokeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni kweli kwamba Taifa limekutwa na janga la mafuriko na mikoa mbalimbali imeathirika na mafuriko haya ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, pale kwenye Jimbo la Kibiti tuna kaya takriban 6,150 zimeathirika, idadi ya watu takriban 31,900, lakini sambamba na hilo ekari zilizokuwa zimesambaratishwa na mafuriko haya ni takriban ekari 71,366. Tukizingatia kwamba wananchi hawa wanategemea sana kilimo; je, nini mkakati wa Serikali mara baada ya hali hii ya mvua kuwa imepungua, kuweza kuwasaidia wananchi hawa wa Jimbo la Kibiti pamoja na Rufiji kuweza kupata mbegu ili kuendelea na masuala ya kilimo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampa pole, miongoni mwa wilaya ambazo zimepata athari kubwa ni Wilaya ya Kibiti, eneo la *delta*. Kwa bahati nzuri eneo lile nalifahamu, nimeishi pale, nimefanya kazi pale na athari hii tumeitembelea na tunazo taarifa ofisini kwetu. Kwa hiyo, pole sana Mheshimiwa Mpembenwe na wananchi wote ambao wamepata athari kwenye eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na Taifa zikiendelea kuratibu utoaji misaada kwenye maeneo yote ikiwemo Kibiti bado pia tumeweka mpango imara wa kuhakikisha kwamba baada ya utulivu wa hali ya hewa sekta zetu zote ambazo zinaguswa na maafa yale; miundombinu, Wizara ya Kilimo, mashamba na maeneo ya mifugo, sekta ya afya kama kulitokea mlipuko wa magongwa baada ya uwepo wa maji mengi yaliyopita katika maeneo mbalimbali. Wizara hizi zina mpango kazi kupitia Kamati ya Kitaifa ya Maafa.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya jukumu ambalo sasa lipo kwa Wizara ya Kilimo kwa wakulima wale ni kwamba tumeshaandaa mbegu. Tulitoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais kiwango cha tani ambazo tumeamua tuzipeleke kwenye eneo lile. Rufiji tumeona mazingira hayo wakulima walikuwa wanalima mazao gani, tumeandaa mbegu za kutosha kwa ajili ya kuwawezesha kuanza kulima tena. Kwa kuwa eneo lile ni chepechepe, tunaamini bado wanaweza wakalima mazao ya muda mfupi na yakaiva. Tumeamua kupeleka mpunga ili waweze kurudisha mashamba ya mpunga kwenye maeneo hayo chepechepe, mazao kama mahindi na mazao mengine ambayo ni ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaratibu wote umeandaliwa na timu yetu iko pale Kibiti, Rufiji na maeneo mengine ambayo yamepata athari, wanaendelea kuratibu na kufuatilia mwenendo huo. Mwisho, kila hatua inayofikiwa wale watakuwa wanatupa taarifa. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge na yeye atakuwa anatupa mrejesho wa huduma zinazoendelea kutolewa pale ili tushirikiane na wananchi wale

waweze kurudi kwenye hali yao ya kawaida. Huo ndiyo Mpango kazi wa Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali na tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 178

**Mikopo ya Halmashauri Kutolewa kwa Wajasiriamali Mmoja Mmoja**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya mikopo ya 10% inayotolewa na halmashauri kutolewa kwa mjasiriamali mmoja mmoja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mikopo ya 10% inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, Kifungu cha 37A. Kifungu hicho kimeeleza namna halmashauri zote zinavyopaswa kutenga 10% ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaufanyia tathmini utaratibu wa mikopo ya 10% kutolewa kwa mjasiriamali mmoja mmoja ili kuona tija na ufanisi wake ili ikibidi maboresho yafanyike. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Serikali imeona kwamba ipo haja ya kufanya tathmini ili kuweza kukidhi uhitaji wa kukopesha mjasiriamali mmoja mmoja, sasa nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; je, tathmini ambayo wanategemea kufanya, itakwenda sambamba na maboresho ya mikopo hii yanayoendelea hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali itatuletea marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ili iweze kukidhi haja ya kukopesha mjasiriamali mmoja mmoja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba Serikali inaona umuhimu wa kufanya mapitio na kuona uwezekano wa kukopesha mjasiriamali mmoja mmoja badala ya vikundi na hilo litafanyiwa tathmini na kuona ufanisi na uwezekano wake wa kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa watu wenye ulemavu wanapata mikopo ya 10% hata akiwa mtu mmoja mmoja; kwa hiyo makundi yaliyobaki ni ya vijana pamoja na wanawake. Kwa hiyo tutalifanyia tathmini suala hilo. Suala hili tutalifanya baada ya kupitia sheria yetu ya mikopo ya 10%, baada ya maboresho ya mikopo hii ambayo inatarajiwa kuanza mwezi Julai mwaka huu wa fedha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 179

**Kukarabati Kituo cha Afya cha Nhobola – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini Kituo cha Afya cha Nhobola kitafanyiwa ukarabati baada ya kuwa chakavu kwa kipindi kirefu ikiwa ni pamoja na upanuzi wa kituo hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Nhobola ni miongoni mwa Vituo vya Afya 202 kongwe ambavyo vinahitaji ukarabati mkubwa ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itavifanyia ukarabati vituo hivyo kwa awamu kikiwemo Kituo cha Afya Nhobola katika Halmashauri ya Kishapu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nitoe shukrani kwa Serikali kwa taratibu na mipango iliyoiandaa kwa ajili ya kuhakikisha vituo hivi vinakarabatiwa ikiwa ni pamoja na kufanya upanuzi. Swali la kwanza; nataka tu nipate *commitment* ya Serikali, je, kwa huu mwaka wa fedha 2024/2025 unaokuja kituo hiki ni moja kati ya vituo ambavyo vitapewa kipaumbele na kukarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kituo cha Afya cha Dulisi, Mwigumbi na Ng’wang’halanga ni moja kati ya vituo ambavyo vina upungufu mkubwa wa miundombinu japokuwa vina sifa ya kituo. Je, Serikali iko tayari kuvitazama vituo hivi na kuhakikisha kwamba miundombinu muhimu iwekwe pale ikiwa ni pamoja na

wodi kwa ajili ya wagonjwa, nyumba za watumishi na mochwari katika hivi vituo vya afya vitatu nilivyovitaja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Serikali wa ukarabati wa vituo hivi vya afya tumeanza kwanza na kipaumbele cha ukarabati wa hospitali za halmashauri. Katika hospitali za halmashauri zilizoainishwa 50 tayari hospitali 39 zimeshafanyiwa ukarabati na bado hospitali 11 ambazo tunatarajia kuzikamilisha. Baada ya hapo tutakwenda kwenye ukarabati na upanuzi wa vituo vya afya vikongwe. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakapoanza ukarabati wa vituo vya afya tutahakikisha pia hiki nacho kinapewa kipaumbele, kinakarabatiwa ili kiweze kutoa huduma vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusiana na baadhi ya vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja vyenye upungufu wa baadhi ya majengo. Serikali inatambua na tumeshaelekeza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote Nchini kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu unaopungua kwa awamu. Hata hivyo, Serikali Kuu itatafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono kuhahakikisha majengo hayo yanakamilishwa, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama nimewaona moja kwa moja kwenye swali usianze na hadithi. Mheshimiwa Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Kituo cha Chikobe kitafanyiwa uboreshaji kwa sababu miundombinu yake ni mibovu sana? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Chikobe, kitafanyiwa ukarabati mara tutakapoanza kukarabati vituo vya afya baada ya kukamilisha ukarabati wa hospitali za halmashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Misha kilichopo kwenye Jimbo la Tabora Mjini hakijakamilika. Serikali ina mpango gani wa kukamilisha kituo hiki ili kiweze kuanza kufanya kazi kwa ufanisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Misha katika Manispaa ta Tabora ni moja ya vituo ambavyo vilipewa fedha na Serikali kwa ajili ya ujenzi na ni kweli kwamba hakijakamilika na tunatafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Tumemwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kutenga fedha kwenye mapato ya ndani ili kuendelea na hatua za ukamilishaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nataka nijue je, ni sahihi kituo cha afya kuwa na wodi moja inayolaza mama, baba, watoto na hata watu waliofanyiwa *operation?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ujenzi wa vituo vya afya upo kwa mujibu wa mwongozo wa ujenzi wa miundombinu hiyo, lakini pia kwa mujibu wa Sera ya Afya. Vituo hivi vinajengwa wodi ya wanawake, wodi ya wanaume, wodi ya watoto lakini pia wodi ya wazazi, majengo

ya upasuaji na majengo mengine. Kwa hiyo, siyo sahihi kwamba tunaweza tukawa tuna wodi moja ambayo inatumika na watoto, wanaume na wanawake jambo hilo halikubaliki. Kwa kweli nina uhakika kama kuna sehemu inafanya hivyo, tutachukua hatua kwa haraka, kwa sababu ni suala ambalo halipo katika utaratibu wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Vituo vya Afya, Kata ya Kala, Kata ya Ninde na Kata ya Kate, Wilayani Nkasi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, vipo vituo vya afya ambavyo bado havijakamilika kikiwemo Kituo cha Afya cha Ninde na vingine ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Nimhakikishie tu kwamba Serikali imeshaweka mkakati wa kwenda kukamilisha vituo hivi kwa awamu kwa sababu, tumejenga vituo vingi, tunakwenda kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba muda utafika, tutakwenda kukamilisha vituo hivyo ambavyo amevitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itafanya ukarabati na upanuzi Kituo cha Afya Masama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Saashisha amekitaja ni miongoni mwa vituo vya afya 202 ambavyo vipo kwenye

mpango wa vituo kongwe vya kukarabatiwa na kuongezewa majengo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Wilaya ya Nkasi, Kata ya Itete ina vijiji vinne na havina kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Itete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tulikwishaelekeza halmashauri kuainisha maeneo ya kimkakati ya kata zile ambazo zinakidhi vigezo vya kuwa na vituo vya afya kwa kuzingatia idadi ya wananchi, umbali kutoka kituo cha afya cha Jirani, lakini pia hali ya kijiografia ya eneo hilo. Kwa hiyo, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutawasiliana na Halmashauri ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa tuweze kuona kama wanakidhi vigezo, baada ya hapo tuweke mipango ya ujenzi wa kituo hicho, ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la myongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itafanya ukarabati na upanuzi katika Kituo cha Afya Mkwedu kilichopo Jimbo la Newala Vijijini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba twende tukakifanyie tathmini kituo hiki cha afya katika Halmashauri ya Newala Vijijini ili tuweze kuona kiasi cha fedha kinachohitajika na tuweke mipango ya kwenda kukarabati, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kuuliza, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Msandamuungano?

**SPIKA:** Ulikuwa hujawasha kisemeo, japokuwa umesikika lakini sina uhakika kama Taarifa Rasmi za Bunge, zitakuwa na hilo swali.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Msandamuungano? Nakushukuru.

**SPIKA:** Hakijawaka, japokuwa sauti yako inasikika.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, kimewaka.

**MBUNGE FULANI:** Hakijawaka tumia hiki.

**SPIKA:** Hebu nenda kinachofuata.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Msandamuungano, kilichopo ndani ya Jimbo la Kwela? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Sumbawanga Vijijini kutuma wataalamu pale, Mganga Mkuu wa Halmashauri na *engineer* kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika, lakini pia kuanza kuandaa bajeti kupitia mapato ya ndani na kuleta maombi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo hicho. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Lunguya? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Iddi Kassim amekitaja tutakwenda pia kukitafutia fedha tuweze kukikarabati kwa awamu, lakini pia kuongeza majengo ambayo yanapungua, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakamilisha Kituo cha Afya kilichopo Kata ya Itale, Wilaya ya Ileje ili wananchi waweze kupata huduma iliyokusudiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo hivi vya afya, vipo vituo ambavyo vimepata milioni 500, lakini vipo ambavyo vimepata milioni 250.

Kwa hiyo, nitaonana na Mheshimiwa Mbunge kujua kituo hiki kilipata shilingi milioni 250, kinasubiri shilingi milioni 250 au kama kilipata milioni 500, tujue kwa nini majengo hayajakamilika na baada ya hapo tutafute fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 180

**Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela Kutopandishwa Hadhi**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, vikwazo gani vinasababisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela usipandishwe hadhi kuwa Halmashauri ya Mji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji na umuhimu wa kuanzisha maeneo ya kiutawala ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na (Mamlaka za Miji), Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela ilianzishwa mwaka 2008. Serikali itakapoanza utekelezaji wa kuanzisha maeneo mapya ya kiutawala itaifanyia tathmini mamlaka hiyo na kuendelea na hatua za kuipandisha hadhi ikiwa itakidhi vigezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, mamlaka hii ina zaidi ya miaka 16 na leo hapa tunapata majibu ambayo ni *too general* na hayaoneshi matumaini ya kwamba ni lini sasa mamlaka hii itapandishwa. Nina maswali mawili. Swali la kwanza; madiwani zaidi ya 14 hawana KAMAKA (Kamati za Maendeleo) wanaelea na kumeingia mgogoro wa maslahi ambapo Wenyeviti wa Vitongoji na Madiwani hawawezi kukaa pamoja kirahisi na

kufanya maendeleo, je, Serikali inafikiria nini kwenye jambo kama hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Halmashauri ya Wilaya ya Kyela inaendesha mabaraza mawili kwa wakati mmoja, Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo na Baraza la Halmashauri ya Madiwani pale Kyela. Je, Serikali haioni ni wakati sahihi kuzisaidia pesa halmashauri zilizo katika hali hiyo ili ziweze kuendesha hayo mabaraza mawili kwa wakati mmoja? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inatambua uwepo wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela kwa kipindi cha takribani miaka 16. Kwa kipindi hicho chote mamlaka ile haijawahi kukidhi vigezo vya kuwa halmashauri ya mji ikiwemo idadi ya wananchi, ukubwa wa kijiografia wa eneo husika pamoja na vigezo vingine. Walishawahi kuleta maombi hayo, Serikali ilifanya tathmini na kuwapa maelekezo ya kwenda kufanya maboresho. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba tunahitaji kupata halmashauri ya mji lakini tunasubiri kwanza vigezo viweze kutimia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, tunaelekeza Wenyeviti na Madiwani wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela na Baraza la Madiwani, waweze kufanya kazi kwa ushirikiano na ni kazi ya Mkurugenzi na Viongozi wote wa Serikali kuhakikisha kwamba wataalam hawa, watendaji hawa na viongozi hawa wa vijiji na kata wanafanya kazi kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na Serikali kupeleka fedha za ziada kwa ajili ya kuendesha Baraza la Mamlaka Mji Mdogo na Baraza la Madiwani. Suala hilo linatokana na mapato ya ndani ya halmashauri. Kwa hiyo, nisisitize kwamba Halmashauri ya Kyela kupitia mapato ya ndani waendelee kuhudumia pia Mamlaka ya Mji Mdogo mpaka pale mamlaka

hiyo itakapopandishwa hadhi au itakapoondolewa kwenye orodha ya Mamlaka za Mji Mdogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 181

**Kupeleka Mashine ya *X-Ray* Hospitali ya Manispaa ya Mpanda**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mashine ya *X-ray* katika Hospitali ya Manispaa ya Mpanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma za uchunguzi za radiolojia kwa kusimika mashine za *X-ray* na *ultrasound* katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ya Msingi nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2022/2024, jumla ya mashine 280 za kidigitali za *X-ray* na mashine za *ultrasound* 322 zimenunuliwa na kusimikwa katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imepeleka mashine tatu za *X-ray* katika Mkoa wa Katavi ambapo zimefungwa katika Halmashauri ya Mpimbwe, Mlele, Nsimbo. Aidha, Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda iko kwenye orodha ya vituo vitakavyopelekewa mashine za *X-ray* awamu inayofuata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kapufi anashukuru sana kwa jitihada ambazo zinafanywa na Serikali, lakini, nina swali moja la nyongeza, Kituo cha Afya cha Ushetu kimeboreshwa na kimekarabatiwa lakini hakina *digital X-ray*. Je, ni lini Serikali itapeleka *digital X-ray* katika Kituo cha Afya cha Ushetu, kilichopo Jimbo la Ushetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua uhitaji wa huduma za afya katika Kata ya Ushetu ilikarabati Kituo cha Afya cha Ushetu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunaelekea kupeleka mashine ya *digital X-ray* kwenye vituo vyote vilivyopanuliwa na kujengewa majengo ya *X-ray* kikiwemo Kituo hiki cha Ushetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tanganyika hatuna kabisa mtaalamu wa *X-ray*. Je, ni lini Serikali itapeleka mtaalamu huyo ili kuwasaidia wananchi waweze kupata huduma zilizokusudiwa? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upungufu wa Wataalam wa *X-ray* na *Ultrasound* kwenye vituo vyetu vya huduma hususani ngazi ya afya ya msingi. Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari tumeshaanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Wataalam wa *X-Ray* na *Ultrasound* ili kuhakikisha kwamba hospitali zote zenye mashine hizo zinapata wataalam kwa ajili ya huduma hiyo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Kituo hicho cha Afya lakini pia Halmashauri ya Tanganyika itapelekewa Wataalam wa

*X-Ray* na *Ultrasound* ili kuhakikisha kwamba huduma zinatolewa vizuri, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu, ni lini Wizara itapeleka *X-Ray* katika Kituo cha Kamsamba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba baada ya hivi vituo vya afya kukamilika na kujengewa majengo maalum ya *X-ray* vinatafutiwa fedha na kupelekewa vifaa vya *X-ray* kwa maana ya mashine za *X-ray* kwa ajili ya huduma hizo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kukamilisha jengo la *X-ray* tutahakikisha tunatafuta fedha kwa ajili ya kupeleka mashine ya *X-ray*, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Hospitali za Wilaya za Mkoa wa Simiyu tumepata mashine za *X-ray,* lakini hatuna wataalam, je, ni lini Serikali itatuletea wataalam wa *X-Ray*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoa wa Simiyu na halmashauri zake ni moja ya mikoa ambayo ina upungufu mkubwa wa Wataalamu wa Huduma za Mionzi ikiwemo *X-Ray* na *Ultrasound*. Nimhakikishie tu kwenye kibali cha ajira ambacho kitatangazwa hivi karibuni tutaupa kipaumbele Mkoa wa Simiyu pamoja na halmashauri zake kupata wataalam wa *X-Ray,* ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italeta huduma ya *X-ray* katika Kituo cha Afya cha Mkuyuni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba Kituo cha Afya cha Mkuyuni bado hakina jengo la *X-ray* na majengo haya ni maalum kwa sababu mashine zile ni mashine za mionzi. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Morogoro kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo maalum kwa ajili ya mashine ya *X-ray* na baada ya kukamilisha tutapeleka mashine ya *X-ray* kwa ajili ya huduma hizo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.182

**Kukamilisha Kusambaza Umeme wa *REA* Vijiji 20 Vilivyobaki Mkalama**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme wa *REA* kwenye vijiji 20 vilivyobaki – Mkalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mkalama lina vijiji 70 na vyote vimepatiwa umeme, vikiwemo vijiji 25 vilivyokuwa katika Mradi wa Kusambaza Umeme, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, uliotekelezwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*. Aidha, Jimbo hilo lina vitongoji 388 ambapo vitongoji 192 vimepatiwa umeme na vitongoji 196 bado havijapatiwa umeme. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia *REA* imetenga fedha za kutekeleza mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 vya kila jimbo ikiwemo Jimbo la Mkalama. Kwa sasa, *REA* inakamilisha taratibu za kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza mradi huu. Vitongoji vitakavyobakia vitapatiwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nishukuru Serikali kwa kutupatia umeme kwenye vijiji vyote 70, lakini changamoto kubwa iliyopo ni *size* ya *transformer* zilizofungwa. Wamefunga *size* ya *transformer kVA* 50 na mahitaji ni makubwa, wananchi wana viwanda vya alizeti na viwanda vya kuchomelea. Swali la kwanza; je, Serikali haioni kuna haja ya kufunga *transformer* za *kVA* 200 mpaka 345 ili kupata umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nimesikia Serikali kwamba wako kwenye hatua za kutafuta wakandarasi kwa ajili ya kutengeneza kwenye vitongoji. Kumekuwa kuna kasumba miaka yote ya kupata wakandarasi wasiokuwa na sifa. Nataka kujua Serikali wamejipanga vipi kuhakikisha katika eneo la *due diligence* hawafanyi makosa? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tumepokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge na maoni ya Waheshimiwa Wabunge wengi na kwa hivyo tumefanyia kazi, kuanzia mwaka huu unaokuja wa fedha 2024/2025, tutaongeza ukubwa wa *transformer*. Zitakuwepo *transformer* za ukubwa wa *KVI* 50, *KVI* 100 na *KVI* 200 na zitafungwa kulingana na mahitaji ya

eneo husika. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, jambo hilo tumelipokea na lipo tayari kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wakandarasi wanaosuasua kwenye miradi; maelekezo ya Serikali, kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, yalishatoka. Hatutawavumilia wakandarasi wote wanaotekeleza miradi kwa kusuasua na kutoendelea mbele, kupitia Taasisi zetu za *TANESCO* na *REA* hatutawapatia kazi wakandarasi wanaosuasua katika miradi yetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Wilayani Rungwe vijiji saba mpaka sasa hivi havijafikiwa na umeme wa *REA*. Vijiji hivyo ni Mpindo, Kata ya Bulyaga; Isumba Kata ya Kinyala; Kyobo Juu, Kata ya Ikuti; Ngumbulu, Kata ya Isongole; Mpombo, Kata ya Lupepo; Isabula, Kata ya Kisiba; na Kasanga, Kata ya Mpombo. Je, ni lini vijiji hivyo vitapata umeme wa *REA*? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, katika vijiji vyote hivi saba vilivyopo katika Jimbo la Rungwe mkandarasi yuko *site*. Namhakikishia kwamba, tutaongeza usimamizi kuhakikisha vijiji hivi vinapatiwa umeme kulingana na mikataba yetu ambayo ni Juni, mwaka huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, tutasimamia vizuri na tutahakikisha wananchi wa Jimbo la Rungwe wanapata umeme katika vijiji hivi saba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kumaliza kuweka umeme katika vijiji vyote 70 vya Mkalama. Naomba *commitment* ya Serikali kuhusu vitongoji 15 ambavyo nimeviombea umeme, ni lini umeme utawashwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, vitongoji hivi 15 katika Jimbo la Mkalama na katika majimbo yote, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na ninalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tupo katika hatua za manunuzi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, hivi karibuni tutakamilisha na tutaenda kwenye utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 katika kila jimbo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itasambaza umeme kwa bei ya vijiji katika Kata ya Katindiuka, kama ilivyokuwa imeahidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote ambayo tunatekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini bei ya kuunganisha umeme ni 27,000. Katika maeneo ya vijiji-miji ambako bei ni zaidi ya hiyo, tunaendelea kufanya mkakati wa kuona namna ambavyo tunaweza tukaenda kwa ajili ya ku-*incorporate* hata wananchi ambao hawana uwezo wa kulipa 321,000, lakini katika maeneo yote tunayotekeleza miradi yetu ya vijiji bei ya kuunganisha umeme ni 27,000 na tutaendelea kufanya hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, je, ni lini Serikali itamaliza kusambaza umeme katika vijiji vilivyobaki katika Mkoa wa Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, katika vijiji ambavyo vimebakia katika Mkoa wa Singida wakandarasi

wanaendelea na kazi ya kufikisha umeme kwenye vijiji hivyo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kusimamia kwa weledi mkubwa sana ili vijiji vilivyobakia viweze kupata umeme kwa wakati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa twende Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, sasa aulize swali lake.

Na. 183

**Ujenzi wa Chuo cha Uvuvi na Mifugo Kata ya Igamba - Mbozi**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Chuo cha Uvuvi na Mifugo utaanza katika Kata ya Igamba, Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya mifugo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada hutolewa na Wakala wa Mafunzo ya Mifugo *(LITA)* kupitia kampasi zake nane na vyuo binafsi 12 vinavyotambuliwa na Serikali. Aidha, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, mafunzo ya uvuvi hutolewa na Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi *(FETA)* kupitia kampasi zake tatu na vituo vya mafunzo viwili.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Mafunzo ya Mifugo *(LITA)* imepanga kujenga kampasi ya kutoa mafunzo ya mifugo katika Kata ya Igamba, Wilaya ya Mbozi, Mkoani Songwe. Ujenzi wa Kampasi ya Igamba, Mbozi, utagharimu takribani kiasi cha shilingi bilioni 15 ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia *LITA* imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya

kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi. Aidha, ujenzi kwa awamu ya kwanza utahusisha ujenzi wa jengo la utawala, hosteli ya wanafunzi na ukumbi wa mihadhara.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuongeza majengo ya chuo hicho kadiri itakavyopata fedha za maendeleo ili kuhakikisha ujenzi na usimikaji wa miundombinu yote ya mafunzo inayohitajika unakamilika na kampasi hiyo kuanza kutoa mafunzo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo tumefikia, lakini mpaka jana tunaongea, mkandarasi amepokea shilingi milioni 50 tu kati ya fedha zote hizo alizoomba. Sasa swali langu la kwanza ni hili; ni lini sasa Serikali itakuwa *serious* kuhakikisha kwamba, fedha zote anazohitaji mkandarasi zinaenda kwa sababu wananchi wa Igamba wanakisubiri kwa hamu sana chuo hiki?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari sasa kuongozana na mimi kwenda Igamba, Mkoa wa Songwe, akaangalie kinachoendelea pale? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Mifugo tumetimiza wajibu wetu. Tumeomba fedha Wizara ya Fedha na tayari *documents* zote ziko Wizara ya Fedha na mara tutakapopata fedha, tutapeleka kwenye ujenzi wa chuo hicho. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha zitakapokuwa tayari tutazipeleka kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, la pili la kutembelea chuo hiki; Wizara iko tayari, mimi au Mheshimiwa Waziri tuko tayari, kutembelea

chuo hicho na kama kuna mapungufu ama changamoto zozote tuko tayari kwenda kuzitatua, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 184

**Hitaji la Fedha na Wataalam kwa ajili ya Ufugaji wa Samaki katika Vizimba, Kata ya Manda**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha na wataalam katika eneo la Mbongo, Kata ya Manda ambalo linafaa kwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika ziwa ni lazima kuzingatia vigezo vya kisheria na kitaalam, ikiwemo kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira *(Strategic Environmental Assessment)*. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, kupitia Progaramu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP II),* Serikali imetenga kiasi cha shilingi 233,500,000 kwa ajili ya kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(TAFIRI)* kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira, ambayo ni takwa la kisheria katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa yakiwemo maeneo ya Manda ili kutambua maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini kukamilika, maeneo yatakayobainika kuwa yanafaa kwa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba yataingizwa kwenye Bajeti na Mpango wa Wizara wa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuwezesha upatikanaji wa fedha na wataalam katika eneo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Taasisi ya Uvuvi na Utafiti kwa kuweza kuendelea na mchakato wa kubaini maeneo yanayofaa kwa ajili ya ufugaji wa samaki wa vizimba. Swali langu la kwanza; ni lini Serikali itamaliza mchakato huo ili wananchi wa Ludewa wapate fursa ya kuendelea na biashara hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Wizara ina mkakati gani wa kufanya utafiti katika maeneo ambayo ni mazalia ya samaki kwa lengo la kuhifadhi na kufanya samaki waendelee kuwa wengi katika Ziwa Nyasa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, tumepokea *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, tutaiweka katika bajeti ya 2024/2025 ili kwenda kufanya tathmini katika eneo hilo analolizungumza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, namna gani ya kuongeza uzalishaji wa samaki; kama nilivyosema katika majibu ya msingi kwamba, Serikali sasa imekuja na mpango wa vizimba na tunazidi kuhamasisha wavuvi wajikite zaidi katika vizimba kwa sababu, uvuvi huu wa sasa umebadilika duniani kote, kwamba sasa tunakwenda katika hali ya kutengeneza vizimba ili kuleta tija zaidi katika uzalishaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu katika Maziwa yetu yote makubwa Nyasa, Victoria na Tanganyika, ukweli ni kwamba, mazalia ya samaki yanapotea kwa sababu ya wingi wa watu na uvuvi haramu. Kwa hiyo, ni lazima tuje na mkakati mpya ambao utawezesha watu wetu kuendelea na uvuvi wa kisasa zaidi, hasa kwenye vizimba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, aulize swali lake.

Na. 185

**Kurejesha Kiwanda cha Chai cha Wakulima wa Lupembe Muvyulu**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha Kiwanda cha Chai cha Wakulima wa Lupembe, Muvyulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mwezi Januari, 2024, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilianza kufanya tathmini ya mali za Kiwanda cha Chai cha Wakulima, Lupembe, kwa ajili ya kumlipa mwekezaji *(Dhow Mercantile East Africa Limited)* fidia kulingana na thamani halisi ya mali za kiwanda kabla ya kukirejesha kwa Wakulima wa Lupembe (MUVYULU). Kazi hiyo ya tathmini inatarajiwa kukamilika kabla ya Mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa kazi hiyo kutawezesha mwekezaji huyo kulipwa fidia kulingana na makubaliano yaliyofikiwa baina ya mwekezaji huyo na Chama cha Ushirika cha Muvyulu ambapo Serikali itarejesha kiwanda hicho kwa wakulima wa zao la chai, Lupembe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kumaliza huu

mgogoro wa Kiwanda cha Lupembe ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 20 sasa. Kwa hivyo, sasa hivi tuko hatua ya mwisho, ni hatua nzuri kwa Serikali, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri. Swali la kwanza; kwa kuwa, kiwanda hiki ni kiwanda cha muda mrefu cha tangu mwaka 1958 mpaka leo, kwa hiyo, mitambo mingi imechakaa. Je, kitakaporejeshwa kwa wananchi, Serikali iko tayari kuwakopesha Wakulima wa Chai, Lupembe, fedha kupitia Mfuko wa Kilimo ili waendeshe kiwanda hiki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, Wakulima wa Chai Lupembe, baadhi wana madai kwa mwekezaji na wapo baadhi ya wafanyabiashara, pia wana madai kwa mwekezaji na mwekezaji huyu anakusudia kuondoka baada ya kulipwa fidia. Je, ni nini Kauli ya Serikali kwenye madeni ya wakulima ambao hawajalipwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, baada ya kiwanda kurudishwa kwa wananchi, Serikali itakuwa tayari kutoa mkopo kupitia Benki ya *TADB* ili kuweza kukifufua kwa kuweka mitambo mipya ili kiweze kufanya kazi kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai kwamba, sehemu ya tathmini inayofanyika kabla ya kumlipa maana yake unapofanya tathmini ni pamoja na kuangalia madeni ambayo wanalipwa, kwa hiyo, itakuwa ni sehemu ya huo mchakato mzima. Kwa hiyo, wananchi watalipwa kabla ya kiwanda hiki kurejeshwa kwa wakulima, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya miezi miwili sasa Viwanda vya Chai vya Ambangulu na Dindira

vimefungwa na wananchi hawana maeneo ya kupeleka chai. Ni nini Kauli ya Serikali kuwasaidia wananchi hawa, ili waweze kuendelea na shughuli zao za kilimo na uzalishaji?  Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameieleza na kwamba, Wizara ya Kilimo tumeshawaandikia wawekezaji wote akiwemo mmiliki wa Kampuni ya *Mohamed Enterprise* kwanza kufungua hicho kiwanda.

Mheshimiwa Spika, pili, tunaendelea na mazungumzo kama ambayo tunafanya katika Halmashauri ya Lupembe kuhakikisha kama ameshindwa uendeshaji. Maana yake viwanda hivi sisi kama Serikali tutakuwa tayari kumlipa fidia ili kuvirejesha kwa wananchi ili waweze kuviendesha wenyewe kupitia vyama vya ushirika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 186

**Ukarabati wa Mabwawa ya Umwagiliaji Nachingwea**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Mabwawa ya Naipingo, Chemchem, Mkumba, *Farm Four* na *Eight*, Ntila na JKT Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kubaini na kufanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya umwagiliaji yakiwemo mabwawa na

skimu za umwagiliaji nchini. Kipaumbele kimeelekezwa katika maeneo makubwa yanayohusisha wakulima wengi na kwa yale yanayohusisha wakulima wachache. Serikali imejikita zaidi kuendeleza kwa kuchimba visima ambapo kisima kimoja kinaweza kuhudumia ekari 40.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni miongoni mwa maeneo yenye hekta chache ambapo Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kuchimba visima katika Skimu ya Ntila. Aidha, kwa Mabwawa ya Naipingo, Nkumba, Chemchem, *Farm Four* na *Eight*, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kuyabaini kwa kushirikiana na Ofisi ya Mbunge na Halmashauri ili nayo yafikiwe kadri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la JKT Nachingwea ni miongoni mwa mabwawa yaliyopo chini ya Jeshi la Kujenga Taifa ambalo ndilo linaloratibu uendelezaji na usimamizi wake. Hivyo, nitawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili kulikarabati bwawa hilo, chini ya uratibu wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kutokana na majibu ya Waziri amesema kwamba, Kisima cha Ntila kitaanza kuchimbwa mwaka huu wa fedha na najua imebaki miezi miwili tu. Je, ni lini hasa kisima hiki kitachimbwa au kimeshachimbwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kutokana na majibu ya swali la msingi. Je, Waziri yuko tayari sasa kuongozana na Mheshimiwa Mbunge wangu wa jimbo hilo ili aende akabaini maeneo haya kulingana na majibu aliyojibu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha unaoisha Juni, imebaki miezi

miwili na kwamba, hatua iliyopo sasa hivi ni kwamba, tunatafuta mkandarasi kwa ajili ya kuchimba, maana yake tenda ilikuwa imetangazwa. Kwa hiyo, tukishamaliza maana yake tutasaini mkataba na kazi itaendelea, kikubwa tu ni kwamba, kazi lazima ianze katika mwaka huu wa fedha..

Mheshimiwa Spika, kuhusu utayari wa mimi kufika; niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwenda kujionea kazi nzuri ambayo imefanywa huko na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini na kujionea changamoto chache ambazo zinahitaji ufumbuzi. Kwa hiyo, niko tayari, ahsante sana

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

Na. 187

**Kuunganisha Kodi ya Jengo na Kodi ya Ardhi**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, kwa nini Kodi ya Jengo na Kodi ya Ardhi zisiunganishwe na kuwa moja ili kumwondolea usumbufu mwananchi?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi inaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya mifumo ya kodi, ada na tozo za huduma kwa lengo la kuondoa urasimu na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Tathmini hiyo inajumuisha mapendekezo ya maboresho ya mfumo wa usimamizi wa kodi ya jengo na kodi ya ardhi kama inavyopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, Serikali inaandaa mfumo wa kielektroniki wa kutoa ankara ya pamoja kwa huduma zinazolandana ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaostahili kulipa kodi ya jengo na kodi ya ardhi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya ziada.

Swali la kwanza, kwa kuwa suala la utafiti ni suala linalochukua muda, je, Serikali inaweza ikawaambia wananchi ni lini wanategemea kumaliza utafiti huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu mifumo ni jambo kubwa, je, Serikali iko tayari kuendelea kutoa taaluma zaidi kwa wadau ambao wanasumbuka sana na mifumo hii? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zahor, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathimini hiyo ni sehemu ya maandalizi ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Fedha wa mwaka 2024 ambao unatarajiwa kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu ndani ya mwaka huu na Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali kupitia taasisi zake imekuwa na utamaduni na imekuwa na desturi ya kutoa mafunzo siku hadi siku kwa wadau wanaostahiki, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta matangazo tuliyonayo hapa mbele kisha tutaendelea na ratiba yetu.

Kwanza ni tangazo la wageni na tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, yupo mgeni wa Mheshimiwa Judith Kapinga ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati, Ndugu Paul Kaunda ambaye ni mume wake, karibu sana. Haya ahsanteni sana, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga**,** Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, yupo Ndugu Francis Kiwanga ambaye ni Mkurugenzi wa *Foundation for Civil Society* anayemaliza muda wake; yupo Ndugu Justice Rutenge, Mkurugenzi Mpya wa *Foundation for Civil Society;* yupo pia Ndugu Nicholas Mhozya, Afisa Programu Mwandamizi Kituo cha AZAKI Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao ni wageni wenu.

Wabunge mnaozungumza, nimesimama, ahsante sana.

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambaye ni Naibu Spika, hawa ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT),* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Yahya Omary Massare ambao ni walimu na wafanyakazi wa Shule ya Sekondari *St. Margreta Naseau* kutoka Itigi, Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Mthamini *(Valuer)* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni wadau wa utalii kutoka Kampuni ya *Vocational Awaits* ya Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni familia yake kutoka Mbozi, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 105 na walimu kumi kutoka Shule ya Msingi *Gloryland* iliyoko Suye, Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Elimu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Watanzania wawili wafanyabiashara kutoka nchini Uingereza, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawaalika katika Sherehe ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho hayo yatafanyika tarehe 26 Aprili, 2024, siku ya Ijumaa katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam kuanzia saa 1.00 asubuhi mpaka saa 7.00 mchana na baadaye kufuatiwa na Dhifa ya Kitaifa itakayofanyika katika Viwanja vya Ikulu saa 8.00 mchana. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanaotarajia kuhudhuria maadhimisho hayo wanaombwa kuchukua kadi maalumu kwa ajili ya zoezi hilo katika eneo la mapokezi lango *A*, kadi zenu ziko hapo kwa wanaotarajia kwenda kuhudhuria maadhimisho hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo majina hapa ya Wabunge walioomba kuchangia. Wabunge wanaotoka Chama Cha Mapinduzi watachangia kwa dakika saba. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Angeline Lubala Mabula na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, mwaka 1987 Marehemu Baba wa Taifa alipokuwa akihutubia Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama chake Cha Mapinduzi alisema; "Tatizo kubwa la Afrika si ukosefu wa rasilimali bali tatizo kubwa la nchi za Kiafrika ni matumizi sahihi ya rasilimali walizopewa na Mwenyezi Mungu." Maneno haya ya Mwalimu yananifanya nitafakari sana juu ya namna tunavyosimamia uchumi wa gesi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kusikia mipango ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya gesi asilia tangu nilipoingia kwenye Bunge hili Tukufu mwaka 2010. Ni kama miaka 14 hivi na kwa bahati mbaya hatujaweza kutekeleza kikamilifu mipango hiyo ya kutekeleza uchumi wa gesi kama tulivyodhamiria. Nitaeleza jinsi tunavyopoteza fursa mbalimbali za kiuchumi kadiri tunavyoendelea kuchukua muda mrefu kutekeleza mipango hiyo ya uchumi wa gesi na nitatoa mifano kwenye maeneo manne.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza, nchi yetu inatumia takribani 50% ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza mafuta kutoka nchi za nje. Kama tungefanya maamuzi kwa wakati

mwafaka tukatekeleza miradi ya kuanzisha nishati ya gesi kwa ajili ya matumizi ya magari na mitambo bila shaka tungepunguza sana matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza mafuta kutoka nje. Jambo hili lingekuwa na maslahi mapana sana kwa ajili ya uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, hivi sasa vitendo vya ukataji miti vinaendelea kwa kasi sana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, hata katika ripoti ya Waziri Mkuu amelisema jambo hili. Naamini kama tungetekeleza miradi hii na mipango ya uchumi wa gesi kwa wakati bila shaka tungeweza kusambaza gesi katika majumba mbalimbali ya wananchi. Sasa badala ya wananchi kuendelea kukata miti wangetumia gesi kupikia na hatimaye tungeweza kuokoa miti na kuimarisha mazingira ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, hivi sasa tunatumia 40% ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza mbolea kutoka nje na kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametubariki hazina kubwa ya gesi asilia hapa nchini. Tungeitumia gesi asilia kikamilifu tungeweza kuanzisha viwanda vya kutengeneza mbolea na tungeweza kuleta mapinduzi makubwa sana ya kilimo hapa nchini. Kwa isivyo bahati hatujalifanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne na la mwisho, hivi sasa tuna upungufu mkubwa sana wa fedha za kigeni, ningetarajia huu ungekuwa ni wakati mwafaka wa kutekeleza mradi wa muda mrefu wa kusindika gesi asilia ili tuweze kuuza nje kimiminika cha gesi ili tupate fedha za kigeni. Kwa isivyo bahati mradi huu haujatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu mradi huu umechukua muda mrefu sana na moja ya sifa kuu ya viongozi ni kufanya maamuzi kwa wakati mwafaka na kutumia fursa zilizopo. Natambua kuna haja ya kufanya majadiliano kwa umakini, lakini nina wasiwasi, kadri tunavyoendelea kuchukua muda mrefu ndivyo tunavyoendelea kupoteza fursa za kiuchumi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuzingatie mambo matatu, laiti tungeutekeleza mradi wa kusindika gesi kwa 100%, miaka mitatu iliyopita tungeweza kuitumia fursa ya vita inayoendelea kati ya Ukraine na Russia kwa ajili ya kuuza kimiminika cha gesi Nchi za Ulaya na kupata pesa za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili la tafakari, kadiri tunavyoendelea kutafakari namna tutakavyoitumia nishati ya gesi katika kuendesha mitambo na magari, wenzetu kwa mfano *Elon Musk* ameshaanza kuzalisha magari yanayotumia betri za umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu la kutafakari ni kwamba, hivi sasa kuna utafiti mkubwa sana unaoendelea katika Nchi za Ulaya wa kutumia hewa ya *nitrogen* kama chanzo kikuu cha nishati na bila shaka jambo hili likifanikiwa basi hapana shaka matumizi ya gesi asilia duniani yatapungua sana. Kwa maana hiyo Tanzania kama Taifa tutakuwa tumepoteza fursa kubwa sana ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba nimalize mchango wangu kwa kunukuu maneno aliyoyasema Hayati Baba wa Taifa; "Inawezekana, timiza wajibu wako."

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Angeline Lubala Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza ajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na muda naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na namna anavyotuongoza, lakini nitoe pongezi za jumla kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa katika Wizara hii. Mungu azidi kuwabariki kwa sababu tumeona juhudi walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na machache tu kwa sababu ya muda, kwanza niishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutangaza *tender* kwa ajili ya kuweka umeme katika visiwa. Nchi yetu ina visiwa 289 na katika visiwa 289 ni visiwa 229 vina shughuli za kibinadamu na kati ya hivyo visiwa 16 vina uwekezaji. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba umeme ulioko kule pengine ni wawekezaji wenyewe wameweka. Kwa hiyo, katika *tender* ile inaonekana ni visiwa 120 ambavyo vimetangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwa sababu nimekuwa nikiomba katika suala zima la kuweka umeme kwenye Kisiwa cha Bezi kilichopo Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Ilemela ambacho kina wakazi takribani 3,742. Wamekuwa na umeme wa *solar* kutoka kwa mwekezaji anayeitwa *PowerGen Renewable Energy* lakini alikuwa anatoza pesa shilingi elfu moja kwa saa na umeme unawaka saa 11, mwisho saa tatu usiku, lakini wakati mwingine hauji ila kesho yake inabidi utoe tena 1,000. Kwa hiyo, niishukuru sana Serikali kwa sababu itakwenda kuokoa uchumi wa wale wavuvi ambao wamekuwa wakikusanya pesa zao kwa ajili ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, napenda kuishukuru Serikali na kuipongeza sana katika suala zima la uzalishaji wa umeme. Umeme unaozalishwa, uwezo wa mitambo yetu au vyanzo vya maji ni *megawatts* 2,138 lakini mpaka sasa inazalisha *megawatts* 1,756, lakini mahitaji ambayo tuko nayo ni 1,590. Maana yake kuna *extra* lakini katika *extra* inaonekana kabisa pengine kunakuwa na changamoto za hapa na pale kulingana na mitambo na uchakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe tu Wizara, kwa sababu juhudi zinaonekana na ongezeko la uzalishaji kuingiza umeme kwenye *Grid* ya Taifa unakwenda kuwa mzuri baada ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kuanza kuingiza umeme wa *megawatts* 235 kupitia mtambo namba tisa. Nadhani tutajikuta tuna umeme wa ziada ambao tutakwenda kuhudumia nchi za jirani. Tuna imani kazi hii ikikamilika Tanzania inakwenda kuuza umeme katika nchi jirani jambo ambalo litatuletea fedha za kigeni na kufanya

mambo mengine yaende vizuri. Niishukuru sana Serikali kwa hiyo kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu nataka kuzungumzia umeme wa gesi asilia. Tuipongeze Serikali kwa wazo zuri hasa la kufanya magari yetu na mambo mengine yaweze kutumia umeme huo, lakini tayari kuna baadhi ya miji kwa mfano, Dar es Salaam umeanza kuingia katika maeneo ya nyumba zetu lakini pia na magari yanatumika. Ombi langu na rai kwa Serikali, tunahitaji kuwa na vijana wengi wanaobadilisha mfumo wa magari kwenda kwenye mfumo wa kutumia gesi, waliopo ni wachache na mahitaji ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, pia, uingizaji wa magari nchini ni vyema sasa kwa sababu tuna gesi nyingi tuone tu namna ya kuingiza magari ambayo yatakuja na mifumo tayari ambayo itakuwa imeshawekwa. Unapowekwa kwa utaratibu wetu na ujuzi wa vijana wetu kidogo hata ile hali ya mazingira kwenye gari inakuwa siyo nzuri. Kwa sababu gari limeandaliwa kuweka pengine mizigo kwa nyuma lakini unakuta ndiyo mtungi wa gesi umewekwa kule. Kwa hiyo, yale matumizi yanakuwa si sahihi sana. Kwa hiyo, tuombe kwa yale yatakayokuwa yanakuja, basi yawe na hiyo mifumo tayari imewekwa, lakini vijana waweze kupata ajira na waongezeke wale wanaokwenda kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni vituo ambavyo vinasambaza gesi hii, tuna vituo viwili tu kwa Dar es Salaam. Kipo kile kimoja cha kule *Airport* na Ubungo. Kama alivyosema Mheshimiwa Kanyasu juzi ni adha kubwa kwa sababu foleni ni kubwa, mahitaji ni makubwa, mtu anapoteza zaidi ya masaa nane anasubiri kuweka gesi. Kazi zake anafanya saa ngapi? Kwa hiyo, tuombe sana vituo viongezeke na ile kasi ya kuweka katika mikoa mingine basi waone hata ile miji mikubwa tuweze kuweka huduma hiyo kwa sababu mahitaji yatakuwa ni makubwa zaidi. Pia, tutakuwa tumesaidia sana kwa suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa

kinara wa kutaka sana kufikia mwaka 2032 tuweze kuwa na nishati safi. Kwa maana kuwa na *clean energy* katika masuala mazima ya mapishi na mambo mengine. Tumefanya juhudi kubwa Wabunge wote hapa tumesambaza mitungi ya gesi katika maeneo yetu. Bahati nzuri sana wananchi wameitikia vizuri, changamoto inakuja wanapotaka ku-*refill* zile gesi zao wanatembea mwendo mrefu sana. Matokeo yake hata ile nafuu tunayoitegemea inakuwa haipo. Tuombe sana mawakala wawepo mpaka katika maeneo ya vijijini ambako gesi hii imefika na matumizi ni makubwa. Niombe katika hilo kwa sababu namna bora ya kuweza kuwafikia hawa ni kuwapa huduma ya karibu ili waweze kuona nishati ile ni safi na salama, lakini pia ni nafuu ukilinganisha na suala la matumizi ya kuni au mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni umeme wa *REA* ambao umesambazwa katika nchi yetu na niipongeze tu Serikali kwa sababu imefikia vitongoji na vijiji vingi. Rai yangu, ile *scope* ya mwanzo katika kufikisha umeme wa REA ilikuwa ni ndogo. Matokeo yake sasa hivi watu wako kata moja, mwingine ana-*enjoy* umeme wa shilingi 27,000, mwingine anaambiwa sasa alipe 320,000 kwa sababu tu *REA* imemaliza kazi yake katika yale maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali kwa sababu ni Serikali sikivu na wananchi wanaiamini sana na ndiyo maana tunaye Rais ambaye ni msikivu na ni Rais ambaye katika kujielekeza kwake kwenye kutawala nchi hii amekuja na maridhiano, amekuja na 4R. Sasa niombe hilo hilo katika kumuenzi Mheshimiwa Rais katika ule mtazamo wake, kwa sababu maeneo yale tulishayagusa kwa umeme wa *REA* katika maeneo yote nchini na Ilemela ikiwemo, basi tuone namna yale ambayo bado yana sura ya vijiji tukamilishe tu kwa kuweka *REA* badala ya kuwa-*charge* tofauti kati ya mtu mmoja na mwingine. Hiyo itatusaidia sana katika suala zima la kupeleka huduma hiyo kwa wananchi ambao wata-*enjoy* huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala zima la usafiri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, sekunde thelathini malizia.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na naipongeza Serikali kwa kazi nzuri, lakini pia naipongeza sana Kamati yangu ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri na nakubaliana na yote ambayo yamewekwa mezani. Serikali basi ikapokee ule ushauri wa Kamati ili tuweze kwenda vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza na Mheshimiwa Mary Francis Masanja ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo iko mbele yetu. Nitumie nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kung'ara.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Morogoro Kusini kwenye upande wa umeme, mwaka huu tumeweza kupewa zaidi ya bilioni 20 kwa ajili ya kufanikisha jambo hilo. Nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. Kiuhalisia na kwa kweli nina imani kubwa na wao na naamini kwamba imani yangu kwao wataweza kumsaidia sana Mheshimiwa Rais, Mama huyu ili aweze kuifikisha nchi pale ambapo anataka ifike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Meneja wangu wa *TANESCO* wa Wilaya na Watendaji wote ambao wako chini ya Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Vilevile, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa umeme ambao tumeupata.

Mheshimiwa Spika, tunavyo vijiji 89 tunapozungumza leo hapa tayari vijiji 83 vyote vinawaka umeme na dada yangu

Kapinga tulikuwa wote katika Kata ya Lundi kwa ajili ya kuwasha umeme na hivi sasa vimebaki vijiji sita ambavyo tayari kila kitu kimekamilika isipokuwa ku-*charge* na kuviwasha. Wananchi wa Morogoro Kusini tuna kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya.

Mheshimiwa Spika, katika vitongoji ambavyo tunavyo ni 437 lakini mpaka leo hii tunavyozungumza, vitongoji 162 vina umeme na vitongoji 60 vipo katika utaratibu wa kuwekwa umeme (nguzo zimekwishasimamishwa na waya zimekwishawekwa bado kuwashwa tu). Vilevile, tuna vitongoji 15 ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kwamba vitakuja. Hivyo, tutakuwa tumebakiwa na vitongoji 200 ambavyo havina umeme. Ombi langu kwa Serikali, tuhakikishe na kuangalia tunafanya vipi ili kuhakikisha hivi vitongoji navyo vinawaka umeme ili tutakapokuwa tunakwenda kwenye uchaguzi 2025, Wanamorogoro Kusini tuseme hakika Mama Samia Suluhu Hassan, ameitendea haki nafasi ambayo amepewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo nitumie nafasi hii kuwasilisha ombi maalum kwa *TANESCO*. Sisi Halmashauri ya Morogoro Vijijini tunapata umeme kutokea Pwani lakini pia tunapata umeme kutokea Morogoro Mjini. Hatuna kituo cha kupoza umeme. Mara tu itakapotokea hitilafu, halmashauri yote inakosa umeme.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo tayari sasa hivi limekwishapeleka umeme kwenye gridi ya Taifa, tunawaomba watupatie *line* ndogo ikaunganishwe na mvua ili lolote litakalotokea, halmashauri yetu iendelee kuwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuwaomba Makao Makuu ya *TANESCO,* Ofisi ya *TANESCO* katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini wako ndani ya *container*. Ni vizuri basi Meneja wa *TANESCO* wa Morogoro *DC* akapata ofisi na gari litakalomfanya akafike katika maeneo ya mbali. Pia katika hilo suala la magari kwenye Mkoa wa Morogoro ambao ni Mkoa wa Kimkakati kwa *TANESCO*, bado tuna upungufu wa magari.

Mwaka 2023 nilisema na nikapata ahadi kwamba watafanya lakini hawajafanya. Niiombe Wizara ikamilishe jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunayo kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya ukamilishaji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tunapoingia sasa hivi, tayari 98% limekamilika, nina shida moja ambayo mwaka jana nilisema na mwaka juzi pia nilisema. Hadi tunakamilisha kufikia asilimia hiyo, bado *CSR* ya Bwawa la Mwalimu Nyerere haijafika kwa walengwa wenyewe ambao ni Mkoa wa Morogoro, Pwani na Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani na Lindi tuna shida, jana ndugu yangu Kuchauka alikuwa amezungumza na akafika mahali hapa akasema anataka kukamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Kwangu mimi nasema sitokamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Waziri na msaidizi wake ni watu wema na wenye hofu ya Mungu. Tulipofikia hapa ni kwa sababu ya watangulizi wake kwenye *TANESCO* na watangulizi kwenye Wizara. Waliweka mbele maslahi binafsi na wakaamua kudhulumu haki ya Wanamorogoro na wananchi wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, ninachojua ni kwamba, Lindi wamepewa bilioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha TEHAMA. Nimwombe Ndugu yangu Mheshimiwa Kuchauka, Lindi imeguswa, amwachie shilingi yake ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ili akatekeleze majukumu. Pia imepelekwa shilingi bilioni 80 Kigoma, shilingi bilioni 40 Dodoma, shilingi bilioni 40 Tanga. Tunaomba shilingi bilioni 80 iende Morogoro ambayo ni ya Kigoma, shilingi bilioni 40 Dodoma na ile ya Tanga iende Pwani. Wananchi wa Morogoro na Pwani tuna haki hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafuriko ambayo yanatokea leo hii Mlimba, Malinyi, Ifakara, Rufiji na Morogoro ni kutokana na uhifadhi wa mazingira ambayo yanapeleka maji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, tuna haki ya msingi kupata hela hiyo. Kwa hiyo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ni mtu mwema na muungwana sana, kupitia timu yake ya *TANESCO* ambako

Mtendaji mpya amepatikana watupe haki yetu Wanamorogoro. CAG amekwishasema kwamba wakae, walishakaa zaidi ya mara mbili, Wizara na Mkandarasi, Mkandarasi anawakatalia kwa sababu miradi waliyoipeleka haihusiani na mkataba unavyosema.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba, sisi wananchi wa Morogoro na wananchi wa Pwani tuko tayari kukaa pamoja na Wizara watupatie haki yetu, naomba sana Ndugu yangu Mheshimiwa Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ni mtu makini na naamini kama nilivyosema ana hofu ya Mungu, sitaki kukamata shilingi yake, lakini naomba atusaidie Wana-Morogoro.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Francis Masanja na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magesa, ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kutoa mchango wangu. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, mdogo wangu Judith Kapinga, nimpongeze sana kwa kazi nzuri. Ameingia katika kipindi kigumu lakini ametumia kipindi hicho vizuri na ameonesha uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya. Wote tunaona ni namna gani ambavyo Mheshimiwa Rais amepambana katika kukamilisha miradi yote ya kimkakati ambayo iliachwa katika awamu iliyopita. Amejijengea historia kubwa na sisi kama Wabunge hatutoacha kulisema hilo na kuendelea kumshukuru.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuendelea kuzungumzia masuala mbalimbali hususani katika Mkoa wa Songwe. Sote tunafahamu matatizo makubwa ambayo tulikuwa nayo sisi kama nchi hususani suala la kukatikakatika sana kwa umeme katika Nchi ya Tanzania, vilevile katika Mkoa wetu wa Songwe. Hii inatokana na kwamba tumekuwa na vyanzo vichache, Tanzania kwa muda wa miaka mingi tulikuwa tunategemea vyanzo vichache kwa ajili ya kuzalisha umeme. Naomba nitumie nafasi hii kutoa ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ni wakati muafaka sasa Serikali iangalie ni namna gani ya kuweza kuongeza vyanzo vingine vya kuzalisha umeme hususan umeme ambao unatumia maji, huu ni miongoni mwa umeme ambao una gharama nafuu. Pia, tumeona namna ambavyo Mheshimiwa Rais amekamilisha Bwawa la Mwalimu Nyerere, kwa hiyo, niiombe sana Wizara ijikite kwenye mikakati madhubuti ya kuja na vyanzo vingine vya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, tunao Mradi mkubwa sana wa Ruhuji pamoja na Lumakali kule Njombe, mradi huu ulifanyiwa usanifu mwaka 1998, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu ameamua kuuhuisha mradi huu ambao ulisimama kwa muda mrefu na tayari amakwishatoa maagizo kwa Wizara ili kuhakikisha mradi huu unaanza kutekelezwa. Niiombe sasa Wizara iweze kusimamia ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati kwa sababu utasaidia sana kuongeza hali ya upatikanaji wa umeme katika nchi yetu. Vilevile, kama ambavyo Waziri Mkuu amesema juzi utasaidia sana kama nchi kuuza umeme katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba viko vyanzo vingi vya umeme. Pia, tunao umeme wa jotoardhi, Mkoa wetu wa Songwe tumebarikiwa. Katika Mkoa wa Songwe tunayo maeneo mengi sana ambayo tunaweza kuzalisha umeme wa jotoardhi. Kwa mfano, ukienda pale kwenye kile Kijiji cha Majimoto Wilayani Mbozi, tayari pale ipo kampuni tanzu ambayo imeanza kuufanyia kazi ule mradi. Naomba sana Wizara iweze kuongeza msukumo ili

mradi ule uweze kukamilika kwa wakati na Mkoa wa Songwe tuweze kuwa na vyanzo vya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa sababu tunayo maeneo mengi niiombe pia Wizara iweze kufanya utafiti kwenye maeneo mengine ndani ya Mkoa wa Songwe ambayo yanaweza kusaidia kuzalisha umeme wa jotoardhi.

Mheshimiwa Spika, pia tunao umeme wa jua. Tumeona Wizara ambavyo imekuja na mkakati na tayari wamekwishaanza kuzalisha umeme wa jua kwenye mikoa mingine kama vile Mkoa wa Singida na Mkoa wa Shinyanga. Naomba watanue wigo kwenye mikoa mingine, kwa mfano Mkoa wa Songwe na mikoa mingine ili tuweze kuzalisha umeme wa jua.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la usambazaji wa umeme, katika Mkoa wa Songwe kwa miaka mingi tulikuwa tuna changamoto ya kukatika kwa umeme. Mkoa wa Songwe ilikuwa ni kawaida umeme unakatika asubuhi, unakuja kuwaka saa nane halafu saa kumi na mbili umeshakatika, lakini ndani ya muda mfupi tumeona tayari umeme umeshatengemaa ndani ya Mkoa wa Songwe. Hizo ni jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya pamoja na viongozi wa Wizara, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ninalo ombi moja, kwa sababu tunayo ile gridi ya Taifa ya kutoa umeme kutoka Iringa kuja Mbeya mpaka Songwe pamoja na nchi nyingine za *SADC*, naomba sana Wizara iweze kukamilisha huo mradi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, pia tunayo ile *Station* ya umeme pale Nkangamo, tunaomba pia Wizara itusaidie kukamilisha ili sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe tuondokane na kutegemea *station* kutoka katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine ambalo nalo ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na umeme wa kuweza kujitegemea. Tunafahamu hali ya usambazaji wa umeme na niipongeze sana Serikali imefanya kazi nzuri sana,

sisi kwenye Mkoa wa Songwe tuna vijiji 470, katika vijiji hivyo 470, vyote vimeunganishwa kwenye umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali inapokwenda kwenye mkakati mwingine wa kuhakikisha kwamba wanakwenda kusambaza umeme kwenye vitongoji na sisi Mkoa wa Songwe tuna vitongoji 1,489. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ambaye amekuwa akija sana kwenye Mkoa wetu wa Songwe, watakapoanza kusambaza umeme kwenye hivi vitongoji 789 ambavyo vimebaki, ambavyo havijaunganishwa umeme katika Mkoa wa Songwe, niombe sana usambazaji huo uende kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kimekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi, utakuta kwamba nguzo zimewekwa lakini umeme hawauoni. Naomba wakandarasi wasimamiwe ili waweze kuwaunganishia umeme wananchi kwa wakati ili Mkoa wetu wa Songwe ambao umekaa kimkakati, uweze kuwa na umeme na kuwavutia wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalize kwa kumpongeza sana Meneja wetu wa *TANESCO,* Mkoa wa Songwe, anafanya kazi nzuri sana, sisi kama Wabunge tunapata ushirikiano wa kutosha, nampongeza sana pamoja na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Masanja, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ajiandae.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupatia afya njema na fursa ya kusimama katika Bunge lako Tukufu. Kabla ya kuanza kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo aliniamini na kunipa heshima kubwa ya kuhudumu katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Namshukuru sana kwa sababu imenipa upeo mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu mengine ambayo naendelea nayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, kwa usikivu wao na namna ambavyo wanajituma katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimepitia hotuba hii na nikaona Wizara ina vipaumbele kama tisa. Moja ya kipaumbele ni kuendelea kupeleka nishati vijijini ikiwemo kusambaza umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara. Nawapongeza sana kwa sababu malengo haya ni mazuri na ni makubwa kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mwanza, nasikitika kuona takribani vitongoji 2,476 bado havijafikiwa na huduma hii ya umeme, kikubwa zaidi Mkoa wa Mwanza umezungukwa na visiwa, takribani Majimbo matano yana visiwa. Moja ya Jimbo ambalo lina visiwa vingi zaidi ni hili Jimbo la Ukerewe ambako kuna visiwa takribani 38. Jimbo hili halina umeme wa uhakika. Mfano, katika Kisiwa cha Irugwa pamoja na Ukara ambapo kuna *population* kubwa ya wananchi, hawana umeme wa uhakika, umeme wanaoutumia ni umeme wa jua.

Mheshimiwa Spika, *unit* moja ya umeme huu inauzwa kwa takribani shilingi 1,500 mpaka shilingi 2,000, hii ni gharama kubwa na ukizingatia umeme huu hawautumii kwa masaa 24, ikifika saa nne usiku tu umeme huu unakatwa. Hivyo, tunaiomba Serikali iweze kuharakisha mradi uliopo pale Ukerewe upelekwe moja kwa moja katika visiwa hivi ili kupunguza changamoto iliyopo

katika visiwa hivi na kuharakisha uchumi katika maeneo haya ya visiwani.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Magu ambako kuna Kisiwa cha Ijinga napo kuna giza, tunaomba sana Serikali iweke jicho pale. Kuna Jimbo la Sengerema, kuna Visiwa vya Lyakanyasi, Bihila, Chitandele, Chikomelo, Jimbo la Buchosa pia kuna Soswa, Nyamg'honge, Itole, Ikuru, Yodzu, Kasalazi na Gembale, maeneo haya yapo gizani. Tunaomba sana Serikali kama imeamua kutupatia sasa umeme wa *solar* basi wananchi waweze kupata kwa bei iliyo nafuu ili uchumi wa wananchi hawa uweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu nishati safi ya kupikia. Niipongeze sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo imeweka mkazo katika matumizi safi ya nishati safi ya kupikia. Nina masikitiko makubwa sana katika eneo hili, takribani 90% ya nishati inayotumika ni ya mkaa na kuni, nishati ya gesi inayotumika mpaka sasa ni asilimia tano tu. Naiomba Serikali iweze kuhamasisha katika maeneo haya ili wananchi wabadilishe namna ya matumizi ya kutumia nishati safi ili kuokoa mazingira pia kuangalia namna ya kuepukana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa yakiikumba dunia mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, wananchi sasa hivi wamehamasika sana kutumia nishati safi ya gesi, lakini gesi hii ina gharama kubwa sana. Tunaiomba Serikali na kwa kupitia hotuba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, tumeona kuna punguzo la bajeti ambapo mwaka jana kwa bajeti hii inayoishia Juni walikuwa na trilioni 3.08 na sasa imepungua mpaka trilioni 1.88, tunaiomba Serikali kwa hili punguzo basi iweke ruzuku kwenye nishati safi ya kupikia ili akinamama ambao kwa 90% ndiyo wahanga wa eneo hili, waweze kunufaika na nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona tunawahamasisha wananchi wasikate miti hovyo, wasiharibu

mazingira lakini wanaporudi kwenye upande wa pili wanakutana na gharama kubwa za matumizi ya nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupitia hotuba ya Wizara niliona *TANESCO* ina deni ambalo wanazidai taasisi takribani bilioni 86, deni hili linaonesha kwamba limesababishwa na baadhi ya taasisi hazijaunganishwa katika umeme wa LUKU. Wananchi wanapokuwa na changamoto ya umeme mara nyingi madeni yao wanahakikisha wamekamilisha na ndipo LUKU ianze kuendelea kutumika, hivyo naziomba hizi taasisi kupitia Wizara wawaingize kwenye LUKU ili madeni yao wawe wanakatwa taratibu wakati huo huo wanalipa deni la *TANESCO* ili kuiwezesha *TANESCO* kujiendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya kuongea tena Bungeni kwenye Wizara hii ya Nishati. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi, uwezo na uhai aliotupatia ili kuweza kuifikia siku ya leo na kuweza kupata nafasi ya kuongelea nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa utashi na kukubali kuendelea kutoa fedha nyingi kwenye Wizara hii ya Nishati na tukaona mambo mengi yanayotekelezwa sasa kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati akiwemo Naibu wake mdogo wangu Mheshimiwa Judith Kapinga kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwenye Wizara hii. Ni ukweli usiopingika kwamba tunakumbuka tulikuwa na changamoto kubwa sana ya umeme na sasa tuna mazungumzo kwamba kuna

ziada kidogo kwenye umeme, maana yake kuna kazi kubwa sana imefanyika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza sana wataalamu wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu yangu Mramba. Vilevile nawapongeza viongozi na wataalamu mbalimbali katika Taasisi za Wizara hii ya Nishati ikiwemo *TANESCO, TPDC, REA, EWURA* na *PURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipita kwenye Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa nane kifungu cha 11 utaona utekelezaji mkubwa uliofanyika mwaka jana pia ulifanyika kwa mwaka huu wa fedha ambao unamalizika kwa sababu tulipewa shilingi trilioni tatu. Kwa hiyo yako mambo mengi sana yamefanyika. Ukiangalia fedha ya maendeleo takribani shilingi trilioni 2.6 mpaka Machi imekwishatolewa shilingi trilioni 1.7, maana yake pesa nyingi imetolewa kwa ajili ya utekelezaji huu. Kwa hiyo nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu iko pesa nyingi imeingia kwenye maeneo haya na wanamalizia mwaka huu kwa kuendelea kufanya hizi kazi ambazo zimeandikwa hapo chini kwenye utekelezaji. Wamepeleka umeme kwanza kwenye uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na umeme kote nchini.

Mheshimiwa Spika, pia, tumeuona umeme vijijini, vitongojini, mahali fulani kwenye visiwa, kwenye vituo vya afya na maeneo mengine mengi. Labda tu niseme hapa kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa sababu mimi nilikuwa na vijiji 58 vilivyokuwa havina umeme, hivi ninavyozungumza leo Jimboni Busanda vijiji vyote vina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja tu ninayobaki nayo ambayo naendelea kuiomba Serikali ni vitongoji. Nilivyoiona bajeti imepungua kutoka shilingi trilioni 3.0 kwenda trilioni 1.8 nikawa na mashaka. Nilitegemea hiyo bajeti iwe *maintained* yaani isipungue kwa sababu bado tuna vitongoji vingi.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu wa *REA* wanashindwa kusema tu, lakini ukweli ni kwamba wanahitaji fedha nyingi kwa

sababu zaidi ya 40% ya vitongoji ndani ya nchi hii havijapata umeme. Kwa hiyo niombe sana Serikali pamoja na kazi nzuri iliyofanyika, ndugu zangu wa Wizara ya Fedha waone namna gani wanavyoweza kushughulika na hii *REA*. Itakuwa ni kitu cha ajabu kama kitongoji kimoja kina umeme kingine hakina na watu wanaishi ndani ya kata moja au ndani ya kijiji kimoja. Tutaanza kutengeneza mambo ambayo yanaonekana kama kuna kupishana na matabaka yatatokea. Kwa hiyo ni ombi langu kwamba tungeshughulikia vitongoji vyote vikaisha, *REA* wawezeshwe vitongoji vyote viweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vizuri uzalishaji wetu *(installed capacity)* ndani ya nchi hii inaonekana kuna umeme wa maji unaotokana na maji, gesi asilia, mafuta na tungamotaka. Vyote hivi kwa pamoja ukiviangalia vimetuletea *megawatt* 2,138. Ukiangalia kiuhalisia tunaweza leo tukaridhika kwamba *installed capacity* ile inaweza kuwa inatupeleka kwenye hiyo *megawatt* 1,756 ambayo ndiyo tunaipata, lakini kiuhalisia ni kwamba tukiruhusu watu wote watumie umeme tunaweza kuona kama umeme tulionao huu ni kidogo sana. Hii ni kwa sababu tunakutana na *power ratio* ya mahali fulani, umeme unagawanywa ndiyo sababu tunaona kama mahali fulani tunaenda vizuri. Kuna watu ambao sasa wanatumia mitambo yao kuzalisha umeme ili kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, wote wakianza kutumia mashine ya kutumia umeme wa *TANESCO,* tutafika mahali tutagundua hiki tunachokipata sasa hivi ni kidogo. Kwa hiyo ni ombi langu tu kwamba tuendelee kuzalisha na kuanza kubuni vyanzo vingine vingi. Nimeona mahali fulani kwamba sasa tunakwenda kwenye dunia ya *renewable energy,* tunakwenda kwenye habari ya jua. Shinyanga pale tunaanza na *megawatt* 150, bado ni kidogo. Kuna mahali tunakwenda kuanza *hydro-powers* bado ni kidogo kwa sababu naona kabisa kwamba ndani ya miaka miwili baada ya watu kuufahamu huu umeme tunaweza kwenda kwenye *megawatt* 7,000 ambazo tutakuwa hatuna, tutarudi kwenye shida hii ambayo tulikuwa nayo hivi karibuni. Kwa hiyo nawapongeza kwamba chanzo kimoja cha Julius Nyerere chenye *megawatt*

2,115 kwa mashine moja tu au mbili, kimetupunguzia tatizo hili lakini tujiandae kuhakikisha kwamba tunapata uzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, nilikuwa napitia hali ya usafirishaji ikaonekana Mwaka wa Fedha 2022/2023, tulikuwa tumeshapita kwenye njia za usafirishaji takribani kilometa 6,363, lakini mpaka leo tunavyozungumza tumekwenda 7,745, maana yake tumeongeza njia za usafirishaji. Ukiangalia hali ya usambazaji tulikuwa na kilomita 168,548 na sasa tumeshakwenda kwenye 176,000, maana yake kuna mahali fulani tunakwenda. Kwa hiyo nimpongeze Mheshimiwa Waziri amekuwa mwepesi wa kufanya hizi kazi.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kabisa kazi za kiuhandisi hizi zingekuwa changamoto lakini, sasa anaonekana anajifunza haraka. Sasa ameshajua *penstock, spillways* utafikiri naye ni Mhandisi, lakini ni uwezo wake mkubwa wa kufanya haya mambo na dada yangu Mheshimiwa Judith naye ameingia hukohuko naye kama Mhandisi kumbe ni Mwanasheria. Kwa hiyo niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambayo imefanyika. Nigusie kidogo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana hasa inavyogusa maisha ya Watanzania wengi kwa ujumla. Niungane pia na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote waliopo ndani ya Wizara hii. Kwa

kweli wanafanya kazi kubwa na sisi kama Watanzania tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipitia kipindi kigumu hapa katikati cha changamoto kubwa sana ya umeme, lakini tumeona kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa nao na kazi kubwa ambayo wameifanya, leo hii changamoto ya umeme imekwisha. Lazima tuwapongeze sana kwa hili kwa kweli mpewe maua yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba uzalishaji umekuwa mkubwa bado sasa hivi nguvu kubwa sasa tuielekeze kwenye usambazaji pamoja na usafirishaji kwa sababu wananchi sasa hivi wao wanataka kuona umeme unapatikana. Leo tunawaambia kwamba uzalishaji kule upo wa kutosha mpaka kuna ziada, lakini wanapoona baadhi ya maeneo umeme unakatika wanakuwa hawaelewi kwa sababu tu aidha, changamoto ipo kwenye usafirishaji hasa kwenye miundombinu au kwenye usambazaji. Kwa hiyo niombe sana tutenge fedha na bajeti ya kutosha kwenye usafirishaji na kwenye usambazaji ili wananchi wetu waweze kunufaika sana na umeme huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye upande wa *REA*. *REA* wanafanya kazi kubwa, sisi sote tumekuwa mashahidi tunawapongeza wao na *DG* wao kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. Tunaomba aongeze nguvu hasa yale maeneo ya vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme na nguvu kubwa iende kwenye vitongoji ili wananchi wetu waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Wilayani kwangu Chunya bado nina changamoto, baadhi ya vijiji bado havijafikiwa na umeme na hapa tunapozungumza sasa hivi takribani kata tatu bado hazijapata umeme; Kata ya Lualaje ambayo ina vijiji viwili: Kijiji cha Lualaje na Kijiji cha Mwiji. Tayari miundombinu imeshafika pale na *transformer* imeshafungwa, lakini umeme bado haujawashwa. Wananchi wanauliza ni lini sasa umeme utawashwa ili waweze kunufaika na umeme huo kwa sababu wameusubiri kwa muda mrefu sana?

Mheshimiwa Spika, wakati mradi huu unapelekwa kwenye Kata hii ya Lualaje mwanzoni kwenye mipango hakukuwa na shule ya sekondari, lakini hapa katikati tumepata shule ya sekondari ambayo haikuwepo kwenye mpango wa kupeleka umeme wa *REA*. Niiombe sana Wizara na watu wa *REA* tuifikishie umeme Sekondari ya Lualaje ili na wenyewe waweze kunufaika. Tufanye wakati huu ambao mkandarasi bado yuko *site* ili na wananchi hawa waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kata nyingine ni Kata ya Mafyeko pamoja na Kata ya Kambikatoto. Hizi kata zote mbili bado na zenyewe hazijaweza kufikiwa na umeme kwa sababu mkandarasi aliyekuwepo mwanzoni alipata changamoto na mkataba wake ukawa umesitishwa na taarifa nilizokuwa nazo ni amepatikana mkandarasi mwingine. Naiomba sana Serikali impe nguvu mkandarasi huyu hapa, tumsukume kwa nguvu kubwa aweze kukamilisha mradi huu kwa wakati kwa sababu wananchi wa Kata hizi za Mafyeko pamoja na Kambikatoto wana uhitaji na wanausubiri umeme huu kwa nguvu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na umeme huu kwenda kwenye vijiji hivi, sisi pia kule Wilaya ya Chunya ni wachimbaji. Tuna mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya wachimbaji hasa wachimbaji wadogo. Mradi unakwenda lakini *speed* yake mpaka sasa hivi toka mradi umeanza takribani uko kwenye 28% mpaka 30%. Naiomba sana Serikali tuweze kupeleka fedha za kutosha ili tuweze kuwafikia hawa wachimbaji wengi zaidi ili umeme huu uweze kufika katika maeneo yao na wao waweze kunufaika na uzalishaji hasa wa madini ya dhahabu na uweze kufanyika vizuri zaidi ili tuongeze pato la Taifa kwa upande wa uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Chunya tunapata umeme, lakini umeme tunaoupata ni mdogo kwa sababu kwenye chanzo cha umeme cha Mwakibete *(Substation Mwakibete)* mpaka Chunya Mjini ni umbali takribani kilomita 150. Kutoka Chunya Mjini mpaka mwisho wa wilaya yetu Kambikatoto takribani kilomita 300 zinafika. Kwa hiyo tunaiomba Serikali ilikuwa ina mpango wa kupeleka *substation* maeneo ya Makongolosi

pale, tunaomba ipate fedha ipeleke *substation* pale ili wananchi hawa waweze kupata umeme mkubwa na wa uhakika na uzalishaji uweze kuendelea vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze suala la Gesi la *CNG*. Sisi kama Kamati tulitembelea maeneo kadhaa Dar es Salaam ambako kuna vituo kadhaa vya kujaza hii gesi kwenye magari. Mwitikio wa wananchi sasa hivi umekuwa ni mkubwa sana, lakini changamoto kubwa sana ambazo tumeziona ni mbili. Jambo la kwanza, gharama kubwa sana ya kubadilisha mfumo huu kuweka mfumo wa gesi kwenye magari. Tunaiomba Serikali ione namna ambavyo inaweza ikapunguza kodi kwenye vifaa hivi vya gesi ya kwenye magari ili wananchi waweze kupata au kufunga mifumo hii kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuhakikisha kwamba vituo hivi vya kujaza gesi vinaongezeka. Tumesikia kwenye hotuba mpango wa Serikali ni kuongeza vituo, lakini tunaomba sana Serikali ifanye jambo hili kwa nguvu kubwa na kwa uharaka kwa sababu uhitaji wa wananchi ni mkubwa. Tulikaa pale tukaona watu wanakaa saa mbili mpaka tatu kwenye foleni ya kujaza gesi. Kwa kweli kwenye uchumi wa nchi, mtu kukaa saa mbili kusubiri kujaza gesi, hili jambo halikubaliki. Tunaomba tuone namna ambavyo Serikali italichukua jambo hili kwa udharura wake. Tuongeze vituo hivi ili wananchi hawa wasikae muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa sasa tunaenda kutumia gesi kwenye magari tuanze na sisi, kwenye magari ya Serikali. Serikali kila siku imekuwa ikituambia, lakini utekelezaji wake unaenda kwa kusuasua. Serikali inapoagiza magari yake sasa hivi yaje kwenye mfumo wa gesi moja kwa moja ili wao ndiyo wawe wa kwanza kutumia hii gesi. Wakitumia wao hii gesi itawezesha sasa hata hawa wawekezaji binafsi ambao wanaenda kufungua hivi vituo watakuwa na uhakika wa magari kuwa mengi hasa magari ya Serikali ambayo yatajaza kwenye vituo vyao.

Mheshimiwa Spika, pia pamoja na kwamba sasa hivi tumeanza hasa pale kwa Dar es Salaam, sasa twende kwenye

miji mikubwa ikiwemo Dodoma, Arusha, Mwanza na Mbeya ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na huo mfumo wa gesi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ili nitoe machache kwenye hii Wizara ambayo kimsingi ndio *catalyst* ya uchumi (ndio inachochea ukuaji wa uchumi), ni kwamba bila umeme uchumi hauwezi kukua. Tunaweza tukaona mfano mdogo tu wa nchi ambazo tulikuwa tunadhani zimeenda mbele, lakini leo zina-*suffer* sana kwa sababu ya umeme. Mfano kama South Africa, leo tunavyoongea South Africa ina mgao wa umeme mpaka masaa nane. Kwa hiyo sasa unaweza uka-*imagine* kama nchi ina mgao wa umeme kwa masaa nane; je, uzalishaji wake ukoje? Kama unatumia *generator* ni gharama kiasi gani inatumika kuzalisha umeme?

Mheshimiwa Spika, niongelee tu kitu kidogo sana, mfano kama wafanyabiashara wa Kariakoo, niongee kwa niaba yao. Kumekuwa na *tendency* ya kukatika kwa umeme tukijua *nature* na mazingira ya Soko la Kariakoo kweli biashara zina-*suffer* sana. Unakuta wamefungua *generators,* ni makelele lakini pia wanatumia gharama kubwa sana na hiyo gharama si kwamba wanaibeba wao, *at the end of the day* gharama hiyo inaenda kwa yule anayeenda kununua biashara zao, kwa hiyo tuliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa ku-*scrutinize budget* kwa sababu mwisho wa yote yaliyofanyika katika Wizara husika yanapimwa kwa fedha kiasi gani imeenda kule chini. Utekelezaji wa bajeti ya hii Wizara bado ni mdogo kwa maana fedha iliyoenda mpaka mwezi Februari ni 52.27% *roughly,* ukiona mfano mishahara ni 69%, *OC* ni 17%, fedha ya maendeleo kutoka

kwenye fungu la ndani ni 50% kutoka nje 69% ambayo *bottom line* inaleta 52.27%.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bajeti kwa kutotimia walau hata ingefika 70% au 80% tungejua kwamba miradi mingi tuliyokaa kuijadili Bungeni imetekelezwa, lakini kwa bajeti kuwa 52% ni lazima miradi mingi haijatekelezwa na imeelezwa kwenye Taarifa ya Kamati. Nisisitize kwamba *at least* hii Sekta ya Umeme tukijua umuhimu na ukubwa wake katika uchumi, bajeti yake basi iende hata kwa 100%. Ndiyo namna pekee ya kuzuia kukatika kwa umeme, ndiyo namna pekee ya kuzuia kero za umeme ambazo tumekuwa tukizisikia hapa na hapa. Pia, itaondoa hata Mawaziri wenyewe, watu wanakuwa wanasema Waziri huyu ameshindwa hii wizara imeshindikana, ni kwa sababu ya fedha. Fedha isipoenda hata mshahara wa Waziri hautoshi kusema kwamba atachukua hela yake au maduhuli yaweze kusaidia upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, niende kuongelea changamoto ya umeme katika Wilaya ya Kyerwa. Kyerwa tuna vijiji 99, tunashukuru mpaka sasa naongea vijiji 92 vimewaka umeme bado vijiji saba. Naomba sana hivi vijiji viwashwe umeme. Vijiji hivyo nitavitaja; kuna Kijiji cha Rwamashaju, kinapatikana Kaisho, kuna Kijiji cha Kakerere. Hiki Kijiji cha Kakerere kinapatikana katika Kata ya Nkwenda ya Mjini kabisa. Sasa unajiuliza hii inakuwaje? Kijiji cha Ruhita, Kamuli; Kijiji cha Nsunga kiko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa yenyewe, Kijiji cha Kijumbula, Kijiji cha Kitega. Hii Kitega nimewahi kusema kwamba Kitega ipo mpakani mwa Rwanda, ilikuwa na changamoto ya mawasiliano na vitu kadha wa kadha. Kwa kipekee sana eneo la Kibare nilikuwa nikiongelea hapa Kijiji kinaitwa Kigorogoro kina changamoto ya maji na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba hivi vijiji vyetu saba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri vipelekewe umeme na vyenyewe vijione ni vijiji sawa na vijiji vingine. Ni kwa nini naombea umeme *specific* katika haya maeneo? Ni kwa sababu umeme ndio *catalyst,* umeme ndio tunauhitaji kwa ajili ya

kuendesha maisha na Uchumi, lakini wamewawekea nguzo, wamebaki kuziona zile nguzo kama mapambo, si sawa.

Mheshimiwa Spika, nikiongelea Jimbo la Karagwe ambalo ni jimbo jirani. Karagwe ina vijiji 77 na vijiji 76 vimewashwa umeme kuondoa Kijiji kimoja tu cha Nyabiyonza, si sawa. Nawaombea watu wa Nyabiyonza pia waunganishiwe umeme ili wawe pamoja na wenzao. Kwa hiyo katika masuala ya umeme naomba niishie hapo. Tumekuwa tukiongelea…

Mheshimiwa Spika, nina dakika 10, naona kama kengele imewahi, mimi sina dakika saba. Tumekuwa tukiongelea matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hakuna anayebisha kwamba matumizi ya kuni yanaharibu mazingira, hakuna anayebisha matumizi ya kuni ni ghali; hakuna anayebisha katika hilo, lakini nataka niulize ni kwa kiwango gani sasa tumeweza kusaidia upatikanaji wa miundombinu ya mabomba au ya kuwezesha kupatikana kwa nishati hiyo tunayoisema ni nishati safi ya kupikia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, Taarifa ya Kamati imeonesha ukitumia hiyo nishati mbadala ya kupikia utaweza ku-*save* kiasi gani. Hiyo gesi asilia imeonyesha unatumia shilingi 27,000, lakini kwa kitu kilekile utakachokipika kwenye mkaa utatumia shilingi 40,000 ambayo una-*save* 32%. Kitu kile kile ukitumia gesi ya mtungi ya *LPG* utatumia shilingi 76,000 ambayo ni sawa na 64%, lakini kitu hichohicho chenye *quantity* hiyo utakachokipikia kwa umeme utatumia shilingi 105,000 ambayo ni sawa na 74%.

Mheshimiwa Spika, leo tunavyoongea naishukuru Wizara, wametusaidia, tumepata mitungi ya gesi, lakini watu wakija kujaza gesi watahitaji gesi ya *LPG* ambayo *it is too expensive*. Kwa hiyo, namna pekee ya kuwezesha upatikanaji wa nishati ambayo ni nafuu ni kwa kutumia *LNG*. Sasa ni lazima mitambo iwekwe ili hii gesi iweze kuwafikia watumiaji.

Mheshimiwa Spika, kwa Dar es Salaam pekee, habari ya kusambaza gesi hiyo ili itumike viwandani na nyumbani imekuwa ni *story* ya muda mrefu, lakini kimekuwa ni kitu ambacho

hakitekelezeki. Kwa nini? Hiyo gesi inapatikana hapa nchini, kwa hiyo, itatumia gharama kidogo. Hizo tunazoita *LPG* zinatoka nje, na kwa hiyo, tunatumia dola kununua hizo *LPG* ambazo ni *expensive,* kumbe hiyo *LNG* tutapata hapa nchini na tutaokoa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine wengi sana wameongelea matumizi ya gesi kwenye gari, nasi tuseme basi na Dodoma hicho kituo kijengwe haraka sana ili kusaidia kupunguza matumizi ya *petrol* na *diesel. Diesel* na *petrol* zinaagizwa nje kwa dola ilhali gesi inapatikana hapa nchini. Hivyo, tungeweza kuokoa fedha ya kutosha na kwa sababu hiyo tungeweza kupunguza gharama kwenye uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, hii Wizara isipowekewa bajeti ya kutosha na isipoweza kukusanya fedha, haitaweza kutekeleza malengo yake. *TANESCO* unayoiona hapa imekuwa ikidai fedha nyingi sana. *TANESCO* inadai Wizara kadhaa ambazo hazilipi ankara lakini Wizara hizo hizo zimekuwa zikija hapa Bungeni, tunapitisha bajeti zao ikiwa ni pamoja na kununua umeme.

Mheshimiwa Spika, nataka nijue, ni kwa nini wanakuwa hawalipi ankara zao na hivyo kuifanya *TANESCO* ishindwe kujiendesha? Mwaka hadi mwaka unaambiwa *TANESCO* mizania yake iko chini, haijatengeneza faida, lakini Wizara hizo hizo zimekuja, tumezipitishia na zina hela ya kununua umeme, lakini hazilipii umeme.

Mheshimiwa Spika, hiyo hiyo *TANESCO* imekuwa ikidaiwa. Yaani ni mchezo wa kuku na yai. *TANESCO* inadaiwa. Mfano mdogo tu, *TPDC* inaidai *TANESCO* zaidi ya shilingi bilioni 720. Yaani ni wale wale watoto wa baba mmoja, kati ya kuku na yai ametangulia nani? Sasa hicho ni kitu gani? Ninadhani ifikie wakati hizi Wizara ziwe *harmonised.* Kama ni Wizara ya Maji ama Wizara nyingine zozote unazoweza kuzitaja, zinunue umeme kwa kulipa kwa kuwekewa mita. Kama ni *pre* au *post,* zilipe, lakini vilevile na *TANESCO* ilipe. Hiyo ndiyo namna pekee ambayo tunaweza kuondoa hiki tunachokiona.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nakushukuru, lakini nisisitize juu ya vijiji vyangu vya Kyerwa na hivyo vijiji ambavyo sasa vimewashwa umeme. Kule ni pakubwa, yaani unakuta kijiji kimoja, ndiyo zimewashwa sasa nyumba 20, lakini hicho kijiji ni kikubwa sana kiasi kwamba ukishaondoka, inakuwa kwamba wale wajiunganishie umeme kwa mfumo wa *TANESCO* ambao ni shilingi 300,000. Hii haitakaa iwezekane, hawataweza.

Mheshimiwa Spika, Kyerwa ni moja kati ya Wilaya ambazo zinatajwa kuwa maskini. Sasa maskini kama sisi tunawezaje kuunganisha umeme kwa shilingi 300,000? Kwa hiyo, narudia, nasimama pamoja na Wabunge wengine ambao wamesisitiza umuhimu wa shilingi 27,000 kuendelea kutumika. Hata kama hiyo *REA* ikiwa imekamilika, ikirudi kwenye *TANESCO,* basi baadhi ya maeneo yawe *considered* na hivyo wawafungie umeme kwa gharama hiyo. Nakushukuru sana kwa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ulivyodai dakika kumi, sikutaka kukukatisha. Kuna siku nyingine utachangia kama Wabunge wa CCM kwa muda wanaopewa na sababu ni moja tu. Kwa sababu ya uchache wenu, kuna wakati huwa mnapewa watu wengi kuliko idadi ya asilimia mliyonayo hapa ndani. Kwa hiyo, leo ni kwa sababu nilikuwa nimetoa hilo agizo.

Sasa anaweza akakaa Mwenyekiti hapa, halafu ikaonekana ninyi inabidi mpewe muda tofauti na Wabunge wengine. Nimeona hilo nilifafanue. Kwa hiyo, iko siku ambayo mtachangia sawa na Wabunge wa CCM kwa sababu ya muda tunaokuwa nao.

Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi uliyonipa ili nami niweze kuchangia hii hotuba muhimu ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kiujumla ambayo niliyoyaona, moja ni kwamba taarifa ya Waziri imeacha baadhi ya mambo muhimu sana ambayo Waheshimiwa Wabunge tulitaka tuyasikie, lakini taarifa ya Kamati ibara ya 2.4 na kielelelzo cha tatu imeripoti mkanganyiko wa takwimu. Kwa hiyo, ni vizuri na yenyewe hizo takwimu za mapokezi ya fedha zikafanyiwa marekebisho ili kuweka kumbukumbu sawa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *LNG* umetangazwa kwamba mkataba wake sasa rasimu yake ipo tayari. Sasa ni muhimu sana, kwa sababu tulishafanya makosa huko nyuma. Mradi mkubwa kama huu wa *LNG* tusifanye makosa tena. Kama rasimu ya mkataba imekamilika, tufuate *procedure* zilizowekwa, kwa maana ya kwamba mkataba huo kuletwa hapa Bungeni kwa mujibu wa Sheria ya *TEIT* pamoja na Sheria ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017* inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, pia nimeona utekelezaji wa mradi wa *ECOP*, ule mradi wa bomba, ambapo shilingi milioni 289.74 tayari Serikali imeshalipa kwenye mradi huo na tayari mradi huo umefikia 27.1%. Hiyo ni kazi nzuri ambayo Serikali inapaswa kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, nimeona pia kwenye eneo la Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao ni kama unaelekea mwisho sasa na malipo ni kama yameisha. Wenzangu wamesema hapa kwamba mpaka sasa hivi malipo ya *CSR* shilingi bilioni 270 hayajalipwa, na fedha kwa ucheleweshaji shilingi bilioni 822 haijalipwa.

Mheshimiwa Spika, iwe mchana iwe jioni hizi fedha za Watanzania lazima zilipwe. Hata kama kuna sarakasi kubwa kiasi gani, hizi fedha za Watanzania lazima zilipwe. Waziri leo atuambie hizi shilingi bilioni 270 za *CSR* na shilingi bilioni 822 za ucheweshaji wa miaka miwili na nusu uliofanywa na kampuni hiyo wahakikishe kwamba zimelipwa kwani fedha hizo ni za Watanzania, na hapo hatutakubali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa *REA*, vitongoji vyangu vingi (vitongoji 15) bado havijaanza; kule Mumunu, Dabwisha,

Machimu na Mwanani miradi hii bado haijaanza. Mheshimiwa Waziri tafadhali hii miradi sasa ianze ili wananchi katika vitongoji vyote kama tulivyonuia kama Serikali wapate.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia hali ya upatikanaji wa umeme na wamesema kuanzia Januari umeme umeanza kuimarika. Napongeza sana jitihada hizo, na hasa Mheshimiwa Waziri alipoingia tukaanza kuziona jitihada za makusudi. Kwanza, usimamizi makini wa kuhakikisha kwamba Bwawa la Mwalimu Nyerere linakamilika, na sote tumeshuhudia.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukaanza kumwona anaenda kwenye ziara moja kwa moja kwenye maeneo yote ya uzalishaji wa umeme. Tukaanza kuona jitihada hizo, akaanza kufuta mpaka likizo ya watumishi wake na yeye mwenyewe likizo za sikukuu ili kuhakikisha kwamba umeme unapatikana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na sarakasi nyingi sana pale *TANESCO*. Kwa mfano, waliajiriwa watumishi sita bila usaili wowote, bila ushindani na bila hata kutangazwa na hawajulikani hata waliletwa kutoka wapi na waliletwa kwa ajili ya nini kwenye shirika muhimu kama lile, na hasa hao ndio waliokuja kuanza katakata ya umeme ambayo ilikuwa inafanyika pale *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, pia hata *EWURA* yenyewe haikutekeleza majukumu yake sawasawa katika kuisimamia *TANESCO* katika kuhakikisha kwamba umeme unapatikana. Sasa hizo zote ni sarakasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumwondoa Waziri wa Nishati aliyekuwepo hapo, kumwondoa Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* na kuvunja Bodi ya *TANESCO* na kukuteua. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukuteua wewe Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko kuwa Waziri wa Nishati ambaye umeonesha uadilifu na unyeyekevu mkubwa sana kwa wananchi kwa kuwajibika kikamilifu. Tunataka Mawaziri wa aina yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka kazi moja tu, Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba sasa anashusha bei za umeme. Bwawa limekamilika, sasa tunataka bei ya umeme ishuke. Adhibiti hitilafu za umeme zinazotokea na wananchi walipwe fidia haraka hitilafu zikitokea, na pia sababu nyingine zilizokuwa zinasababisha katakata ya umeme ziweze kudhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *SONGAS* umefika mwisho. Miaka 20 imefika na hivyo mkataba huu umefika mwisho. Waziri hajatujulisha hatima ya mkataba huu ni nini? Hata hivyo, tunajua bei ya umeme ilikuwa kubwa sana. *SONGAS* ilikuwa inaiuzia *TANESCO* umeme kwa bei kubwa. Pia hawa watu walianza hata kutu-*charge*. Hata wakifanya ukarabati wa visima, wanatu-*charge*. Mpaka sasa hivi wanatudai shilingi bilioni 107 za kutu-*charge* kwa ajili ya matengezo, kazi ambayo haipo kwenye mkataba.

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka tuelezwe, huu mkataba kwa sababu umefika mwisho, maelezo ya utekelezaji wake yakoje? Tusije tukafika tukakuta mkataba tena umerejewa wakati ulikuwa na migogoro yote hii. Mkataba uletwe kwenye Kamati husika, uletwe hapa Bungeni ili tuone tathmini ya utekelezaji wake kabla ya maamuzi mengine yoyote yale ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu mkataba baina ya *TANESCO* na Kampuni ya Erolink. Hii Kampuni ya Erolink ndiyo ambayo imepewa jukumu kwamba wananchi wakitaka kupiga simu wapige kwao kwa ajili ya miito ya simu hasa simu hizi za dharura. Wananchi wetu wameonewa sana na huu mkataba wa *TANESCO* na Erolink. Kwanza haifahamiki huyo Erolink alitoka wapi, na maamuzi yakafanywa ya kuondoa vituo vya miito ya simu kwenye mikoa, yakawa *centralized* pale Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wananchi wanalazimika mpaka wapige simu Dar es Salaam halafu ndipo wapokelewe na ndipo waende kutatuliwa hitilafu zao za umeme. Watu wameunguza vifaa vyao, viwanda vimeungua, nyumba zimeungua, huduma mpaka upige simu Dar es Salaam; na uwezo

wa hiyo Erolink mpaka sasa hivi kupokea simu ni 30% tu. Maana yake ni kwamba 70% yote wananchi hawapati huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa siku wananchi wanapiga simu 70% hawapati huduma. Unategemea nini? Upige simu kiwanda kinaungua, nyumba inaungua! La pili kulazimika kulipa. Unalipia huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, hivi kwanza tuelezeni, hizi fedha anapewa nani? Ukipiga simu *Vodacom* au kampuni yoyote ile ya simu kwenye mambo ya dharura hakuna malipo, Polisi hakuna malipo; lakini leo wananchi wanalipia. Usiku wa manane nyumba inaungua, utapata wapi fedha kwenye simu? Haya yamewezekana na hiyo Kampuni ya Erolink hatujui nani kaileta na ni kwa sababu zipi?

Mheshimiwa Spika, lakini siri zinavuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja tu.

**SPIKA:** Sekunde thelathini.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba sana maamuzi kwanza huu mkataba wa Erolink uvunjwe haraka, na hivi vituo virejeshwe kwenye maeneo ya awali na vifanye kazi kama vilivyokuwa vinafanya zamani. Tuelezwe, leo tunaona....

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Ooh, ahsante.

**SPIKA:** Shukrani. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali na nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kufanya mabadiliko na kumweka Waziri mpya, Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. Tunakupongeza sana na kwa kweli umefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuwepo humu huu ni mwaka wa nane. Wizara hii ni moja ya Wizara ambayo leo humu tusingekuwa tunaongea, lakini tangu jana kwa kweli kila Mbunge ameona jitihada zako, hongera sana kwa unyenyekevu wako, pia hongera kwa timu yako.

Mheshimiwa Spika, nadhani na timu yako sasa umeipa nafasi ya kuwa na afya ya akili ya kufikiria vizuri jinsi gani tunaweza tukalipeleka shirika vizuri kuliko vitisho na mambo mengine yaliyotokea huko nyuma. Nakupongeza sana, na ninaamini mtaendelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* tunawafahamu vizuri, mmepata Mwenyekiti mzuri, Bwana Nyansaho amefanya vizuri sana kwenye benki, nami ni mkopaji kwake. Ulifanya vizuri benki, sasa ukija kutuzamisha huku, nadhani hatutaelewana. Ukifanya vibaya, Bunge lijalo tutakushughulikia vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mambo machache. Kwanza Mheshimiwa Waziri tunakupongeza kwa hali ya umeme na jinsi mlivyokuwa watulivu, hamko mitandaoni na hamko kwenye *TV* na watu wanaona jinsi mnavyofanya kazi. Hongereni sana. Umeme kwa sasa umeimarika ukilinganisha na hali ya nyuma pale ulivyokuwa unaingia, tulikuwa kwenye hali mbaya sana. Mungu awabariki sana, mwendelee kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, nina baadhi ya mambo nataka kushauri. Kuna baadhi ya sehemu humo *TANESCO* siyo nzuri. Mheshimiwa Dkt. Doto fanya *reshuffle,* na

ulishapewa hilo rungu na Mheshimiwa Rais. Tunaona kuna sehemu ambazo siyo nzuri, nami nitatoa mfano wa sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, nenda kaangalie mkataba wa uwekaji umeme wa Mji wa Serikali. Umeme wa chini ule kwa kizungu mnaita *underground,* au siyo, ule umeme kwenye mikataba ya kuomba kwenye *tender,* yaani mtu wa mwisho alikuwepo wa shilingi bilioni 37, shilingi bilioni 39 na shilingi 41, lakini kwenye kusaini mkataba umesainiwa kwa shilingi bilioni 55, yaani shilingi bilioni 14 zimeongezeka kutoka wanakojua wataalam.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninakushauri tu Mheshimiwa Waziri, mimi ni wa muda mrefu; naomba uende kwenye manunuzi, mle angalia kuna watu urekebishe ili pakae vizuri. *Model* nzuri anzia huo Mji wa Serikali kwenye umeme wa *underground,* utagundua kitu kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, sisi tunatoka vijijini, na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi humu wanatoka vijijini. Tulianzisha vituo vya kuwasaidia wananchi wetu kule vijijini, lakini ghafla vikafungwa, watu waanze kushughulika na simu aliyoisema Mheshimiwa Mpina. Natoa mfano, jana tu, sisi na Nyehunge tuko Jirani. Kumetokea *short* ya umeme, nyumba imekata umeme na kurudi zaidi ya mara kumi. Watu wanapiga simu Dar es Salaam, simu haishikwi, nyumba imeungua mpaka imeteketea.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Kituo cha Nzera ambacho kilikuwa kinaweza kufanya kila kitu, kimenyang'anywa mamlaka mpaka upige simu Dar es Salaam. Hii siyo sawa. Sisi tunakoishi, kwingine kuna umeme, lakini hakuna *network* ya simu. Sasa ni vizuri kwa sababu vituo hivi mmesambaza umeme vijijini kwa watu maskini, ni lazima kuwe na sehemu ambazo mtu anaweza akakimbia kwa miguu, siyo lazima apande gari.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu nataka kuchangia kuhusiana na suala la gesi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati, tumeenda India na Dar es Salaam tumeona. Wenzangu wamesema, ukitaka kuweka gesi leo kwenye vile vituo viwili vya Dar es Salaam unaenda saa tisa usiku. Tumefika pale saa tano, watu

wanaongea kutuelimisha, wale watu waliopanga foleni wanasema hivi, hawa ni Wabunge au ni akina nani? Wamekuja kufanya nini? Hatuna shida ya Wabunge, tunataka gesi. Kwa saa tisa mtu anakaa kwenye foleni kwenda kujaza gesi.

Mheshimiwa Spika, mimi ninashauri, kitu kizuri huwa kinaanzia kwenye Serikali na ukiangalia masharti, yaani wale wale wenye sheli ndiyo watengeneza mfumo. Hii mifumo inaweza kutengezwa na mtu yeyote kwa sababu hakuna kitu kigeni. Kwa mimi *genius* niliangalia mara moja tu, hata ukinipa gari lako leo nakuundia. Sasa masharti yamewekwa kwenye kituo, bei anapanga yeye na bei ya gesi yeye na kutengeneza mfumo yeye.

Mheshimiwa Spika, kitu kizuri ambacho nilijifunza, gari kama V8 kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma ukitumia mafuta utatumia kama shilingi 500,000 lakini ukitumia gesi, utatumia shilingi 94,000 kwenda na kurudi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu tunahangaika na *Mr. Kichere* sana kwenye matumizi mabovu ya Serikalini, ninashauri V8 zote za Mawaziri tuzifunge mfumo wa gesi. Kwa sababu kwanza sasa hivi muda mwingi na mko Dar es Salaam, mko Dodoma, sasa kwa kubana matumizi tukiwapiga ile mitungi kule nyuma msafiri hata kila wiki kwenda mara tatu Serikali itakuwa ime-*save* kutoka shilingi 480,000 mpaka shilingi 97,000 kwenda na kurudi.

Mheshimiwa Spika, nadhani na watu wengine tungeanzia hapo ili hata tukisema humu suala la kuongeza vituo vya gesi mtakuwa na uhitaji kwa sababu ya zile *routes* zenu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya pili!

**SPIKA:** Ya pili, ahsante sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami nampongeza sana Waziri kwa bajeti nzuri ambayo ametupatia na kwa utendaji mzuri kwa ujumla katika Wizara hii ya Nishati pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali, kwamba mpango wa *REA* kwa kweli umekuwa ni mkombozi kwa kiasi kikubwa ingawa ukienda kwenye vijiji na vitongoji bado ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa majimbo yale ambayo ni ya mjini; Halmashauri za Miji ambazo zina vijiji na miji, bado tuna tatizo kubwa sana maeneo ya miji; mitaa ina-*expand* kwa haraka sana kiasi kwamba hata ule umuhimu au ile *credit* ambayo tungeipata kwa kusambaza umeme vijijini kwa maeneo ya mijini, bado tuna tatizo kubwa, *especially* Njombe, tuna shida kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mitaa ya Mpumbwe na Ihanga, iko jirani kabisa na Makao Makuu lakini haina umeme. Ihanga, Igominyi kuna mtaa unaitwa Unguja na Pemba nikadhania pengine kwa sababu ya Muungano mngeweza mkaufikiria haraka haraka zaidi kuupa umeme kwa sababu hauna umeme na wananchi kwa kweli wanapata taabu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna maeneo ya uwekezaji. Njombe ni mji unaokua haraka kiuwekezaji, tunawaomba sana mtuangalie. Ndiyo maana kwenye swali la juzi niliuliza kuhusu *grid substation.* Tunahitaji kuwa na *grid substation* kwa haraka sana ili tuweze kuendana na kasi ya ukuaji wa mji.

Mheshimiwa Spika, kwenye hilo, napenda kusema namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, alitembelea njombe, na alikaa na wazalishaji wadogo wadogo wa umeme na aliwatia

moyo. Kulikuwa na wazalishaji wengi ambao ni wadogo wadogo. Njombe ni nchi iliyobarikiwa kwa maporomoko ya maji na inaweza ikatoa mchango mkubwa sana kwenye *grid* ya Taifa kwa kutoa umeme wa kutokana na maporomoko madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna *project* moja ya muda mrefu ambayo ni nzuri. Naomba ni-*declare interest* kwamba naimi ni mmoja wa wanahisa, inaitwa Mapembas, Mheshimiwa Waziri anaifahamu vizuri sana, *10 megawatts.* Hizi *megawatts* leo tungekuwa tunafanya maamuzi zingekuwa tayari zimekuwa *connected* kwenye gridi.

Mheshimiwa Spika, ni *10 megawatts* za Watanzania, maana yake tunaongelea ku-*empower* Watanzania ambao wamejikusanya wakaamua ku-*sacrifice pensions* zao kwa ajili ya kutengeneza *hydropower project*.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi fulani ungefikiria hawa wangesaidiwa. Sasa wanachokwama ni kitu kidogo sana kwenye *financing,* kwa sababu masharti ya *SPPA* bado yanataka ndani ya miezi 36 uwe umeanza ku-*deliver* umeme, inakuwa ni ngumu kwa sababu wanategemea fedha za benki, na benki zinataka uhakika kwamba, je, baada ya kusaini *SPPA* Serikali itakuwa tayari ku-*facilitate* ili *project* hii ijengwe?

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, *project* hii iangaliwe kwa macho ya ukaribu sana kwa sababu ni Watanzania, wengine ni wafanyakazi walio-*retire* katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, baada ya ile ziara tulikuuliza masuala ya nguzo za zege, Wananjombe, Wananyanda za Juu Kusini hatuna tatizo na maamuzi ya Serikali kwenda kwenye zege, lakini tunasema lifanyike kwa uangalifu.

Mheshimiwa Spika, nimesoma hapa na nimeona kwamba tunakwenda kujenga viwanda vingi vya nguzo za zege, nasi pia

tunaona umuhimu kwenye maeneo oevu, ni kweli lazima tuwe na hali kama hiyo, itatusaidia kupunguza matumizi ya fedha za Serikali. Hata hivyo, tukumbuke kuna mamilioni ya watu ambao maisha yao wameyaelekeza kwenye kuzalisha miti, miti ndiyo uchumi wao. Tuwaangalie hawa kwa sababu sera yetu na Sera ya Chama cha Mapinduzi ni kuwasaidia wananchi ili waweze kuwa na nguvu za kiuchumi na waweze kupunguza umaskini. Tunachosema, viwanda vinavyojengwa vya nguzo za zege visiongeze umaskini kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naongelea suala la *LNG*, muda hautoshi; tumeona hapa mradi huu wa kuchakata na kusindika gesi asilia ni mradi muhimu sana na utakuwa na *impact* kubwa sana kwenye uchumi wa nchi. Mimi niongee wazi kwamba tunatakiwa tuwe makini kama wengi walivyosema, tu-*balance* na *time*, tusije tukatafuta mkataba ambao ni *silver bullet*, haupo duniani.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kupata mkataba ambao ni *silver bullet* lakini tuweke *provision* zitakazotusaidia kuwa na *ability* ya kuweza kubadilisha mkataba huko mbele ya safari baada ya ku-*negotiate* vizuri kwa *level* tuliyofikia. Ninaloliona hapa, kuna ucheleweshaji unaoendelea, siyo kwa makusudi, nadhani ni kwa nia nzuri ya kutaka haya mambo yakamilike. Pia tukumbuke *we are a global village*. Wawekezaji tulionao wana miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tukumbuke kwamba tuki-*sign* hizi *host agreements* maana yake ni kwamba wanatakiwa wafanye *financial decision*, *investment decision* ndani ya miaka mitatu. Baada ya miaka mitatu ndiyo waanze *construction*. Sasa tatizo tulilonalo ni kwamba, sasa hivi *natural gas* imeshapata *competitor*. Tuna *hydrogen*, kampuni nyingi za kimataifa na kidunia kwenye *air transport*, *chemicals*, *steel* na *rail* yanaanza ku-*move away from natural gas* na yamepeana muda. Hii yote ni kwa sababu dunia inakwenda ku-*cut down emissions* na kampuni zimekuwa *tasked* ku-*make sure* zina-*cut down emissions*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaweza tukawa na gesi, tukatumia muda mrefu tukitafuta mkataba ambao ni *silver bullet* lakini mwisho wa siku tutakutana na soko ambalo limeshaharibika. Nitoe ushauri kwamba tutumie njia za kila aina tunazoweza. Tuna mshauri mwelekezi ambaye analipwa mabilioni ya shilingi, tumtumie vizuri, na kama hatufai, basi tumfukuze ili tujue kwamba hawezi kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwenye *LNG* tuongeze *speed* kidogo ili tuweze ku-*benefit* kwenye *upside*. La sivyo, hatuta-*benefit* na yale ambayo tungeyapata kwa kuendeleza mradi huu mkubwa wa *LNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naipongeza sana Serikali kwa kukamilisha Mradi wa *Mwalimu Nyerere Dam*. Mimi hapa nina *article* moja iliandikwa na gazeti la *The Economist*, gazeti linaloheshimika duniani. Wao walisema, katika Mbuga ya Selous kuna *elephant* na wakatoa picha ya *elephant*, wakasema kwamba sasa anakwenda kuongezeka *elephant* wa pili ambaye ataitwa *white elephant,* wakimaanisha hiyo itakuwa *Mwalimu Nyerere Dam*.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba Serikali ya Mama Dkt. Samia ikiongozwa na wewe Mheshimiwa Dkt. Doto imewa-*prove wrong* watu ambao waliamini kwamba sisi hatuwezi kujenga *dam*, waliamini hatuwezi kupata fedha, waliamini kwamba *dam* hii itajaa baada ya miaka saba, haiwezekani. *Dam* imejaa katika muda mfupi na tumeweza kupata umeme. Tunakushukuru sana na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niwe miongoni mwa wachangiaji kwa siku ya leo. Naomba kuanza kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya ili niweze kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anafanya kwa Taifa hili. Pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa na nzuri, na ametupa maneno ya kuiga kwamba Watanzania hawataki maneno, wanataka vitendo, wanataka umeme. Naomba nipongeze kwa moyo wa dhati. Nina uhakika hicho ambacho Watanzania wanakitarajia kimeanza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa katikati tumepitia katika wakati mgumu sana ambao umeme ulikuwa unakatikakatika, lakini leo hivi tunavyoongea hali ya umeme inazidi kuwa nzuri hasa baada ya hilo bwawa ambalo lingeweza kujaa baada ya miaka mitatu, lakini msimu mmoja tu wa mvua umetosha, huo ni ufundi wa Mwenyezi Mungu kwamba tunavyopanga sisi, yeye akitaka ya kwake yanakuwa kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanza kupatikana kwa umeme wa uhakika lazima kuende na mipango ambayo lazima tuharakishe na hususani ni mpango wa kuunganisha Mkoa wa Rukwa pamoja na Mkoa wa Katavi kwenye Gridi ya Taifa. Katika mpango uliokuwepo hapo awali, walikuwa wametarajia kwamba uunganishwaji wa mikoa hii kwenye Gridi ya Taifa ungefanyika baada ya kipindi cha miezi 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, kwa ajili ya upatikanaji wa umeme kwa wingi, huo mpango uliokuwa umewekwa kwamba tuunganishwe baada ya miezi 18, ni vizuri Serikali mpitie utaratibu huo, muuharakishe kwa sababu haileti tija pale ambapo tunaambiwa kwamba tunalazimika kuzima baadhi ya mitambo kwa sababu umeme ni *excess*, lakini kuna maeneo ambayo bado hatujajiunga kwenye Gridi ya Taifa na umeme unaendelea kukatika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni muda mrefu tumekuwa tukipata umeme kutoka kwa jirani zetu Zambia na kwa vile Mungu alivyokuwa fundi, wale waliokuwa wanatupatia umeme wa ziada, leo wao wana ukame mkubwa kiasi kwamba hakuna uhakika wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu kwamba *it is high time* ile mipango muipitie kwa upya ili tuunganishwe na gridi ya Taifa. Maana umeme ni maendeleo na kwa vyovyote vile, ili tuwe na uwekezaji wa kutosha, tuwe na viwanda vya kuchakata mazao, ni pale ambapo watu watakuwa na uhakika wa umeme kupatikana katika mikoa hiyo miwili ambayo nimeitaja na mikoa mingine yoyote ambayo haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia busara hiyo hiyo ambayo ilitumika wakati tukiwa na upungufu wa umeme, tukalazimika kupata umeme kutoka kwa nchi Jirani. Sasa katika mpango wa kuanza kuuza umeme, ili tupate dola, ni vizuri Serikali mkaanza kufikiria wale waliokuwa wanatuuzia sisi, tubadilishe tuwauzie kwa sababu tuna umeme wa ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo maeneo mawili, naomba niende upande wa *REA*. Katika mikoa ambayo kuna upelekaji wa umeme vijijini kwa maana ya *REA* kwa kusuasua ni pamoja na Mkoa wa Rukwa; na pia wamesema wenzangu waliotangulia kuhusu Katavi na hata Mkoa wa Kagera, na sababu ni moja tu. Ukitafuta kwa nini umeme vijijini katika maeneo hayo umepelekwa kwa kusuasua, katafute mkandarasi ni nani? Utakuta mkandarasi ambaye yuko Mkoa wa Rukwa, yuko Katavi huyo huyo, ndio unaenda kumpata kwenye Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utafiti ambao nimefanya, nini changamoto ambazo nimegundua? Mkandarasi huyo ameshindwa kufuata mpango kazi ambao walikuwa amekubaliana na mwajiri wake, lakini kama hiyo haitoshi, ana magenge machache sana ya wafanyakazi na hata wafanyakazi alioajiri, hawalipi mshahara kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, ana magari machache sana ambayo yanatumika katika kusambaza nguzo. Mkandarasi huyo hata akipelekewa taarifa na Mshauri Mwelekezi ha-*respond,* akitumiwa barua, hajibu na amekuwa akiongezewa muda kila wakati. Ifike mahali pale ambapo mkandarasi hatimizi wajibu wake kwa wakati, yale makubaliano ya kimkataba ikiwa ni pamoja na *performance bond,* itumike kukata ili iwe fundisho kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo vijiji ningependa Mheshimiwa Waziri uhakikishe kwamba umeme unaenda ni Kijiji cha Kapele, Kipwa, Tunyi, Kachele, Safu, Kifone, Ilango, Katapulo, Jengeni, Nondo na Mozi. Haipendezi pale ambapo wengine wanaongelea habari ya vitongoji kupelekewa umeme, sisi tunaongelea vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo Serikali yetu ilifanya vizuri katika *operation* vijiji ni Mkoa wa Rukwa. Ukienda vijiji vyetu *center* ni sawasawa na mijini. Kwa hiyo, tunaposema upelekwe umeme kwenye vijiji hivi, tunamaanisha uhitaji ni mkubwa sana. Ni vizuri Serikali ifike mahali ambapo baadhi ya wakandarasi mvunje nao mikataba, mtafute wakandarasi ambao watahakikisha kwamba umeme unafika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ni vizuri pia tuiombe Serikali, baada ya tamko la Makao Makuu kuwa Dodoma, nayo iangaliwe katika matumizi ya gesi kwenye magari. Nami naomba nisisitize kwamba iko haja ya kuhakikisha kwamba vituo kwa ajili ya ku-*convert* magari ambayo yanatumia *diesel* na *petrol* sasa yaanze kutumia gesi ambayo inatoka Tanzania. Hatuhitaji dola, tunahitaji shilingi ili tuweze kutumia gesi yetu na itasaidia katika kupunguza matumizi, na hasa Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Nishati. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutufikisha siku ya leo na nikapata muda wa kuchangia bajeti hii. Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi ambazo anaendelea kuzifanya katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Waziri wa Nishati, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri, Mheshimiwa Judith Kapinga, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuchangia kuhusu umeme vijijini *(REA)*, katika Mkoa wa Kilimanjaro. Katika miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia, tumepokea shilingi bilioni 79.683 ya kutekeleza miradi minne katika Mkoa wa Kilimanjaro. Mradi wa kwanza ni kusogeza miundombinu kwa wateja ambapo tumepokea shilingi bilioni 16.048. Mradi wa pili ni kuimarisha nguvu za umeme, shilingi bilioni 12.385. Mradi wa tatu ni matengenezo ya miundombinu, shilingi bilioni 16.538. Mradi wa nne ni kuunganisha umeme kwa wateja wapya, shilingi bilioni 25.379. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika miradi yote, mradi wa nne ambao ni mradi wa kuunganisha wateja wapya umechukua fedha nyingi sana, shilingi bilioni 25. Maana yake ni nini? Ina maana kwamba Watanzania wengi wanaoishi maeneo ya vijijini wamehamasika kupata umeme. Naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri na fedha nyingi ambazo tumezipata katika mkoa wetu wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, tunazo changamoto kidogo. Katika Mkoa wa Kilimanjaro tuna vijiji 519, vilivyopata umeme ni 506, vilivyobaki ambavyo mpaka leo havijapata umeme ni vijiji 13 na vijiji hivi 13 vinatoka katika wilaya mbili tu, Same pamoja na Mwanga. Same Mashariki ni vijiji vitano, nitavitaja: Kijiji cha Kirore, Kirongwe, Lugulu, Kanza na Makokane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Same Magharibi ni vijiji vitano pia; Kijiji cha Gavao Ngarito, Ruvu Mbuyuni, Chekereni, Gundesinde na Imugiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado vijiji vitatu vya Mwanga; Kijiji cha Mwanga Karamba, Mwai, na Pangoro. Inasikitisha sana. Inasikitisha kwa sababu wenzetu sasa hivi wanaongea habari ya vitongoji, lakini sisi vijiji 13 katika wilaya mbili havijapata umeme. Maana yake ni nini? Wananchi wanadhoofika, wanashindwa hata kufanya shughuli za kuongeza uchumi wao na kwa Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo sitaunga mkono hoja. Nataka Waziri akija atuambie tatizo liko wapi? Shida iko wapi? Ni ile milima ya upareni wanashindwa kupanda au ni nini? Sitaunga mkono hoja na nitashika shilingi ya Waziri kama hatanipa majibu ya kuridhisha. Wale wananchi wanataka kusikia kwa nini wao wanashindwa kufanya biashara? Kwa nini wao wanashindwa kujiendeleza kiuchumi? Leo nitashika shilingi ya Waziri kama sitapata majibu ya kuridhisha ni kwa nini vijiji 13 mpaka leo havijapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nitaongea kuhusu changamoto ya wakandarasi. Baadhi ya wenzangu wameongea, kuna wakandarasi wengine ambao wameshika kazi nyingi na unakuta kuna maeneo mengine sasa kutokana na wingi wa kazi, kazi nyingine zinazorota. Inaamanisha kwamba wananchi wanachelewa kupata umeme kwa muda.

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano katika vitongoji 24 vya Mwanga. Mkandarasi juzi amekaa na uongozi na akakiri kwamba amechelewesha kutekeleza mradi ule wa vitongoji 24 Mwanga kwa sababu alikuwa na kazi nyingine Tanga. Namwomba Waziri, wanapofanya mipango hiyo ya wakandarasi waangalie na mkandarasi. Kwanza nguvu ya mkandarasi na kazi alizonazo ili kugawa kazi ziweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya changamoto hiyo, nitaongelea kuhusu changamoto ya nguzo za zamani. Ni ukweli

tumepata mvua nyingi sana na maeneo mengi nguzo zetu za zamani zimechoka, maeneo ambayo yana mchwa mpaka zimepinda, ambayo ni hatari hata kwa wananchi. Naiomba Serikali ihimize kuhakikisha kwamba nguzo za zege za kisasa zinasambazwa katika maeneo mengi hasa maeneo ya vijijini na maeneo ambayo yana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo ipo ni kuhusu *transformer*. Mwanzo kabisa tulivyoanza zoezi la umeme vijijini nakumbuka Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli alikuwa anasema hapa hakuna Mtanzania ambaye atashindwa kufanya. Tulikuwa tunasema jogoo mmoja tu unaweka umeme ndani ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, wakati ule watu wengi walikuwa hawajajiunga, sasa hivi watu wengi wamejiunga na umeme, wamehamasika, wameona faida ya kuwa na umeme. Vijana wengi badala ya kukimbilia mijini, sasa hivi wako vijijini. Nitatoa mfano, mimi natoka katika Jimbo la Same Mashariki, katika Kijiji cha Gonja Maore, kuna *transformer* ambayo imezidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kipindi kama hiki tunavuna mpunga, vijana wengi wamenunua mashine zao za kisasa wanasaga mchele na kupeleka katika mikoa mbalimbali. Inasikitisha kwa sababu unakuta kutwa nzima mashine hazifanyi kazi kwa sababu umeme ni mdogo. Naiomba Serikali ijaribu kuangalia, kutokana na hali ambayo sasa hivi wananchi wengi wamejiunga, waongeze nguvu katika vituo vya kuongeza umeme. *(Makofi)*

*(Hapa kengele Ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** *Wooi!* Haya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim iddi, na Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuendelea kutupa afya na uzima, ili kuendelea kuwatumikia wananchi waliotuchagua. Tunajadili Bajeti ya Wizara ya Nishati kukiwa na utulivu mkubwa sana. Hii inatokana na sababu mbili; ya kwanza, ni hali ya umeme nchini ni nzuri sana na ya pili ni hali ya upatikanaji wa nishati ya mafuta kwenye vituo ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kabisa kumshukuru Kinara na Kiongozi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wetu, kwa kusimamia vizuri Serikali kiasi mbacho mambo haya yanakwenda vizuri kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ambaye pia ni Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara, Manaibu na watendaji wote wa taasisi za *TANESCO, REA, TPDC, PBPA, EWRUA, PURA* na *TGDC*. Hawa wote kwa sababu mimi niko kwenye Kamati hii, kwa kweli wanatoa ushirikiano mzuri sana kwa Kamati yetu kiasi ambacho na sisi tunaona kazi wanayoifanya ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa hali nzuri ya umeme nataka kutoa ushauri ufuatao; la kwanza ni *TANESCO* waendelee na kasi ya kuunganisha mikoa ambayo haiko kwenye Gridi ya Taifa, hasa inayotumia umeme wa mafuta, ili kuendelea kuwasaidia katika kupunguza gharama za uendeshaji na uzalishaji wa umeme. Mkoa kama Kigoma umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa katika wilaya tatu tu, waendelee kukamilisha kwa sababu, hizi wilaya zilizobaki ambazo zinatumia umeme wa mafuta, zinawalia gharama kubwa sana ya uzalishaji wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa sababu sasa wanakwenda kuzalisha umeme wa gharama nafuu, yaani wa maji, na kupunguza umeme wa gesi na mafuta, basi *TANESCO* nayo

ioneshe uungwana kwa kuwalipa *TPDC* deni lao awamu kwa awamu kuliko sasa hivi ambapo *TANESCO* inadaiwa shilingi bilioni 720 bila kutikisika kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tunaomba sana *TANESCO* wachukue hizo hatua mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *REA*, ndugu zangu kazi kubwa sana imefanyika. Ni basi tu, sisi wengine inawezekana hatupati nafasi ya kwenda kuona kwenye nchi za wenzetu, lakini zipo nchi za wenzetu tena jirani hapa, Makao Makuu ya Kata hakuna umeme, Makao Makuu ya Vijiji hakuna umeme, sisi sasa hivi tunazungumza habari ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. Napenda kuwapongeza sana *REA* pamoja na kwamba changamoto bado ipo, lakini kuwatia moyo ni kuwaongezea ari ya kuifanya kazi hii vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamezungumzia mafanikio tunayoyapata katika suala zima la kutumia *CNG,* yaani gesi kwa ajili ya uendeshaji wa magari. Kwa sababu ninahudumu kwenye Kamati hii nimepata nafasi ya kuona, lakini jambo ambalo nataka kuishauri Serikali ni kwamba, suala la kuweka vituo vya kujaza gesi kwenye magari, msihangaike nalo ninyi kama Serikali, itisheni sekta binafsi. Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe umeona, kituo kile cha *Taqwa* ni cha sekta binafsi, ukifika unaona kweli hiki ni kituo cha kuweka *CNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda katika kituo chetu kina *pump* mbili tu, hawa wana *pump* sita halafu zipo vizuri, wanahudumia watu 1,000 kwa siku. Sisi katika sera yetu, katika miaka ya 1990 tulibadili sera. Serikali haimiliki njia kuu za uchumi. Serikali sasa imebaki ni mhimili wa uchumi. Njia kuu za uchumi sasa zinasimamiwa na sekta binafsi. Kote ambako tumeshirikisha sekta binafsi, tumefanikiwa na hata pale tulipoingia ubia na sekta binafsi tumefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii unaangalia *TANOIL* inayosimamiwa na Serikali imeanza kufa, lakini kule kote ambako tumewekeza pesa za Serikali kwenye sekta binafsi kama vile *Puma Energy*, kwenye Benki za *CRDB*, *NMB, TBL, TCC, ALAF*, kote huko tunapata gawio na mashirika haya yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, msijibebeshe mzigo wa kuhangaika na vituo vya *CNG,* itisheni sekta binafsi wafanye hii kazi. Mheshimiwa Waziri kama unavyofahamu kuna maombi 11 ya kuweka vituo pale Dar es Salaam, harakisheni kuwapa vibali hawa waweke vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la aibu, tumewahamasisha watu kutoka magari 1,000 mwaka 2023 mpaka magari 3,000 mwaka huu, halafu watu wanapanga foleni masaa matano, sita, wanasubiri kujaza gesi. Waruhusuni hawa walioomba wapewe vibali waweke vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima la gesi kwa matumizi ya kupikia nyumbani. Kwa sasa tunatumia *natural gas* kwa sehemu ndogo sana ambayo imepelekewa hizi *pipe* kule Dar es Salaam. *Natural gas* ambayo inatumika Dar es Salaam, ambayo imeanza kuunganishwa katika taasisi, gharama yake ni nafuu sana. Kilo moja ni kama shilingi 1,000, lakini *LPG* hii ya mitungi ambayo tunasambazia watu, gharama yake kilo moja ni shilingi 4,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tufike mahali Serikali ije na mkakati. Serikali ilikuwa imeanza kufanya utafiti wa kuona namna ya kuweza kufika mahali kutumia *natural gas* iweze kuwa *LPG* ili kuweza kuisambaza kwa urahisi zaidi. Endeleeni na utafiti huo ili utafiti ukikamilika basi tuweze kuanzisha *plant* ya *LPG,* ili iweze kusaidia kusindika hiyo gesi na kuiweka kwenye matenki na kuipeleka maeneo mbalimbali kwa matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, jambo moja…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Ooh!

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema kwamba, kwa sababu hii *LPG* kwa sasa ina gharama kubwa na wananchi wetu wanavutiwa kuitumia, Serikali sasa iangalie uwezekano wa kufika mahali ianzishe utaratibu wa ununuzi wa pamoja wa gesi hii ya *LPG* kama ilivyofanya kwa mafuta, ili wananchi waweze kuipata kwa gharama nafuu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya leo. Pia, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya, bila kusahau kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wa Jimbo la Msalala, tuna imani kubwa sana na Waziri. Naendelea kumwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, apatapo wasaa, basi wananchi wa Jimbo la Msalala wanamwalika aweze kufika kuzungumza nao. Wanatamani sana waweze kusikia sauti yake. Karibu sana Jimbo la Msalala Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Nakiri kwamba Sekta hii ya Nishati ilifikia wakati watu wakatunga nyimbo mbalimbali, wakatunga misemo mbalimbali, kwa ajili ya kukosekana kwa umeme.

Mheshimiw aSpika, ilifikia kipindi *TANESCO* ikawa inatumika kwenye kibonzo kimoja nilikiangalia, mtu mmoja anamwambia

mpenzi wake kwamba, mimi siwezi kuwa kama *TANESCO* kwa hiyo, naomba uniamini. Maana yake *TANESCO* ilifikia hatua mpaka ikaonekana kwamba, hawana uaminifu na hawaaminiki katika nchi hii, lakini wewe Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko umeweza kurudisha hali na ikawa sawa na sasa watasema kauli zilizonyooka kama *TANESCO,* kwa sababu *TANESCO* kwa sasa imetulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naanza kwa kuipongeza Taasisi ya *TANESCO,* pia nawapongeza sana watu wa *REA*. Katika Jimbo la Msalala, vijiji takribani 64 vilikuwa havina umeme, lakini tunavyozungumza hivi, tayari jitihada zinaendelea kuhakikisha ya kwamba vyote 64 wanapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuleta ombi langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwamba, katika Wilaya ya Kahama kuna halmashauri tatu na halmashauri zote hizi tatu tuna kata zaidi ya 58 ambazo tayari zote tunaenda kupatiwa umeme vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana, kwa ukubwa wa Wilaya ya Kahama, utenge fedha katika bajeti hii, Mheshimiwa Waziri, twende pale tukaanzishe Wilaya ya ki-*TANESCO* kwenye Wilaya ya Kahama, kwa sababu vijiji vyote ukiangalia, kwa mfano kama mimi nina vijiji 92, na vijiji vyote hivi viko mbalimbali. Kwa hiyo, tunapata taabu sana pale tatizo la umeme linapotokea, ukizingatia tuna uhaba wa magari kwenye eneo lile, basi inatusababishia ugumu sana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kingine ninachoomba ni Wizara iweze kuwatengea watu wa *TANESCO* fedha za kutosha. Tunatumia fedha nyingi kupeleka umeme vijijini, lakini umeme hausambai, matokeo yake sasa tunajikuta tunatumia gharama kubwa kupeleka umeme na umeme hausambai kwa sababu, wananchi hawapati huduma ya kuvutiwa umeme. Hii ni kwa sababu ya bajeti ya kusambaza umeme. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye Kata ya Segese, miji mingi inakua sana kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kata ya Segese, Kata ya Bulyanhulu, Kata ya Isaka na kata nyingine wanahitaji huduma ya umeme, lakini bado bajeti ya usambazaji wa umeme kwenye maeneo hayo imekuwa ni ngumu sana. Kwa hiyo, naendelea kukuomba sana kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kusambaza umeme kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwenye suala zima la gesi. Ni kweli Wizara imefanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba inasambaza gesi za nyumbani. Nakushukuru sana kwa kutupatia kibali kwenda kufanya ziara nchini India, tumeenda pale tumejifunza. Nami nataka kuiomba Wizara, kupitia yale ambayo tumejifunza na ushauri wetu, ni wakati sasa umefika wa kuanza kubuni njia mbadala za kwenda kuzalisha gesi ambayo itasaidia kupunguza gharama kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukiangalia kwa mfano Wilaya ya Kahama, pale tunalo dampo la uchafu wa taka ngumu na taka za vyakula ambazo tulipoenda India kujifunza, tumeona ni namna gani wenzetu wanatumia taka za chakula na takataka nyingine kutengeneza gesi. Hiyo inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu tutengeneze mfano kwenye Wilaya na Halmashauri ya Msalala. Dampo tunalo, tupeni fedha sasa tuweze kujenga kiwanda kile ambacho hakina gharama yoyote. Inaweza ikawa ni dola 100,000 au 200,000 kujenga kiwanda kile cha kutengeneza gesi asilia na wananchi wetu wakapata gesi ambayo kimsingi ina gharama nafuu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kuzungumza kwenye suala zima la wakandarasi na uzambazaji wa umeme. Nataka kushauri kwenye suala hili, tunapoenda kuwapatia wakandarasi kazi za kufanya, utaona wakandarasi wageni wanakuja na kuchukua zile kazi, lakini nani anafanya kazi zile za kusambaza umeme kwenye maeneo hayo? Kwa sehemu kubwa bado unakuta ni Watanzania ndio ambao wanafanya kazi hizo za kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba watu wa *TANESCO*, watu wa *REA*, Mheshimiwa Waziri, nenda kaliangalie hili. Punguzeni masharti ili kuwawezesha wakandarasi wa ndani kuweza kufanya shughuli hizi kwa sababu, hata kama mtawapa wakandarasi hawa wakubwa, hawafanyi kazi hizo, wanaofanya ni wananchi wa Tanzania na uwezo huo wanao. Kwa hiyo, naomba sana *TANESCO* nendeni mkaone namna ya kuanza kuwakuza wawekezaji na wakandarasi wa humu ndani waweze kufanya shughuli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapata changamoto nyingi sana, watu wetu wanateseka kule, lakini mkiweza kuwawezesha hawa wakandarasi maana yake ni nini? Fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya miradi hii itabaki hapa hapa ndani na pia, mtasaidia zaidi kutengeneza ajira kwa vijana wetu kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, naomba sana suala hili, Wizara na Mheshimiwa Waziri mwende kulifanyia kazi ili wakandarasi wetu hawa waweze kupunguziwa masharti na waweze kutumia fursa hii kwenda kupata ajira na kazi hizi za umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, lakini naomba uzingatie hili kwamba, tunahitaji Wilaya ya ki-*TANESCO* katika Wilaya ya Kahama ili kuweza kufanya *facilitation* katika maeneo yetu ya vijijini na wananchi wa vijijini waweze kupata haki ya kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nakupongeza sana kuhakikisha kwamba umepeleka umeme kwenye maeneo ya wachimbaji. Wachimbaji wanahitaji nishati hii ya umeme. Naendelea kuomba mwendelee kuongeza kasi kubwa ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kupunguza gharama za kufanya shughuli kule kwenye maeneo yao na kuweza kujitengenezea uchumi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, nashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami leo niweze kuchangia kwenye hii Wizara ya Nishati. Kwanza, kwa sababu muda siyo rafiki, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa alizozifanya hasa katika ukamilishaji wa Bwawa hili la Mwalimu Nyerere ambalo limegharimu jumla ya shilingi trilioni 6,500 ambazo zimekaribia kulipwa zote na bwawa limeanza kuzalisha. Tumeanza kupata *Megawatts* 235 ambazo zinaingia kwenye gridi ya Taifa. Hongera sana Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii ilikuwa imeachwa kwa 37% na sasa umeikamilisha kwa karibu 95%. Kwa hiyo, tunakupongeza. Umeongeza umeme katika gridi ya Taifa kutoka *megawatts* 1,872 mpaka *megawatts* 2,138 sawa na ongezeko la 14%. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Wizara kwa kusimamia vizuri mradi huu. Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko hatuna shida na wewe, unachapa kazi vizuri na tunakuamini kwamba, wewe ni mmoja wa Waheshimiwa Mawaziri wachapakazi na hodari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bwawa kukamilika, tunaamini pia, mmekamilisha njia ya kusafirishia umeme kutoka *Hydropower Mwalimu Nyerere* mpaka Chalinze, ni hatua kubwa sana, hongereni sana. Pia kukamilika kwa njia ya usafirishaji wa umeme kutoka Morogoro mpaka Dodoma kwa ajili ya treni ya umeme na yenyewe pia tunawapongeza. Naona kwenye kitabu chao wameweka bajeti ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme katika njia ya treni ya umeme ya *SGR* kutoka Dodoma mpaka Tabora. Nawapa pongezi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunaipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kukamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyote nchi nzima, hasa jimboni kwangu, hongereni sana. Jimbo zima la Manonga, vijiji vyote vimefikiwa na umeme na sasa kazi inaelekea kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Spika, tuna jumla ya vitongoji 31,000 Tanzania nzima ambavyo havina umeme. Hapa sasa namwaomba Waziri aweke uzito mkubwa kuhakikisha kwamba vijiji hivi 31,000 vilivyobaki nchini anavivalia njuga. Hapo awali bajeti ilikuwa ni karibu shilingi trilioni sita na yalikuwa ni matarajio. Kwa hiyo, naomba uangalie namna ya kuweza kuvikamilisha kwa wakati ili vitongoji vyote nchini viweze kunufaika na umeme.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mkurugenzi wa *REA* kwa kazi nzuri. *Eng.* Hassan nakupongeza sana kwa kusimamia vizuri miradi hii ya *REA* vijijini, endelea kuchapa kazi. Sisi Waheshimiwa Wabunge tunakuamini pamoja na Wizara yako tunaiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri Dkt. Doto Biteko, kwenye suala zima la *TPDC*. *TPDC* ni uchumi wa nchi. Naomba Mheshimiwa Waziri apate muda akatembee *Saudi Arabia*, akatembee *Oman*, akayaone mashirika makubwa ya petroli yanavyoleta uchumi wa nchi hizo za *Oman* pamoja na *Saudi Arabia*. *Oman* kuna *PDO* na *Saudi Arabia* kuna *RAMCO*, Tanzania tuna *TPDC*.

Mheshimiwa Spika, naomba hili Shirika la *TPDC* tulipe fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba, tunazalisha mafuta kwa sababu, tumeanza kuona dalili za kupata mafuta. Katika njia ile ya pale Wilayani kwetu Igunga, kwenye lile Bwawa la Mto Eyasi Wembele, tunazo taarifa za kupatikana kwa mafuta. Tumeona mmeanza kuchakata kwa kutumia *2D*. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri ongeza fedha twende kwenye *3D* tuweze kupata haya mafuta ili tuweze kuyatumia kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TPDC* inaidai *TANESCO* zaidi ya shilingi bilioni 700. Tunaomba *TANESCO* fedha hizo zirudishwe *TPDC* ili *TPDC* iweze kujisimamia na kuweza kufanya kazi nzuri. Pia napenda kukupongeza Mheshimiwa Waziri, bajeti yako mwaka huu unaoisha ilikuwa ni shilingi trilioni tatu, bajeti unayoiomba ni shilingi bilioni 1,800. Maana yake kuna punguzo la karibu shilingi bilioni 1,200. Hii inamaanisha nini?

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa ambayo mlikuwa mkiisimamia imepungua kwa maana sasa mnaenda kukamilisha, lakini fedha hizi Mheshimiwa Waziri mngezipeleka kwingine, mkazijaziliza kwenye umeme vijijini na vitongojini.

Mheshimiwa Spika, kingine, tunatambua mahitaji ya miundombinu, *TANESCO* Wilayani kwetu Igunga tuna uhaba wa magari. Mheshimiwa Waziri tunakuomba, Wilaya yetu ya Igunga ni kubwa sana, tunahitaji magari ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Igunga inahudumia majimbo mawili, lakini sisi kwetu Jimbo la Manonga pamoja na miundombinu, unatambua jiografia yetu. Umeme wa Igunga unatoka Wilaya ya Nzega, unatembea zaidi ya kilometa 150 kuja Igunga na wakati mwingine huku mwanzoni ambako ni Chomachankola, Ziba, Nkinga, umeme huu unasafirishwa kutoka Nzega unakuja Igunga, unapelekwa Wilaya ya Uyui kwa ndugu yangu huyu Mzee wa Igalula, Loya. Umeme ukikatika huko, Wilaya ya Igunga yote umeme unakatika na miundombinu ya magari hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atupatie gari, pale Wilaya ya Igunga aongeze gari lingine, hasa maeneo ya Choma au Ziba, kwa ajili ya kurahisisha *movement* zile za watu, wapo ambao wanaweza kutembea. Kwa ujumla, Mheshimiwa Waziri, ninawapongeza sana Wizara kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Yangu yalikuwa ni hayo na ninaiunga mkono Bajeti ya Wizara hii ya Nishati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kibali hiki cha pekee alichonipa kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, binafsi nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu Dkt. Doto Biteko na Naibu Waziri wako wa Nishati kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya kwa Watanzania. Kumbe inawezekana Tanzania bila kukatika umeme chini ya uongozi wako na chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kwa upande wa Jimbo la Ushetu, tuna vijiji 112 lakini vijiji 112 vilivyopata umeme mpaka sasa ni vijiji 86. Tuna upungufu wa vijiji vyetu 26 havijapata umeme. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, wananchi wa Ushetu wanahitaji umeme, wananchi wa Ushetu ni wakulima, kila wanapopata mazao yao wanahitaji waweze kufunga mashine. Sasa tunapokosa umeme kwenye vijiji 26, inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye vitongoji vyangu 554 tutapata umeme lini? Niendelee kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuna vijiji vyangu viwili vimesahaulika, havijaingizwa kabisa kwenye mpango. Kuna Kijiji cha Kalama ambacho kipo Kata ya Kinamapula, kuna Kijiji cha Bukale ambacho kipo Kata ya Bulungwa, vilisahaulika kwenye mradi, naomba vijiji hivi viweze kuingizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliahidiwa hapa wakati wa swali langu la msingi kwamba tutajengewa kituo cha kupoozea umeme katika Halmashauri ya Ushetu, ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu mwenyewe hapa kwamba kitajengwa katika Halmashauri ya Nyamilangano, katika Kijiji cha Nyamilangano lakini nimesoma bajeti nzima ya Wizara ya Nishati sijaona mpango huo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba ahadi yangu hii iweze kutekelezwa kwa sababu wakati najibiwa swali langu, wananchi wa Ushetu walikuwa wanafuatilia na kusikiliza. Naomba hili suala liingizwe kwenye bajeti ili anapokuja kuhitimisha Mheshimiwa Waziri naomba nisikie kituo changu cha kupoozea umeme katika

Halmashauri yangu ya Ushetu. La sivyo, nitaondoka na mshahara. Nikiondoka na mshahara ndugu yangu naenda kwenye tumbaku huko, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu huwezi kunipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisimama hapa kusema kwamba eneo la Kahama, Wilaya ya Kahama yote na majimbo yake matatu yanazungukwa na mbuga, sisi hatujawahi kupata hizi nguzo za zege na majaruba haya, hawa ndege weupe wakianguka tu kwenye nguzo, nguzo inadondoka. Wilaya ya Kahama inakosa umeme, halmashauri zake zote zinakosa umeme.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2023 nilisema hapa kwamba tunahitaji Mkoa wa Ki-*TANESCO* Kahama kwa sababu ya makusanyo, lakini pia na shughuli za kibiashara zinazofanyika katika Wilaya yetu ya Kahama. Wilaya ya Kahama ina majimbo matatu; Wilaya ya Kahama ina makusanyo makubwa sana kwa upande wa *TANESCO*. Ndiyo maana hata mwaka 2023 kwenye bajeti nilisema, mtakapotupa Mkoa wa Ki-*TANESCO* makusanyo kwenye Serikali yetu yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, leo tu pamoja na kwamba na umeme wa kuzimazima hivi, umeme unakatika, Kahama inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 5.6 kwa mwezi upande wa *TANESCO*. Sasa kwa miezi mitatu iliyopita wilaya tumekusanya zaidi ya shilingi bilioni 15,600. Sasa kwa nini tusipewe Mkoa wa Ki-*TANESCO* ili Halmashauri ya Msalala iweze kuwa Wilaya na pia Ushetu iweze kuwa Wilaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuomba, Wizara itakapokuja kuhitimisha, waje na majibu ya lini watatupa Mkoa wa Ki-*TANESCO* kwa upande wa Kahama? Tunaomba Mkoa kwa sababu, hata Manispaa ya Kahama tu makusanyo yake, ukiangalia hoteli kubwa zilizopo Kahama ni zaidi ya 11, nenda viwanda vidogo vidogo vilivyosajiliwa ni zaidi ya 491, nenda kwenye biashara Kahama zilizosajiliwa ni zaidi ya 7,680. Kwa hiyo, ni eneo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa macho kwa upande wa *TANESCO* ili kukatikakatika kwa umeme Kahama ikome kama maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine watu wameshasahau kukatikakatika kwa umeme. Mahali kwenye uchumi ambapo unajua kabisa kwamba nitaenda kukusanya mapato, kwa nini msielekeze nguvu? Kwani kutupa Mkoa pale wa ki-*TANESCO* ili maeneo haya yote ya viwanda; ukiangalia Msalala ina wachimbaji wazuri sana, vijana wanajiwekeza kwenye madini lakini umeme unakuwa wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukienda Ushetu tuna wakulima tunajenga viwanda vya kusindika tumbaku lakini umeme haupo. Tutengeeni mkoa Mheshimiwa Waziri ili tuweze kuzalisha na tuweze kuchangia mapato ya halmashauri yetu pamoja na nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni *transformer; transformer* za *REA* zinakuwa ndogo sana, dakika moja tu wananchi wanapofikiwa pale wanaweka mashine, *transformer* inakuwa inasumbua. Wananchi wangu wanalalamika sana kila eneo. Nenda Kata ya Ulowa wananchi wanalalamika, nenda Kata ya Bulungwa wananchi wanalalamika, nenda Kata ya Nyamilangano pale wananchi wanalalamika, kwa sababu ni maeneo ambayo wananchi wake wanawekeza sana kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa wanapopata tu umeme pale, wanajenga mashine, wanaweka mashine ya kukamua, ya kusindika mpunga, wanaleta mashine ya kusaga, mashine ya kukoboa mchele, sasa umeme unakuwa ni wakukatikakatika. Kazi wanayofanya na sisi ni kututukana na kutulaumu pamoja na umeme wa *REA,* lakini *transformer* zote zinakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuomba Wizara itusaidie sana kwenye maeneo ya *transformer*, ziwekwe *transformer* kubwa ambazo zinahimili hali ya uchumi wa wananchi wa sasa. Kwa sababu Serikali ya Mheshimiwa Rais imeweka mapato makubwa sana na fedha zinaongezeka kwenye upatikanaji wa fedha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye mazao, ruzuku ya mbolea imewekwa nyingi, wakulima wamelima kwa wingi, kila

mahali wanahitaji wananchi wawekeze. Sasa bila umeme hatuwezi kuendelea. Kwa hiyo, niendelee kuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati tupeni Mkoa wa Ki-*TANESCO*. Usipokuja tu na hoja hiyo sisi tunaondoka na shilingi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni ambao wameingia hapa baada ya tangazo la wageni. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Esther Midimu ambao ni waumini wenzake kutoka Mkoa wa Kagera. Wageni wa Mheshimiwa Esther Midimu, karibuni sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini. Jambo la kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama tena ndani ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuwawakilisha wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe…

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, Waziri wa Madini asijekuwa amekusikia. Huyu ni Waziri wa Nishati, Madini ina Waziri mwingine…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, sawa nimekuelewa, nilimzoea kwa sababu alikuwa Wizara ya Madini, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nishati ninakushukuru kwanza jinsi unavyotuendesha kama Taifa. Kwanza kabisa napenda kukupongeza kwani toka uteuliwe tumekuwa na neema, malalamiko kidogo yanaenda yanapungua kwa wananchi. Nakupongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu nianze kwa kutoa pole kwenye jimbo langu, mvua zilizonyesha jana watu wameporomokewa na majumba, wengine wamelazwa kwenye Hospitali ya Masumbwe. Kwa hiyo, nitoe pole sana kwa wananchi wangu ili kusudi Mungu awajalie na niwaombe viongozi wote wa dini kwenye Wilaya hiyo ya Mbogwe waweze kuwaombea watu warudi kwenye afya zao.

Mheshimiwa Spika, pia Waziri Mkuu ni salamu kwako, najua kuna Kamati ya Maafa pale Wilayani pamoja na Mkoani na nitoe wito tu waendelee kuwashughulikia wananchi wangu ili kusudi waweze kusaidiwa na kila linalohitajika kwenye ngazi ya Serikali waweze kupata haki yao, hao wananchi wa Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo matano. Kwa vile mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, niungane na wenzangu wa Kamati pamoja na Mwenyekiti na Makatibu wote jinsi tulivyoishauri sekta hii. Kwenye upande wa wilaya yangu, bado nina vitongoji 196 ambavyo vinahitaji huduma ya umeme. Mheshimiwa Waziri wewe unapafahamu, nikizungumza neno Mbogwe, vijiji vyote unavifahamu, hakuna sababu ya kuvitaja. Naomba sana uendelee kunisaidia mdogo wako ili kusudi wananchi waweze kupata neema kuwa jirani na wewe kwamba niko na wewe pamoja ili kusudi kwenye hii bajeti ya shilingi 1,000,800,000,000 iweze kuwa msaada kwa Watanzania wote hata Wanambogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwenye ukanda wetu tunalima mazao, kwenye ukanda wetu watu wana mashine za kusaga, ukanda wetu una watu wana ma-*crusher* wanahitaji huduma ya umeme na Majimbo yetu Wilaya ya Bukombe na Mbogwe hatuna *transformer*. Namwomba kaka yangu kupitia bajeti yako ya shilingi 1,000,800,000,000 uweze kutenga *transformer* ili umeme wetu uweze kutulia nasi tuwe na makusudi sasa ya kusema kwamba wilaya zetu zimetulia lazima tuwe na *station* za kupooza umeme ili kusudi watu waweze kuendesha viwanda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbogwe ina vijiji 87, namshukuru Mheshimiwa Rais mpaka sasa hivi vijiji vyote vimefikiwa na umeme. Vilevile nawaamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tupitisheni hii bajeti bila wasiwasi, maana tunaona; mimi mwenyewe, tumefanya ziara mwaka uliotutuma kwenda nje kujiridhisha na kujifunza mambo fulani kulingana na sekta hii. Tulijifunza mengi, wenzangu wamesema.

Mheshimiwa Spika, ipo sababu ya kutupa nafasi ili kusudi yale tuliyoyaona India pamoja na Ethiopia kwa sababu tulipita huko, tuweze kuyafundisha hapa ili kusudi yafanyike kwa vitendo. Kwa sababu yanayowezekana India hata kwetu hapa yanawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye Hotuba ya Waziri amebainisha mambo mengi siwezi kuyapitia kulingana na muda, naiomba Serikali itoe pesa haraka kwa sababu tukizungumzia sekta hii ndiyo moyo wa Taifa letu. Pia lipo suala la mafuta, kwa vile Mheshimiwa Waziri anasimamia sekta hii, wasimamie kikamilifu. Mimi nakujua, uhakikishe kwamba unakomesha upandaji holela wa bei ya mafuta, kwa sababu mpaka sasa hivi lita ya mafuta ni shilingi 3,000 na kitu na maisha yanazidi kuwa magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme unaonekana sasa ni wa kutosha, mfikirie jinsi ya kushusha bei kwenye *unit* pamoja na kuwaunganishia watu umeme kwa sababu tuna umeme wa kutosha, hausumbui na mmetuthibitishia siku ya maonesho mbele ya Waziri Mkuu kwamba umeme tunao mwingi kuliko mahitaji. Sasa muone namna ya kuwapunguzia Watanzania matumizi ya umeme ili kusudi maisha yaweze kuwa na unafuu.

Mheshimiwa Spika, hali ya maisha ni ngumu ukijumlisha uendeshaji wa maisha kwenye sekta hii. Ukiangalia bei jinsi sasa hivi wananchi tunavyowaunganishia umeme, vipo vijiji tunavipelekea umeme kwa shilingi 300,000. Mimi naiomba Serikali iangalie upya turudi kwenye shilingi 27,000 kama zamani tulivyokuwa tunawaunganishia wananchi wetu ili kusudi waweze kufurahia matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa kwenye miji yangu 17, hii ya Masumbwe *transformer* zake Waziri zimeishakuwa. Sasa hivi wakiwasha umeme vifaa vyote vinavyofanya kazi kwa maana ya mashine za mpunga na ma-*crusher* pamoja na kadhalika na hii uunganishaji wa mita mbili tulioufanya mwaka 2023, umeme unaanza kusinzia.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kwamba *transformer* zilizopo Masumbwe, Lulombela na Lugunga ni ndogo. Kwa hiyo, tunaomba *transformer* nyingine. Kama *transformer* zilizokuwepo ni za *watts* 50, basi ziende *power meter* 100 ili kusudi waweze kupata huduma nzuri kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni vituo vya mafuta. Sheria zetu zinazuia watu kuuza mafuta mitaani, lakini kiukweli na kiuhalisia ipo miji ambayo imeendelea kwa kasi. Hata kama ukiwa hapa Dodoma, ukitoka kidogo tu, kuna watu wanaouza mafuta kwenye makopo, hawana vituo; kwenye bajeti yako, tumezungumza na hata kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi vituo vya mafuta, wapewe vipaumbele hao wanaouza mafuta kwenye makopo huko vijijini ili kusudi wajenge wao hivi vituo na Serikali irahisishe, kusiwe tena nambo mengi mengi ya kufanya. Kwa sababu wapo wauza mafuta, wanauza humo humo vijijini na wana uwezo wa kufanya hiyo kazi. Serikali iweze kuwashika mkono kuwajengea hivyo vituo vya mafuta ikiwezekana hata kupanga, wapange wananchi wale ili kusudi wawe kisheria. Hii itaondoa mgongano kwa sababu sasa hivi askari utakuta wanakimbizana na wauza mafuta mitaani na hii ni kukosa mitaji, watu hawana mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri iende ikawashike mkono machinga, maarufu kama wapiga nyoka ili kusudi waweze kusaidiwa vituo vidogo kwenye kata huko ili waweze kuuza mafuta vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba nikushukuru na kukupongeza wewe kwa jinsi unavyotuendesha na kutufundisha hapa Bungeni na unavyotupanga kwenda kwenye nchi

mbalimbali kujifunza. Nataka nikuhakikishie, huwa unatutuma tunaenda kujifundisha kabisa, kile kilichopo tunakileta huku kuja kukifundisha. Kwa hiyo tutume tena mwaka huu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** ...twende tukajifunze ili kusudi tuweze kulitoa Taifa letu hapa lilipo twende sehemu nyingine... *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga, shukurani. *(Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena. Hairuhusiwi kuzungumza na simu Bungeni. Nimeshasema mara kadhaa na kwa sababu nilikuwa mwalimu, sitachoka kusema, lakini siku ya kuwatoa nje msije mkaleta malalamiko. Nitaita mmoja baada ya mwingine ili nikukumbushe kwamba nenda kazungumze na simu nje. Mkutano huu ni wa muhimu sana na sisi ni Waheshimiwa, nasi tujiheshimu.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Venant Daud Protas, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa nafasi hii. Napenda kuanza kwa kushukuru na tunashukuru ili tuweze kuomba tena. Kushukuru ni jambo la kibinadamu lililoelekezwa na Mwenyezi Mungu hata katika vitabu vyake vitukufu. Mimi najua *Quran* Tufuku kidogo kwa Kiswahili, Mheshimiwa Twaha anajua kwa Kiarabu. Yapo maandiko

yanasema kwamba; "Waheshimuni na mwashukuru wenye mamlaka juu yenu na yule ambaye hamshukuru mtu, basi hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunavyosimama hapa tunamshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali nzima ya Awamu ya Sita akiwemo Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa nchi yetu. Kawaida yetu sisi binadamu ni kusema wakati wa changamoto na mambo yanapokuwa mazuri hatusemi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, amefanya ziara Kilombero. Nilikwenda hapo kwake nikakaa, nikamweleza kwamba Kilombero ina mgodi wa Kihansi na Mgodi wa Kidatu, lakini tunapata mgao wao wa umeme zaidi ya miaka miwili. Akaniitikia kwamba atalifanyia kazi na kweli amefika na helikopta, ametua Kidatu na Kihansi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, tangu amefika na ametoa kauli kwamba, 'hapa kuna mgodi wa Kidatu, kwa nini kilometa mbili? Pia kuna kijiji na kuna eneo umeme hakuna. Hii siyo sawa." Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba mpaka leo umeme haujakatika. Kwa hiyo, tunashukuru kwa kweli na tunaomba hali hii ya kupungua kwa umeme na kupungua kwa mgao, iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jenerali Ulimwengu ameandika katika kitabu chake; "Wakati mzuri wa kwenda kwa daktari ni wakati ambako unajisikia vizuri, mzima," unaenda unapima sukari na *pressure*. Ukishajua majibu yako, vipimo vinaonesha nini, ndiyo unamwambia daktari, nifanye nini ili niwe kama hivi nilivyo, sukari iwe kiasi hiki, au presha iwe kiasi hiki? Kwa hiyo, tunachoshauri ni kwamba hali hii inayoendelea ya kupungua kwa mgao wa umeme, vitu vinavyofanyika viwe *maintained* tuendelee kuwa na hali hii wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amefika katika maeneo yangu, kwa hiyo, nikizungumza hapa nafikiri utanielewa.

Ule mto mkubwa unaozalisha Mgodi wa Kidatu ukijaa kama kipindi hiki cha mvua kwa kweli hali inakuwa mbaya sana katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi, nitakuwa niko njiani kwenda jimboni. Asubuhi ya leo Ifakara tumeamka na mafuriko makubwa kweli kweli. Makubwa sana, karibu nyumba za Ifakara Mjini zinaingia maji. Changamoto hiyo inatokana na Mto Lumemo ambao unaenda kumwaga maji katika Mto Kilombero ambapo Mto Kilombero unaenda kumwaga maji katika Mto Rufiji na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mwalimu Nyerere ukiangalia ramani 46% ya lile bwawa ni bonde la Kilombero na ukisoma, ukiangalia ramani ya bwawa Kata ya Kisawasawa na Kata ya Kiberege ziko kwangu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuwa na mkakati mzuri, mkakati maalumu na mkubwa utaotokana labda na hiyo *community social responsibility* (fedha hizo) ama chochote kuhakikisha mto unaopita Ifakara Mjini unaenda kumwaga maji Mto Kilombero kwenda Rufiji unafukuliwa na unarudisha tuta lililowekwa na wazee zamani. Kwa sababu mafuriko ya Ifakara yanatokana na kingo, yaani kuna kingo zinajulikana kabisa zimebomoka, maji yanapita yanakuja kumwaga mjini. Zikirudishwa zile kingo na mto ukafukuliwa pale Ifakara Mjini, maji hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tuna *46%* ya bwawa mpaka sasa hivi hata *community social responsibility* hata shilingi mia hatujapata. Soma ramani ya Kilombero Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu mwangalie ramani ile muone, Kilombero na Kata ya Kisawasawa na Kiberege ziko kwangu. Kwa hiyo, naomba kwa unyenyekevu mkubwa sana jitahidini tupate mradi mkubwa wa kufukua huu mto, tuachane na hii changamoto. Hali ya watu wetu ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana *TANESCO* walitusaidia kiasi kuhusu fedha na mkandarasi yuko pale hajaanza kufanya kazi.

Nafikiri hajapewa *advance payment* kufukua huu mto. Kwa hela kidogo, hawezi kumaliza wote, lakini hata hivyo hajaanza kwa sababu ya changamoto za pesa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Halmashauri ya Mji wa Ifakara ina vijiji 48, tunaomba vile vijiji vyote zaidi ya 16 ambavyo vimeambiwa walipe shilingi 300,000 na zaidi ya kuunganishiwa umeme warudishiwe ile shilingi 27,000 kama tulivyoomba. *TANESCO* wamefanya kazi kubwa, *TANESCO* Mkoa na *TANESCO* Wilaya kuhakikisha kwamba wanapata sifa hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga…

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo katika nchi yetu na katika dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nami nianze na shukurani kubwa sana kwa Rais wetu jinsi ambavyo katika sekta hii amefanya mambo makubwa sana kwa muda mfupi sana. Tunapomsifu Mheshimiwa Rais, mara nyingi tuna-*relate* na muda.

Mheshimiwa Spika, unakuta jambo linafanyika kubwa kwa muda mfupi sana. Kwa hiyo, hata tunapopongeza kila wakati naomba sana Watanzania wawe wanaelewa kwa nini tunampongeza Mheshimiwa Rais kiasi hiki na kila anayesimama, ni kwa sababu usipompongeza Rais, kwa haya aliyoyafanya kweli wewe utakuwa ni mtu usiye na shukurani.

Mheshimiwa Spika, Rais alikuta Bwawa la Mwalimu Nyerere lina 37%, leo tunaongelea 99%, kwa miaka mitatu. Mradi wa takribani trilioni saba, wananchi waelewe tunapompongeza. Sisi wananchi wa Mkalama shukurani yetu tutaionesha mwaka 2025 kwa kufanya maajabu kwa kupiga kura kwa wale wote watakaojiandikisha kwa asilimia, tutaomba Mungu zifike 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Wizara hii kwa kazi anayoifanya. Waziri ni mnyenyekevu, mtu mwenye hofu ya Mungu, msikivu lakini zaidi ni mchapakazi. Nadhani hii ndiyo sababu, nadhani hata Mama aliona, akaona amwongezee jukumu la kumsaidia Waziri Mkuu kwa mambo haya ambayo anayafanya. Mungu aendelee kukupa maisha marefu kijana wetu Mheshimiwa Dkt. Doto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba tu Wizara, suala la kufikisha umeme kwenye vitongoji, wananchi wetu wameshauona umeme umefika kwenye vijiji. Jambo kubwa sana katika Afrika limefanyika, lakini wananchi wanaishi vitongojini, wanahitaji kuona umeme umewaka kwenye nyumba zao. Kwa hiyo, naomba sana hili zoezi ambalo sasa Serikali inajikita la kwenda kupeleka umeme kwenye vitongoji, lifanyike haraka na kwa umakini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba *REA* wawezeshwe fedha sasa za kununua *transformer* kubwa. Mawazo tuliyokuwanayo zamani ya *KVA* 50, tulikuwa tunaviona vijiji kama vijiji, lakini vijiji vyetu vya Tanzania leo hii ni vijiji vyenye maendeleo, ndiyo maana tuna Shule za Kata kwenye Kata zetu zaidi ya tatu au nne. Watu wamesoma, watu wana kazi za kuchomelea na vitu vingine. Vijiji ni utawala tu, lakini shughuli zinazoendelea kule ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sasa *REA* wapewe fedha ambazo watanunua *transformer* zenye *KVA* kuanzia 200 mpaka 315 ili ku-*cover* eneo kubwa la kijiji au kitongoji. Hata wale wananchi walioko pembezoni mwa kijiji au kitongoji waweze kufikiwa, hizi *transformer* kubwa zinakwenda mpaka kilomita sita.

Kilomita sita ukienda unakuwa umemaliza takribani kitongoji au kijiji kizima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaposema vitongoji, vitongoji vyetu wengine sisi ni sawa na vijiji vya maeneo mengine, tuna vitongoji vikubwa sana havina umeme. Kwa hiyo, tunaomba sana sasa *REA* waachane na habari ya kwenda na *KVA* 50. Hizi 50 wapeleke kwa mtu mmoja ana shamba lake au ana nini, ndiyo apelekewe hizo *KVA* 50, lakini kwenye vijiji na vitongoji vyetu ni *KVA* kuanzia 200 kwenda juu ndiyo zinaweza ku-*cover* eneo kubwa na ndiyo tutakuwa tunamaliza moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, maana yake mpaka sasa wale wenye umeme wanalalamika, kwa sababu wanauona kwa majirani, lakini na wale ambao hawajafikiwa wanalalamika. Sasa badala ya kupeleka hii kitu kuwa neema inakuwa sasa kero. Kwa hiyo, naomba sana *REA* twende na mtazamo wa kuwa na kitu kikubwa kwa sababu wananchi wetu wa Tanzania wanapenda mambo makubwa kama Rais wao anavyowafanyia mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitongoji vyetu vikubwa, kwa mfano Kitongoji kama cha Tatazi ni kitongoji kikubwa sana, kipo Kata ya Mbambala. Kitongoji cha Nzinziru, Mwadada hivi ni vitongoji sawa na vijiji havijapata umeme. Kitongoji cha Senene, Midibwi, Matere, Mtaa wa Singida pale Mwanga, hivi tunasema ni vitongoji kwa sababau ya utawala, lakini ukienda pale unashangaa ni kijiji kikubwa ambacho kina kaya nyingi na shughuli ni nyingi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ya uchapakazi wako, hakikisha tunapata umeme kwenye vitongoji hivyo ili wananchi wa Tanzania waendelee kula mema ambayo Mama yao anawapatia katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, ajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara hii, halafu nimpongeze Mheshimiwa Rais, mwaka 2020 alipokuwa anaingia, alikuta takribani vijiji vya Jimbo la Igalula 46 kati ya 58 havijapatiwa nishati ya umeme, lakini mpaka leo vijiji vimeshafikiwa na nishati ya umeme katika maeneo yote. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake wote, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya kumshauri Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo mambo machache sana ya Jimbo. Leo nitayauliza kwa maswali kwa sababu mimi ni mtu wa mwisho, nadhani na Mawaziri wanaanza kujibu. Mheshimiwa Naibu Waziri akianza kujibu ndiyo aanze kujibu maswali yangu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, kule vijijini tulipeleka umeme sahihi, lakini kuna changamoto sana ya upatikanaji wa *control number* ili watu waingiziwe umeme, pamekuwa na shida sana. Sasa naiomba Serikali katika vijiji vyangu ambavyo inaonekana *transformer* ni ndogo hasa katika Kata ya Tura, Kijiji cha Tura, Izumba, Mwisole, Lutende, Kizengi na Lutoni, hebu naomba muongeze *transformer* ili wale wateja wapate umeme.

Mheshimiwa Spika, hii itakuja kutuletea utenganishi. Tuliwaambiwa wananchi tutawaunganishia umeme kwa shilingi 27,000, muda wenu ukiisha mtawapelekea kwa shilingi 320,000 wakati sisi Serikali ndiyo tuliwachelewesha kwenda kuwanunganishia. Kwa hiyo, naomba mwapelekee mapema ili waweze kupata nishati ya umeme kwa bei elekezi ya shilingi 27,000 kwenye hivi vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili tuliambiwa hapa na Mheshimiwa Waziri, bajeti iliyopita tulileta vitongoji 15 kila mmoja humu kwenye Bunge lako. Tukaandika, tukaenda *stationery,* tukachapa vizuri ili waweze kuona vizuri maana wengine miandiko siyo mizuri. Tukawachapia kabisa waone vitongoji kwa kitongoji. Hivyo vitongoji lini vitaanza kupelekewa umeme? Kwa maana tumeshaenda kusema, bajeti ya kwanza inaenda ukingoni na hii pia tunapitisha nyingine.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ipeleke umeme kwenye vitongoji 15 vya Jimbo la Igalula ambavyo niliorodhesha ili waweze kufikiwa na nishati ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya mradi huu wa *REA*. Pia kuna changamoto kubwa sana ya *transformer* kuharibika. Leo hii tumekuwa na sisi *customer care* wa *TANESCO,* tunapokea *message,* tunapeleka kwa *TANESCO* ndiyo watufanyie ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunapeleka *transformer* na wakienda kuichukua, wanachukua zaidi ya miezi miwili au mitatu? Mwananchi anashindwa amdai nani? Wakienda *TANESCO* wanaambiwa huu mradi bado uko kwa Mkandarasi *REA*, akienda *REA* wanasema *TANESCO* anasubiri aje akague *transformer*. Wananchi hawatakiwi kujua *TANESCO* na *REA* ni nani, wanahitaji umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali, nendeni mkatatue matatizo ya ndani. Leo hii nimeambiwa kule Lutona kule *transformer* wamebeba, wiki iliyopita ilikuwa Isuli, kule *transformer* walibeba miezi mitatu mpaka ulivyoniletea banda hapa, nikambananisha Mkandarasi, *TANESCO,* kesho yake wakapeleka. Sasa tutaweza hivi!

Mheshimiwa Spika, umeme ukikatika, wakibeba *transformer* na mimi nianze kushinda tena kwa Waziri au kwa Naibu Waziri, nakaa pale nasubiri. Naomba sasa watumishi wa *TANESCO* waweze kufanya kazi yao kwa uhakika. Wananchi wanalalamika kule wakipata hitilafu, umeme unarudi kwa kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Serikali ina nia njema sana ya kutengeneza namba moja ya kupiga simu, wanasema *one call center,* wametengeneza mfumo mzuri sana lakini bado kuna changamoto. Leo mwananchi wa Igalula anapata tatizo sehemu inaitwa Makoyesengi anapiga Dar es Salaam. Mtu wa Dar es Salaam amekulia Kilimanjaro, unapomwambia Kijiji cha Makoyesengi katika kukiandika pale anakosea, anakuja kuwapa

taarifa huku wanaanza kukitafuta Kijiji na kule wananchi hawapati umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba hii hali ya kupiga namba moja mliyoiweka ni nzuri, lakini wekeni na namba kila Wilaya iwe na namba yake ili mwananchi akipata shida aweze kupiga kule kwenye Wilaya yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona viashiria vya muda kwisha, niseme tu, naunga mkono hoja ya Wizara hii na bajeti hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Pia naomba kipekee kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya yeye pamoja na wasaidizi wake wote akiwemo Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Viongozi wote wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi hizo zinaambatana na ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa lile ni kubwa, lakini linataka kututoa Watanzania hapa tulipo, kutupeleka katika hatua nyingine zaidi ya kiuchumi. Ni bwawa kubwa ambalo kama tutalitumia vizuri, manufaa yake tutayaona na tumeanza kuyaona kwa sababu umeme umeshaanza kuzalishwa. Shukurani kwa Viongozi wa Chama na Serikali ambao mmesimamia bwawa lile.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kwa Watanzania wote kuendelea kutunza miundombinu ile hasa wale ambao wanatoka maeneo jirani yenye mito inayoingiza maji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, tuendelee kutunza vyanzo vyetu ili mradi wetu uwe endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue pia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati, kwa jitihada kubwa ambazo wamezifanya katika sekta hii ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Newala Vijijini kwa mfano, tunavyo vijiji 107, lakini wakati naingia ni vijiji 31 tu ndivyo ambavyo vilikuwa na umeme. Leo ninapoongea, vijiji 35 tayari vimeshawashwa umeme, vijiji 13 vimeshawekewa *transformer* bado kupimwa umeme uwashwe, vijiji 25 vinaendelea na kazi katika hatua mbalimbali. Ni vijiji vitatu tu ndiyo ambavyo bado na ninaamini kwa jitihada na namna ambavyo Waziri na timu yake wanafanya kazi, basi vijiji hivi navyo vitafikiwa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi, katika mradi huu wa *REA* naomba, hivi vijiji ambavyo nimezungumzia ni vile ambavyo vimefikiwa na kilometa moja tu ya ujenzi wa umeme. Kwa hiyo, maeneo mengi ya taasisi kwa mfano, shule, zahanati, nyumba za ibada, zote bado hazijafikiwa na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo ni kumfikishia mwananchi huduma na kumpunguzia mzigo, naiomba Serikali, zile kilometa mbili ambazo zinaenda kujengwa katika kila kijiji, basi tusimamie zijengwe kwa haraka ili taasisi nilizozitaja zipate umeme na wananchi waweze kuhudumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, leo hii unaenda kwenye zahanati ambayo imejengwa vizuri, kwa mfano kule Newala Vijijini kuna zahanati ya Namangudu, zahanati nzuri kabisa ya kisasa haina umeme. Sasa mama anaenda kujifungua, anamulikiwa kwa mwanga wa simu, hapana! Siyo sawasawa, kwa sababu Serikali inasema kuongeza kilomita mbili itakuwa ni jambo la haraka. Naomba tumsimamie mkandarasi aliyepewa kazi ili kazi hii ikakamilike haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ipo changamoto nyingine ya kukatikakatika kwa umeme hasa Mkoa wa Mtwara. Naomba sana, najua Serikali inafanya jitihada kubwa, imeshaleta mtambo

wa megawati 20, tumeona umeme upo, ila shida ni miundombinu. Ninaiomba Serikali isimamie miundombinu ili umeme ule usikatikekatike sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, najua zipo jitihada nyingine nyingi tu. Kwa mfano, wameshafunga baadhi ya maeneo *auto recloser* ili kupunguza umbali wa kusafirisha umeme. Naomba tuisimamie kwa haraka ili umeme usikatike maeneo mengi kwa wakati mmoja. Najua ni gharama, lakini inawezekana kwa sababu tumeshaamua, basi tufanye hima umeme uwafikie wananchi, na tupunguze hii adha ya kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba *long term plan* iwe ni kuufikishia Mkoa wa Mtwara na Lindi umeme kutoka gridi ya Taifa. Mpaka sasa umeme haujafika Gridi ya Taifa. Tunajua Serikali inayo mikakati ya dhati ya kufikisha umeme, lakini naomba usimamizi wa haraka zaidi na tupeleke pesa ili tupate Gridi ya Taifa kwa Mkoa wa Mtwara kutokea kule Songea kama ambavyo mmetuahidi na wananchi wetu wa Mtwara - Newala waweze kufanya uwekezaji mkubwa sasa. Wengi wanashindwa kuwekeza katika maeneo yetu kwa sababu ya ukosefu wa umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Newala unakutana na viwanda vya korosho vimekaa tu kama maghala ya kutunzia bidhaa, lakini inawezekana sababu mojawapo ya wale wawekezaji kushindwa kuendelea kubangua korosho ni kukatikakatika kwa umeme. Kwa hiyo, naiomba Serikali isimamie tupate umeme kutoka gridi ya Taifa ili uwekezaji Mkoa wa Mtwara ukawe wa uhakika na kuinua kipato cha wananchi wake. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu yake ya kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mwalimu Nyerere kazi imeendelea kutoka 32.82% hadi 97.43%; tunampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Umeme wa *REA* hivi sasa tumefikia zaidi ya vijiji 11,850 sawa na 96.2% na sasa hivi vimebakia vijiji 468.2. Mheshimiwa Rais anaupiga mwingi sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikiwa sana kudhibiti mgao wa umeme nchini, pia Serikali imefanikiwa kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri zinazofanywa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuja na Mradi wa Nishati Safi ya Kupikia hasa mitungi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, nishati safi itasaidia wanawake kuokoa muda wa kutafuta kuni porini na kuokoa misitu na pili nishati safi itasaidia kulinda afya za akinamama na watoto hasa kwa ugonjwa wa kansa unaotokana na moshi jikoni.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali iwekeze zaidi kwenye miundombinu ya umeme ambayo imechakaa. Hivi sasa uchakavu wa miundombinu ndiyo inayopelekea umeme kukatika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara hii ya Nishati na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya kwa kuhakikisha Taifa letu linaendelea kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; elimu kwa wananchi iendelee tolewa kuhusu matumizi ya gesi majumbani na pia Kikosi cha Zimamoto washirikishwe kwenye kutoa elimu hiyo kwa wananchi wajue matumizi ya kwamba hayana athari yoyote kwamba gesi ya sasa hivi ipo salama na haina madhara yoyote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kuwaletea wananchi wa Tanzania maendeleo makubwa, lakini pia pongezi zangu zimwendee Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na msaidizi wake wa karibu Mheshimiwa Judith S. Kapinga ambao hakika wanaitendea haki sana Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema jana kwenye mchango wangu wa kuzungumza kuhusu kusuasua kwa mkandarasi anayetekeleza Mradi wa *REA* Mkoa wa Rukwa, hili jambo limekuwa na sintofahamu nyingi sana. Mimi binafsi kama Mbunge wa Jimbo la Kwela ambalo ndilo lina vijiji vingi ambavyo havijapata umeme kwa awamu ile ya kilometa moja nimefanya vikao vingi sana bila mafanikio yoyote ambapo mpaka sasa kati ya vijiji 40 vya Mkoa wa Rukwa ambavyo havijapata umeme, vijiji 17 vyote ni vya Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Spika, vijiji ambavyo havijapata umeme 17 katika hivi, vijiji 16 mkandarasi ameanza kufanya kazi na kimoja bado hajaanza kufanya kazi kabisa. Vijiji ambavyo mkandarasi bado hajavuta waya *line* kubwa amesimika nguzo tu ni Kisalala, Mnokola, Mititi, Ntumbi na Kitete.

Mheshimiwa Spika, vijiji ambavyo mkandarasi amevuta *line* na transfoma zimefungwa lakini havijawashwa ni Kazi, Tululu, Kilando, Mpona, Kapewa, Mtetezi, Zimba, Mnazimmoja Asilia, Mumbai, Kinambo na Kalumbaleza A. Kijiji ambacho hakijafanyiwa kazi kabisa ni Kijiji cha Liwelyamvula.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuunda timu yake ya uchunguzi ili kutambua chanzo cha huyu mkandarasi kususua kwa muda mrefu ni nini, lakini pia hatua za haraka zichukuliwe ili wananchi wa vijiji vyote 17 vya Jimbo la Kwela waweze kupata hii nishati muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto tulizopata mkandarasi huyu imelazimu binafsi kufuatilia pia maeneo mengine ambayo ametekeleza miradi bado taarifa zake sio za kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa ushirika wa Kampuni ya Pomy na Qwihaya, kwa taarifa za nyuma Qwihaya ni kampuni ya nguzo ila kwa sasa ni mkandarasi wa umeme pia Pomy ni mkandarasi wa umeme tangu kipindi cha nyuma hadi sasa. Mkandarasi Pomy alishawahi kupewa kazi ya mradi wa umeme kwa Mkoa wa Tabora, alitekeleza mradi huo kwa kiwango kisichokubalika na hakumaliza, lakini adhabu na lawama ilielekezwa kwa wafanyakazi wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, tangu anaanza mradi huu wa Rukwa kwa kushirikiana na Qwihaya, kumekuwa na migogoro kati yao isiyoisha na kusababisha mradi kutokwenda kwa wakati na kuwa na dalili zote za kutokamilika na huenda mgogoro ukawa ni sawa na kilichotekea Tabora. Tutambue kuwa mradi huu wa Rukwa ulianza kutekelezwa tarehe 9 Julai, 2021 na mwisho wa mradi huu ilikuwa ni tarehe 8 Januari, 2023 ambapo alikuwa amefikia 38%, *REA* wakaongeza muda wa miezi minne hadi tarehe 30 Aprili, 2023 ili kukamilisha mradi, lakini hadi mwisho wa mwezi wa nne utekelezaji wa mradi ulifikia 41%.

Mheshimiwa Spika, pia *REA* wameongeza muda wa kutekeleza mradi huu hadi tarehe 31 Oktoba, 2023 lakini bado kazi haikukamilika. Cha kusitisha aliongezewa tena muda mpaka Desemba, 2023 lakini bado kazi haikuisha, kaongezewa tena mpaka Machi, 2024 na kwa taarifa iliyopo sasa ameomba *extension* nyingine tena, jambo hili linasikitisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maendeleo haya ya kusuasua ya mradi kwa Mkoa wa Rukwa ni baada ya kutumia nguvu na kuwa na tabia ya kutembelea mradi mara kwa mara, kuwa na vikao vya kujadili mwenendo wa mradi na kuwa na maelekezo, lakini hakuna juhudu zozote za makusudi kuhakikisha mradi unakamilika.

Kuhusu hali ya kiusafiri katika Jimbo la Kwela kwa ofisi ya *TANESCO;* kwa upande wetu kama shirika Mkurugenzi Mtendaji alifanya ziara tarehe 5 Aprili, 2024 katika Mkoa wa Rukwa ambapo kati ya changamoto aliyopewa ni uhaba wa usafiri wa uhakika kwa wananchi wanaoishi katika Bonde la Ziwa Rukwa na alichukua na utatuzi unaendelea. Hivyo niendelee kumuomba Mtendaji Mkuu wa *TANESCO* kulifanyia kazi jambo hili kwani kwa sasa watendaji wa TANESCO hasa kule Bonde la Ziwa Rukwa wanatumia bajaji ambazo kutokana na miundombinu ya barabara kutokuwa rafiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwakilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na Naibu wake Mheshimiwa Judith Kapinga pamoja na wataalam wa Wizara kwa kazi kubwa ya kusimamia sekta ya nishati hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwani hadi kufikia mwezi Machi, 2024 jumla ya vijiji 11,837 sawa na 96.37% ya vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara vilikuwa vimeunganishiwa huduma ya umeme. Hii ni hatua kubwa na ni rai yangu kwamba zoezi la kuunganisha umeme katika maeneo yaliyobaki katika Jimbo la Moshi Vijijini litakamilika ili wananchi wanufaike.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye maeneo mawili; kwanza ni umuhimu wa Serikali kuwekeza kikamilifu kwenye umemejua, na pili ni changamoto

ya umeme katika baadhi ya maeneo ya Jimbo la Moshi Vijijini ambayo hayajaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, huenda huko mbele ya safari tutakumbana na tatizo kubwa la kupata umeme unaozalishwa na maji. Hivyo basi, ninaishauri Serikali iwekeze kikamilifu kwenye matumizi ya nishati safi na salama itakayotumia jua.

Mheshimiwa Spika, nishati ya jua huundwa kwa paneli zinazokusanya nishati ya mwanga na baadaye hubadilishwa kuwa nishati ya umeme. Umemejua ni chanzo cha uhakika cha nishati ya umeme na kama Serikali itahamasisha uwekezaji katika Umemejua hasa katika maeneo ya vijijini, hii inaweza kuwa suluhisho la kuwapatia watumiaji umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ishirikiane na wadau wa nishati ya jua ili teknolojia hii iweze kuwafikia watumiaji kirahisi. Hii ni pamoja na kuondoa kodi mbalimbali kwenye vifaa vya Umemejua vinavyoagizwa kutoka nje ili kuwapunguzia wananchi bei.

Mheshimiwa Spika, kwenye changamoto za umeme jimboni kwangu, ninaiomba Serikali itusaidie katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza katika Kata ya Arusha Chini, kwenye Kijiji cha Mikocheni, Vitongoji vya Masaini na Mashimo ya Mchanga hakuna umeme. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vitongoji hivi.

Pili, katika Kata ya Okaoni, vitongoji vingi katika Vijiji vya Sisamaro, Omarini na Mkomilo vinahitaji kuunganishwa kwani wananchi wamesubiri kwa muda mrefu.

Tatu, kata ya Kindi, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana, katika Kata ya Kindi, Kijiji cha Chekereni Weruweru, Vitongoji vya Miembeni na Kisiwani havina umeme kabisa. Pia baadhi vitongoji vya Vijiji vya Kindi Juu na Kindi Kati havijapata

umeme. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji na vitongoji hivi.

Nne, katika kata ya Mbokomu, kama nilivyoomba kwenye bajeti za miaka mitatu iliyopita, katika Kata ya Mbokomu, Vitongoji vya Mmbede Kyaroni, Tema na Masanga na baadhi ya maeneo ya Korini Kati havijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vitongoji hivi.

Mheshimiwa Spika, tano katika Kaya ya Mabogini, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, katika Kata ya Mabogini sehemu ambazo hazijapata umeme hadi sasa ni Vitongoji vya Sanya *"Line A"* na Mjohoroni vilivyopo katika Kijiji cha Mabogini; pia Kitongoji cha Uru katika Kijiji cha Muungano; katika Kijiji cha Maendeleo, Vitongoji vya Mshikamano na Uarushani; Mgungani katika Kijiji cha Mtakuja; katika Kijiji cha Mserekia, hakuna umeme katika Vitongoji vya Mbeya Kubwa, Mbeya Ndogo, Remit, Mkwajuni na Mafuriko.

Mheshimiwa Spika, aidha Kijiji cha Mji Mpya, Kitongoji cha Utamaduni hakijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kimochi, Kitongoji cha Kiwalaa kilichopo Kijiji cha Sango, Kitongoji cha Iryaroho kilichopo katika Kijiji cha Mowo, na Kitongoji cha Maryaseli katika Kijiji cha Lyakombila havina umeme, ninaiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo niliyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kibosho Mashariki; kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, Kata ya Kibosho Mashariki inahitaji huduma katika Kijiji cha Sungu, Vitongoji vya Kyareni na Nkoitiko havijaunganishwa; katika Kijiji cha Singa, Kitongoji cha Singa Juu hakijaunganishwa; katika Kijiji cha Mweka, Vitongoji vya Mweka Juu na Omi havijaunganishwa, hivyo ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji na vitongoji vilivyotajwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kibosho Kati, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, Vijiji vya Uri na Otaruni umeme una nguvu kidogo *(low voltage)* na kunahitajika transifoma, na katika Kijiji cha Otaruni, Kitongoji cha Ngoroshi hakuna umeme, na tunaomba wananchi wapatiwe huduma.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Uru Mashariki; kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, katika Kijiji cha Materuni, Kitongoji cha Wondo hakijaunganishwa, hivyo ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye kitongoji hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwanza kwa ushirikishwaji na wepesi katika ku-*respond* kwenye changamoto kila zinapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, pili nawapongeza sana *REA* ambao tarehe 17 Aprili, 2024 walitoa mafunzo ya nishati safi ya kupikia kwa viongozi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga ambapo pia mafunzo hayo yalihudhuriwa na viongozi wa dini na wazee maarufu wa Mji wa Mafinga. Katika mafunzo hayo Mkurugenzi wa Nishati Mbadala kutoka *REA* Bi. Advera Mwijage alitoa taarifa kuhusu hali ya umeme na hatua za utekelezaji wa hatua ya Ujazilizi *2C* na pia alieleza fursa ya mkopo wa vituo vidogo vya mafuta somo ambalo liliwavutia wengi. Kwa ufupi mafunzo hayo sambamba na kugawa mitungi 350 ilifanikiwa sana na tunawashukuru sana *REA*.

Pili, naomba kushukuru utendaji mzuri wa Meneja wetu wa *Tanesco* Mhandisi Modest na timu yake, amekuwa *very sharp* hasa katika mawasiliano, sote kuanzia Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Madiwani tunashirikiana naye vizuri mno na kwa wakati. Ni kawaida yetu binadamu hasa sisi wanasiasa kutoa taarifa za kulalamika tu, lakini mtu akifanya vema tuna-*mute*. Hivyo nimeona ni vyema niseme kuhusu utendaji mwema na wa ushirikiano kutoka kwa Mhandisi Modest. Tunaomba kama

anahama basi iwe *vertical* kwamba anapanda, lakini kama ni *horizontal* basi ni afadhali abakie Mufindi/Mafinga.

Tatu, suala la bei kwa sisi ambao kwa mujibu wa ile Sheria ya Mipango Miji inayosema kwamba eneo kutambulika kuwa mji kuna vigezo ambavyo kimsingi kuna maeneo bado ni vijiji, kwa sheria hiyo vijiji, hivyo vinakosa sifa ya kupata umeme kwa bei ya vijijini; mfano Mafinga ni mjini, lakini kuna maeneo ni vijiji kijamii na hata kiuchumi, kwa hiyo, bei ile ya shilingi 360,000 ni kubwa mno, nimeuliza maswali mara kadhaa, majibu ni kwamba kuna timu imeundwa kupitia maeneo hayo ili kuja na majibu ya *way forward*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo suala hili sasa ni mwaka wa pili hakuna majibu, inawezekana kabisa hii bei ya shilingi 27,000 ikawa ni mzigo mzito kwa Serikali, hata hivyo mnaweza kuja na bei tofauti tofauti kulingana na maeneo, kwa mfano vijijini kabisa inaweza kubakia shilingi 27,000, lakini baadhi ya maeneo ambako ni kama *peri-urban* pawepo bei ambayo kidogo ni nafuu. Kwa mfano Mafinga kuna maeneo kama Ndolezi, Luganga, Mtura, Sao Hill na kadhalika inasomeka kuwa ni Mafinga Mjini lakini uhalisia wa kipato kwa maana ya uchumi na hata kijamii maisha ni ya kijijini, kwa sababu hiyo maeneo ya aina hiyo iwepo bei elekezi ambayo sio shilingi 27,000 na wala sio shilingi 360,000 lakini inaweza kuwa hata shilingi 100,000 kulingana na namna ambavyo hiyo timu ambayo tuliambiwa kuwa imeenda kufanya mapitio imejionea.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; katika ujazilizi yapo maeneo imeonekana kuwa yapo mbali na *HT* hivyo vitongoji kadhaa Mafinga vitakosa fursa kwa sababu hiyo, hivyo naomba tuone uwezekano kupitia *TANESCO* kupata *HT* ili kuwezesha *REA* kupitia mkandarasi wa ujazilizi waweze kuendelea.

Mwisho, ni lini utekelezaji wa ahadi ya vitongoji 15 kila jimbo utaanza? Hii ni kwa sababu suala hili limo kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 na bado kama mwezi mwaka wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi kufuatia kuwasilishwa kwa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Dkt. Doto Mashaka Biteko na timu nzima kwa kazi nzuri na yenye matumaini makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro imekuwa na tatizo kubwa la kukatika umeme kila siku na hata kudumu kwa siku Nzima, ninaiomba Wizara itafute suluhu ya changamoto hii ili wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro waweze kujikita kwenye shughuli za uzalishaji bila kukwamisha.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi wa vijiji vya Wilaya ya Ngorongoro waunganishiwe umeme kwa bei elekezi ya shilingi 27,000 kwani wananchi hawataweza kuunganishiwa umeme kwa bei ya shilingi 515,000 kwa nguzo, wananchi wengi wameshindwa kuunganishiwa umeme kwa sababu ya bei ya nguzo kuwa kubwa ukilinganisha na uwezo wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ipeleke umeme kwenye Kijiji cha Pinyinyi ambacho mpaka sasa hakijapata umeme na wananchi wetu wanaona kama wametengwa, kwani umeme umefika kwenye eneo la Kitongoji cha Masusu badala ya makao makuu ya kijiji ambapo ndipo kuna mji.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ianze utekelezaji wa mradi wa umeme kwenye vitongoji 15, vitongoji vya Mijitu, Bwelo, Kirangi, Katoregani, Magunkune, Luselebwe, Madukani, Orkiu Juu, Embulmbul, Lopolun A, Site A, Soitsambu, Esero, Embaash na Kapongoni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lushoto lina vitongoji vyenye idadi kubwa ya watu na wingi wa nyumba, yaani kitongoji kimoja cha Lushoto ni sawa sawa na vijiji viwili vya maeneo ya mabondeni. Kwa hiyo, tunaomba vitongoji vyetu vihesabiwa kama vijiji kutokana na ukubwa wa vitongoji vyenyewe na wananchi wa Lushoto wanajua umuhimu wa umeme, na ndiyo maana imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa Wabunge wa Lushoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo mafupi, naomba vitongoji vifuatavyo viweze kupatiwa umeme kwa maana imekuwa ni kero kubwa; kwa Kata ya Gare ni Vitongoji vya Gare Kaya, Zeta, Kwetango, Kwemdee na Kumbamtoni, Kwemabanda. Aidha kwa Kata ya Kwemashai ni Kwemulua na Golani na Kwemagemo.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Ubiri ni Mziwaishi na Misheni pamoja na Kibago. Aidha katika Kata ya Kilole ni Ula, Kilole Kaya na Kwebarabara.

Katika Kata ya Kwekanga ni Kwemishai, Kwemkashi, Bombo Juu na Kweboma; na katika Kata ya Mlola ni Muheza, Migambo, Mtae na Hondelo A na B na Maweni.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Malibwi ni Kwawambugu, Zahanati na Kwawambugu B; Ngaloi, Mzizima, Mpalai na Ngaloi A; Ngindoi Ofisini, Mlesa na Mavovo. Aidha, katika Kata ya Kwai ni katika Vitongoji vya Kimunyu, Kwemagemo na Kahalawe; na katika Kata ya Migambo ni katika Vitongoji vya Malunga, Milungui juu, Kwebalasa na Mhande.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Makanya ni katika Vitongoji vya Kwemshazi Mboghoi na Mbokoi; Kaghambe Kizelui na Lunguza na vitongoji vyake. Aidha katika Kata ya Mbwei ni

Kwasemaghera, Pongwe, Kidandi na Kweganga, hivyo ni baadhi tu ya vitongoji katika Jimbo la Lushoto, kati ya vingi vilivyobaki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo gharama ya gesi ipunguzwe ili wananchi wetu waishio vijijini waweze kumudu kununua gesi.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Kapinga na mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Naomba nichangie mambo matatu tu. Kwanza naungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza sana mtoa hoja, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na timu yake akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba sisi ambao tunamsaidia anayetusimamia, ana sifa nyingi, lakini utulivu ni jambo la msingi sana. Hapa katikati tulikuwa na wakati mgumu sana wa hali ya umeme kutokana na upungufu uliokuwepo, lakini Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko alikuwa ametulia, anafanya kazi kwa utulivu wa hali ya juu. Nadhani hiyo ni shule kubwa sana ambayo ametufundisha. Nawashukuru wataalamu wake kwa ushirikiano ambao wanampa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni muktadha kidogo tu. Katika miaka 20 iliyopita, mwaka 2001 – 2021 nchi yetu ilipoteza hekta milioni 2.86 za misitu na nchi yetu wataalam wa misitu wanasema angalau 40% ni *forest cover,* na tunapoteza takribani asilimia moja ya misitu kila mwaka ukilinganisha na wastani wa dunia ambayo inapoteza, ni 0.5%. Sababu kubwa ni kukosekana kwa nishati mbadala ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia unaona kwamba, pamoja na jitihada kubwa ambazo tumezifanya kati ya mwaka 2002 – 2022 tulipunguza kiwango cha kutumia kuni kwa takribani 20% kutoka 77% mpaka 55.5%. Kwa hiyo, tumepiga hatua katika miaka 20 lakini bado watu wetu 55.5% wanatumia kuni kwa takwimu za *NBS* mwaka 2022, na 26% wanatumia mkaa, na kama 14% wanatumia gesi ama umeme. Sasa tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tunafanya nini? Ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, moja ya eneo kubwa ambalo amelikazania ni suala la kutoa nishati safi kwa ajili ya kupikia. Jambo hili kwa bahati nzuri, mwaka 2023 kwenye *Dubai Expo* aliweza kuzindua programu maalum ya kuwapa akina mama siyo tu Watanzania, lakini Waafrika, programu maalum ya kupeleka nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi yetu sisi kama wasaidizi wake ni kuweka sera na mipango mizuri kukamilisha hiyo *vision*. Tunayo mambo matatu ambayo tunayafanya. Moja ni miradi hii ya *REA*. *Focus* kubwa tukishapeleka miradi ya *REA* vijijini inamaanisha kwamba, wanawake wengi watatumia umeme kwa ajili ya kupikia na kwa hiyo, kuokoa afya zao, pia kuokoa misitu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ni suala la bei. Wengi wamesema hapa, bei ni kubwa. Kuanzia mwaka huu wa fedha na mipango ijayo, mambo mawili ya kuzingatia ambayo tutaenda kuyafanya, na tutaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie kwa muda mfupi, ni *Finance Bill* ya mwaka huu. Tulikuwa tunaongea na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa kwamba lazima tuweke hatua za kikodi ambazo zitaelekeza kupunguza gharama za matumizi ya gesi na umeme kwa wanawake hususan vijijni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la kodi ni suala la Bunge na Serikali tutaleta mapendekezo hapa tuliangalie ili bei zipungue na wanawake wengi zaidi waweze kutumia njia hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hii miradi mikubwa ya umeme ambayo tunaizungumzia, matumizi yake ni mawili tu. Matumizi ya kijamii kama hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza hapa, nyumbani kuwasha taa na kupikia, pia matumizi makubwa sana ni kwenye suala la uzalishaji, viwanda, kilimo na kadhalika. Kwa sasa takribani zaidi ya 50% ya umeme wote ambao tunautumia hapa Tanzania, unatumika Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani kwa sababu ndiko ambako kuna viwanda vingi. Kwa hiyo, hili suala la kuendelea kuzalisha umeme mwingi ni muhimu, na Serikali katika mipango yake itaendelea kuweka mkazo, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, suala la *energy mix* ni muhimu kwa sababu tunatumia zaidi gesi pamoja na maji, lakini huko mbele lazima umeme wa jua na upepo pamoja na ule wa *geothermal* ambao Mheshimiwa Waziri aliongea jana, tuendelee kuukazania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lengo la Mheshimiwa Rais ambalo ametupatia, tupunguze matumizi ya kuni na mkaa kwa 88% ifikapo mwaka 2034, na ametuwekea lengo kwamba *by 2034* angalau 10% peke yake ya watu wetu wanaotumia kuni na mkaa wabaki huko, lakini 90% watumie nishati safi.

Mheshimiwa Spika, hili ni lengo kubwa ametupatia kwa kushirikiana nanyi Waheshimiwa Wabunge na sekta binafsi. Tunaamini ni lengo ambalo linaweza likakamilishwa. Tutafanya kila liwezekanalo na katika mipango ijayo mtaona, tutaendeleza vizuri sana mikakati ambayo tunayo kufikisha 10% ifikapo mwaka 2034 wanaotumia mkaa pamoja na kuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, nchi yetu katika kipindi hiki cha mvua imejaliwa mvua nyingi ambayo inageuka kuwa adha. Mpango wa Serikali ni kuendelea kujenga mabwawa ili haya maji mengi tuweze kuyaokota, tuweze kuyadaka ili yatumike siyo tu kwenye umeme, lakini pia kwa lengo la kutumika katika maeneo ya kilimo kama ambavyo tumesema kwenye mpango wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu, katika mpango ambao tutawasilisha tarehe 13 Juni, mwaka huu, 2024 mambo haya tutayaainisha kwa kina, lakini lengo ni kuona kwamba tunaokoa afya za wananchi wetu kwa kuwapa nishati safi ya kupikia lakini pia tunaokoa misitu yetu na kulinda mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 34(6) tunakaribia kulihoji Bunge, kwa hiyo, hatutasitisha mpaka tukamilishe kazi iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati, halafu mtoja hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku njema ya leo. Kipekee na kwa dhati ya moyo, naomba kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa unaofanyika katika Sekta ya Nishati. Hii imejionesha kupitia miradi ya kielelezo na miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa kupitia sekta zetu ndogo za mafuta, gesi pamoja na umeme.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ni kielelezo cha uchapakazi na uzalendo wa kweli. Tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu amwezeshe kutekeleza majukumu yake siku zote kwa heri na baraka tele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kwa kuendelea kutusimamia na kutuongoza vyema katika sekta yetu ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa naomba kumshukuru sana Naibu Waziri Mkuu na Waziri wangu wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mshaka Biteko kwa kuendelea kutuongoza

vyema. Amekuwa kiongozi mwema sana kwangu na watumishi wengine wote katika Wizara ya Nishati na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati. Amekuwa kiongozi anayetusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yetu kwa azma na neema. Tunamwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia aweze kutumikia majukumu yake kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru wewe, Naibu Spika pamoja na Katibu wa Bunge kwa kuendelea kutuongoza vizuri hapa Bungeni. Kipekee naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako hili Tukufu kwa kuendelea kutuunga mkono. Tunathamini sana maoni yenu ambayo mnatupatia na ushirikiano mkubwa mnaotupatia katika kutekeleza majukumu yaliyo katika Wizara yetu ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nilishukuru Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa ambao wao ndiyo walinipa dhamana ya Ubunge wa Vijana kupitia Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi. Baraza hili linaongozwa na kaka yangu *Comrade* Kawaida Mohammed Kawaida. Namshukuru sana yeye, Mwenyekiti wetu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa na Wajumbe wote wa Baraza kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Ubunge wa Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Wajumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvama. Ninapoelekea mwisho wa shukrani zangu, kwa kuwa mimi ni Diwani wa Halmashauri ya Mbinga Vijijini, naomba niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Mbinga kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Naomba niwaahidi kwamba nitaendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyomaliza shukurani zangu, naomba nimshukuru sana mume wangu na familia yangu kwa kuendelea kunivumilia na upendo mkubwa wanaonipatia. Nathamini sana, nami ninawapenda na kuwathamini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo, naomba nijielekeze sasa kwenye kuchangia hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na nishati safi ya kupikia, nitasema kidogo kwa sababu Profesa ameeleza vizuri sana. Uhai na afya ya dunia yetu ya sasa ipo kwenye kutunza mazingiara yetu. Linapokuja suala la nishati safi ya kupikia, hii ndiyo nyenzo muhimu ya kutusaidia kutunza mazingira yetu kwa ajili ya afya na dunia ambayo tunaishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, ule Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia ambao tulikuwa tunaungoja, umeshapitishwa na Baraza la Mawaziri na upo tayari kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipomshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ndiye amekuwa kinara wa nishati safi ya kupikia na ametusaidia sana kwa kuwa *champion* namba moja Tanzania, Afrika na ulimwenguni kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, azma yetu ni kuongeza kasi ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, lakini kubwa, pamoja na kuongeza kasi, tunataka tuwawezeshe wananchi waweze kutumia nishati safi ya kupikia ikiwemo gesi ili tuweze kabisa kuondoa matumizi ya mkaa pamoja na kuni. Dhumuni la mkakati wetu ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati safi, salama, endelevu na yenye uhakika.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu bado tuna hatua kubwa sana katika kuhakikisha tunaondoa kabisa matumizi ya mkaa, lakini ni suala ambalo hatuwezi sisi Serikali kulifanya peke yetu. Ndiyo maana tunaendelea kuomba Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kushirikiana katika kupiga vita matumizi ya mkaa na kuni ili kuhamasisha wananchi waendelee kwenda na matumizi ya nishati safi ya kupikia kama ambavyo tumeanza kupitia mitungi ambayo tunaigawa.

Mheshimiwa Spika, mikakati ambayo tunayo inatekelezeka sana. Jambo ambalo linatutesa sisi ni mazoea tu ya mkaa kwa

sababu wapo wengi ambao wana uwezo wa kutumia nishati ya gesi. Ni kwamba tu watu hawaamini kuwa wali nazi wa gesi pia ni mtamu au maharage ya kutumia *pressure cooker* ambayo inatumia umeme mdogo pia ni mtamu. Ni kuongeza tu mapishi. Kwa hiyo, tuendelee kushirikiana kwa pamoja kutoa elimu tuweze kuhamia kwenye nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na gharama. Tayari tumeshaanza kufanyia kazi kupitia *REA* na wadau wetu wengine tunatoa ruzuku. Jambo kubwa lilikuwa ni kwenye kuanza matumizi ya gesi kwenye kupata jiko na vifaa, lakini kupitia *REA* tunatoa ruzuku ya mitungi na mpaka sasa hivi tumetoa mitungi 83,500 na tunao mkakati wa kutoa mitungi 450,000 ili kuweza kurahisisha matumizi ya awali ya gesi ili kuongeza kasi ya matumizi makubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kwa kushirikiana na kampuni za gesi, tuna mpango wa kuongeza miundombinu ya kupokelea gesi pale bandarini kutoka tani 5,000 ambazo tunazo sasa hivi mpaka tani 45,000. Mikakati hiyo tunayo kwa sababu tunaamini tukifanya hivyo, basi tutakuwa tumepunguza bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, tumewasikia Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kuwa na mitungi ya kilo chache. Tayari kampuni zimeshaanza kufanyia kazi. Zipo kampuni ambazo zimeshaingiza sokoni mitungi ya kilo tatu. Tunaendelea kuzisihi kampuni nyingine waende na njia hiyo hiyo ili kuwarahisishia wananchi waweze kupata mitungi hii kwa gharama ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ameshafanya kikao na wadau wa *LPG* ili kuhakikisha tunakuwa na mawakala wengi zaidi hata kwenye maeneo ambayo yako mbali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hoja zenu zote tumezichukua na majibu yake tunayo na tunazifanyia kazi kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye suala la *CNG*. Waheshimiwa Wabunge tumewasikia kuhusiana na umuhimu wa kuongeza vituo vya kujazia gesi, lakini vilevile vituo vya kubadilisha mifumo ya magari ili yaweze kutumia gesi. Waheshimiwa Wabunge, maoni yenu tumesikia na vilevile ni kweli kabisa kwenye Kituo cha Ubungo foleni ni kubwa, lakini mikakati ya muda mfupi tunayo.

Mheshimiwa Spika, kupitia *TPDC* tayari tumeanza ujenzi wa kituo mama pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vilevile tuna ujenzi wa vituo vingine viwili ambavyo vinaendelea na ujenzi katika eneo la Kairuki pamoja na Muhimbili. Kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, tunaenda kufanya ujenzi wa vituo vingine 20. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kwa kipindi cha muda huu mfupi tunayo mikakati ya kuhakikisha tunamaliza foleni na kurahisishia wananchi upatikanaji wa gesi kwenye magari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la vitongoji, ili leo tuweze kufikia hapa kwenye kudai vitongoji ilikuwa ni lazima tuanzie sehemu na tuliweza kuanza kwenye kupeleka miundombinu vijijini. Kwa kuwa tayari tumeshafika huko, vitongoji vyote ambavyo vimebaki tutaenda kuvifikishia umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunao mkakati wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000 na tunapeleka kwa awamu. Tutaanza na vile vya kila jimbo 3,060 ambapo tupo kwenye hatua za mwisho za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, pia kwa mwaka huu wa fedha tunao mkakati wa kupeleka tena kwenye vitongoji 4,000. Kwa hiyo, mkakati wetu wa kupeleka kwenye vitongoji 20,000 ndiyo tunauanza Waheshimiwa Wabunge. Nawahakikishia kama ambavyo tunamaliza vijiji awamu kwa awamu, pia tutaenda kumaliza vitongoji.

Mheshimiwa Spika, ninapoenda kumalizia kuhusiana na wakandarasi ambao hawatekelezi majukumu yao vizuri. Waheshimiwa Wabunge tumewasikia na hususani mkandarasi wa Rukwa. Tuendelee kuwahimiza wakandarasi ambao

tumewaamini katika utekelezaji wa miradi yenye manufaa kwa wananchi wafanye miradi hii kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu tulishatoa maelekezo kwamba wakandarasi wote ambao hawafanyi kazi zao kwa weledi hatutaenda kuwapatia kazi chini ya taasisi ambazo zipo katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuhusiana na suala la huduma kwa wateja, kulikuwa na malalamiko kwamba simu hazipokelewi. Ni kweli, kipindi tuna mgao wa umeme tulikuwa tunapokea mpaka simu 40,000 kwa siku, lakini kutokana na kufanyia kazi changamoto hizi za umeme na umeme kupatikana, simu zimepungua kutoka kati ya 20,000 mpaka 17,000 kwa siku na uwezo wa kituo chetu ni simu kwa 87%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alitolea maelekezo ya namna ambavyo tutaweza kuwafikia wateja zaidi na tumefanyia kazi. Moja, tumerudisha huduma za simu kwenye kila mkoa. Kwa hiyo, kila mkoa wananchi wanaweza wakapiga simu kule. Pili, tumeboresha mawasiliano ya teknolojia kwa kuja na mbinu za kisasa. Tuna *chatbot* ambapo mtu kupitia *WhatsApp* anaweza akasema shida yake na akachati na akapata suluhisho la tatizo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusiana na *toll-free,* kwa kushirikiana na *TCRA,* tayari tumeshapata namba ambayo ni ya bure ambayo ni 180 na tupo kwenye mchakato wa mwisho wa kuhakikisha tunaanza kutumia namba ili wananchi waweze kupiga simu bure. Kwa hiyo, kwenye suala la huduma kwa wateja Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alilitolea maelekezo na vilevile tumelifanyia kazi kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kipekee naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri wenu na michango yenu. Yawezekana tusiwe tunaweza kuyajibu yote kwa mmoja mmoja, lakini nataka niwahakikishie, michango yenu tunaithamini sana sana na yale ambayo yanatekelezeka

tutahakikisha yanafanyiwa kazi kwa mustakabali wa Taifa letu na sekta yetu ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Nishati aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kama walivyoanza wenzangu, nami naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwepo hapa toka siku ya jana tukijadili masuala mbalimbali yanayohusu uendelezaji wa sekta ya nishati hapa nchini kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe kwa kutuongoza vizuri toka tumeanza mjadala huu. Kwa kweli kumekuwa na utulivu mkubwa na karibu kila Mbunge aliyepata nafasi ya kuzungumza kwa kweli amezungumza kwa niaba ya wananchi. Hii ndiyo dhana halisi ya uwakilishi, kwamba yale unayoyasoma kwenye mitandao au kuyasikia watu wakiyasema mahali fulani, ukiwasikiliza Wabunge wanayazungumza tena kisayansi kwa takwimu, kwa namba, kwa mifano na kwa historia ya changamoto ambazo tunapitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kweli kwa michango yao mizuri ambayo wametupatia toka siku ya jana na leo tunapokwenda kuhitimisha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unikubalie tena nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kweli mimi ukiniuliza pongezi zote tulizopata kwa wale waliosema wakatupongeza, tunastahili sehemu ndogo sana ya pongezi hizo. Anayestahili ni yeye mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ananiteua kuwa Waziri wa Nishati aliniambia, katende kila jambo kwa nia njema, hilo la kwanza na la pili, umeme hautaki siasa, unataka matokeo. Akaniambia sema kidogo, tenda sana, kwa sababu ukisema sana usitende mwisho wa siku kuna mahali utajikwaa na utadaiwa kwa kauli yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msemo mmoja mimi nilikuwa siufahamu unasema; "Aliyenyamaza hajuti," alinifundisha yeye. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ualimu wake, maelekezo yake na namna ambavyo amekuwa na kiu ya kuona Watanzania wanapata umeme na changamoto wanazopitia tunazimaliza kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa maelekezo yake, miongozo yake na usimamizi wake, hasa kwenye Sekta Ndogo ya Nishati Safi ya Kupikia ambayo yeye Ofisi yake ya Makamu wa Rais inasimamia masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwani toka nimeingia ofisini kwake, amekuwa mwalimu kwangu, amenifundisha mengi. Nataka nimhakikishie hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, nitaendelea kuwa msaidizi wake mtiifu ninayefuata miongozo yake wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyomjua Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni mtu rahimu, ambaye hakunyimi maarifa ambayo anayafahamu, lakini hachoki kukukosoa mahali ambako anadhani huendi sawasawa. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Judith Kapinga. Huyu, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, pamoja na kwamba ni Naibu Waziri wa Nishati, mtakubaliana nami kwamba sekta ya nishati ameifahamu kwa muda mfupi sana na anajifunza kwa haraka sana. Mheshimiwa Judith Kapinga ni mtu ambaye anasikiliza kila aina ya mtu na hata ikitokea mtu mahali fulani

akamwambia lugha ya ukali, ana *quality* moja ambayo wengi hatuna, anajua kujizuia. Nakupongeza sana Mheshimiwa Judith Kapinga, umekuwa msaidizi bora kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Judith Kapinga amekuwa akiibua vitu vingine wakati mwingine mimi sivifahamu, lakini anakiibua ananiambia kuna hiki cha kufanyia kazi Waziri, tukifanyie kazi. Ninaona fahari kubwa sana kufanya kazi naye na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa msaidizi ambaye ni Mheshimiwa Judith Kapinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana sana wadau mbalimbali wa sekta ya nishati. Wengi tuliwaalika waje; wadau wa maendeleo, wakandarasi, kampuni mbalimbali zinazoshughulika na masuala ya nishati, kampuni za mafuta, gesi asilia na kadhalika. Wote hawa wamekuwa na mchango mkubwa kwetu na utakumbuka miezi ya nyuma hapa ilikuwa kila wakati tukifika mabadiliko ya bei mafuta yanapotea, lakini ukweli yalikuwa hayapotei, yalikuwa yanahifadhiwa kwa ajili ya ku-*attract* bei mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulivyoitana, tukawaambia jambo hili lazima lifike mwisho na litafika mwisho kwa jasho lingi na ninawashukuru sana. Wao wenyewe wameamua kuchukua ile *principle* ya *regulate yourself or perish*, wakaamua kujisimamia wenyewe. Kila aliyeficha mafuta wameshughulikiana wenyewe na sisi kama Serikali tumechukua hatua. Tunawashukuru, kwa kweli ukipata wadau ambao ukiwaambia jambo wanafanyia kazi, siyo busara tena kuendelea kuwalaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kwa kweli kuzishukuru kampuni zote za mafuta hapa nchini kwa kuelewa dhana ya Serikali ya kutaka Watanzania wapate huduma iliyo bora na ya haraka zaidi. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo yote haya yanayotendeka hayawezi kutendeka kama hatuna watendaji ambao wana uwezo na kitu cha kuwasaidia Watanzania. Nawashukuru sana watendaji wote wa Wizara na taasisi zake zote chini ya Katibu

Mkuu, Mhandisi Felchesmi Mramba na Naibu wake Dkt. Mataragio kwa usimamizi mzuri sana wanaoufanya na kutusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukawa na watendaji unatoa maelekezo haya, halafu wanakuletea ugumu badala ya urahisi. Ni kawaida mahali fulani ukiwaambia watu tufanye jambo hili wanakutangulizia ugumu badala ya mkakati wa kufika kule mnakotaka kwenda, tofauti sana na watendaji wetu tulionao Wizara ya Nishati. Ukija na wazo watakwambia, tupe muda tutafute namna ya kulitekeleza kwa mujibu wa sheria na kwa haraka kama unavyotaka. Bila wao tusingefika hapa. Ninawashukuru sana na kwa sababu nimepata nafasi hii, naomba niwashukuru sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru wenyeviti wa bodi zote za Wizara ya Nishati, ni wenyeviti wabobezi kama mnavyowafahamu, walitambulishwa jana. Wana kalba yao, wana uzoefu wao, wana tajiriba kubwa na mimi nataka niwahakikishie kwamba tutaendelea kuwapa ushirikiano wa kila namna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa michango ya Waheshimiwa Wabunge na kwa sababu ya muda, naomba tu unikubalie nitumie fursa hii vilevile kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana kwa namna ya pekee Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Mwenyekiti na Makamu wake Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda kwa namna wanavyotusimamia tunapokuwa tunatekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali japo kwa kifupi zilizotolewa kwanza na Kamati ya Kudumu ya Bunge, na pia Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia. Waheshimiwa Wabunge 49 wamechangia kwa kusema hapa Bungeni, nami nilitaka niiweke michango yao kwenye makundi ili wakati wa kujibu, inawezekana nisitaje

mchango wa Mbunge mmoja mmoja, lakini walau kwa ujumla wake naweza kuzungumzia hoja walizokuwa wamezizungumzia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo takribani kila Mbunge ameizungumza ni hali ya kukatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Suala la kukatika umeme linawakera sana Watanzania, suala la kukatika umeme linawakera sana Waheshimiwa Wabunge, suala la kukatika umeme linakukera sana wewe.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati fulani tukiwa hapa Bungeni, Mbunge mmoja aliuliza swali, nawe ukaamua kutoa mwongozo, ukasema; "Hili suala la kukatikakatika umeme tupeni *timeframe,* litaisha lini?" Sisi tukasema linaweza kwisha mwezi wa Nne. Wewe ukasema mimi nakupeni hadi mwezi wa Sita. Nadhani ulikuwa na mashaka kidogo kutokana na historia ya kule tulikopita na matamko mengi ambayo tumekuwa tukiyafanya.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kuwa suala la kukatika umeme hapa nchini lilikuwa linachangiwa kwa kiwango kikubwa na upungufu wa umeme. Nataka nieleze hapa, kuna watu wengine wanaweza kuwa wanachanganya mambo huko nje, kwamba kukatika umeme kunachangiwa kwa kiasi kikubwa huko tulipotoka, ni upungufu wa umeme, kwamba umeme unaozalishwa na umeme unaohitajika, umeme unaozalishwa ni kidogo kuliko mahitaji.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa umeme tuliokuwa nao ulikuwa *megawatt* 410. *Megawatt* 410 ni umeme mwingi sana, kwa hiyo, kinachotokea ni lazima umeme utakatika kwa sababu kuna mgao wa umeme. Sasa hatua ya kwanza ya kufanya ni kuhakikisha kwamba neno mgao wa umeme linakwisha. Kwa sababu gani? Kwa sababu kile unachozalisha, basi kiwe na uwezo wa kuhimili yale mahitaji yaliyopo. Hiki ndicho kilichofanyika, kwamba uwezo wetu wa kuzalisha umeme unakutana na mahitaji na kunakuwa na ziada kidogo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana utaona tukiwasha mitambo yetu yote ya umeme, hatuna mahali pengine kwa

kupeleka umeme, hivyo inabidi mitambo mingine tuisimamishe iwe *standby* ili kukitokea madhara au tatizo mahali fulani, basi ule mtambo ambao upo kwa dharura unauwasha kwa ajili ya kuondoa hiyo changamoto ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hivi leo ninavyozungumza tuna mitambo mbalimbali ya Kidatu na kadhalika, lakini mitambo ya Kinyerezi mashine zote nne hatujaziwasha kwa sababu mahitaji ya umeme tunayohitaji na uwezo wetu wa kuzalisha unakidhi mahitaji na kwa hiyo hakuna mgao.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna jambo lingine, kwamba umeme utakatika siyo kwa sababu ya upungufu wa umeme, utakatika kwa sababu nyinginezo, na mojawapo ni miundombinu. Ni kweli Waheshimiwa Wabunge wameeleza hapa tena kwa uchungu kwamba miundombinu tuliyonayo mingi imechoka, na kwamba mashine nyingi tulizonazo za kuzalisha umeme ni za muda mrefu. Tukubaliane na ukweli huo kwamba nyingine ni za miaka ya 1970, nyingine ni za miaka ya 1980 na nyingine miaka ya 1990. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile kutakuwa na matengenezo ya hapa na pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njia za kusafirisha umeme; kwa sababu kuzalisha umeme ni jambo moja na kuufanya umeme umfikie mteja, ni jambo lingine. Njia hizo nazo ni ndefu sana. Utakuta kuna njia nyingine, amezungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja, kuna njia moja ya kuchukua umeme kuutoa *Unga Limited* upite mpaka uende Loliondo, ambayo ni kilomita nyingi sana. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, kukitokea shida mahali fulani, labda mti umedondoka au *line* imeharibika, unawatoa Watanzania wengi sana. Hilo halisababishwi na shida ya uzalishaji, linasababishwa na miundombinu

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingine tuliyonayo ya uhujumu tu wa miundombinu. Kuna watu tunao, ni Watanzania wenzetu, kwa sababu ya kujipatia fedha za haraka pengine wameamua kuiba *transformer*. Kwenye *transformer* kuna *product* mbili zinanunuliwa sana; zile waya pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, tuna matukio katika kipindi kifupi, *transformer* zetu 87 zimeibiwa, na unakuta kuna mtu mwingine anakata kwa ajili ya kutoa *cable* akauze. Sasa hivi tunao watu ambao wana kesi wapo Mahakamani. Huyu akichukua *transformer,* kuna watu wengi sana utawatoa kwenye umeme. Sasa atakayeonwa ni *TANESCO,* lakini kumbe kuna watu fulani wamesababisha shida hiyo.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ambayo inatokea ni katika kipindi hiki cha mvua. Waheshimiwa Wabunge tukubaliane na tukubali kwamba mvua hizi zimekuja, pamoja na kwamba ni neema, lakini pia zimeleta na gharama mbalimbali. Barabara zimekatika, kuna watu tunawazungumza hawana mahali pa kukaa. Kwa vyovyote vile, miundombinu yetu mingi itakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tu cha mvua tuna nguzo zaidi ya 651 zimeondolewa na maji. Nguzo ikiondoka maana yake hapo hapatakuwa na umeme. Tuna *transformer* 39 zimeondolewa na maji. Kwa vyovyote vile zile zikiondolewa hakutakuwa na umeme; na zikiondolewa hizo, maana yake umeme utakatika, siyo kwa sababu ya uzalishaji, bali ni sababu ya kimiundombinu.

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanyaje? Tunachukua kila aina ya hatua ili kuhakikisha kwamba tunaimarisha miundombinu. Ni kweli kwamba tunazo *line* ndefu, nchi hii tunahitaji vituo vya kupooza umeme *(substation)* 216 nchi nzima. Tulivyonavyo ni 131 tena na vyenyewe vingi vimechoka, ni vya muda mrefu. Tunahitaji kujenga vituo vipya 85, na tunahitaji kujenga vituo vipya vya kupoozea umeme kwenye maeneo ambayo yapo nje ya gridi 24. Vyote hivi vinahitaji uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupa kila aina ya *support* na Wizara ya Fedha pia. Rasilimali fedha tunapewa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kila shilingi tunayoipata inaleta maana ya maisha ya Watanzania kutafsiri shida tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyozungumzwa ni hatua zinazochukuliwa kwa wakandarasi wasiotekeleza miradi. Anayemulika nyoka, anaanzia miguuni mwake. Kabla hatujawalaumu wakandarasi wanaotoka nje, tujiangalie wakandarasi wa Serikali tulionao.

Mheshimiwa Spika, tunazo kampuni za Serikali zinazopewa miradi mbalimbali ya ujenzi. Kwa mfano *ITIDICO* ni kampuni yetu, ina miradi mingi inajenga. Sasa, *performance* yao ikoje? *Performance* yao siyo nzuri. Tunakubaliana na watu wa Tabora wataniambia, watu wa Katavi watazungumza na maeneo mengine. Sasa unafanyaje? Unaendelea kusema ongezeni kasi halafu hali inabaki kama ilivyo, hapana, ni lazima kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tuliivunja Bodi ya *ITIDICO* kwa sababu ya kutaka tuwe na ufanisi. Tukaibadilisha Menejimenti ya *ITIDICO* ili tupate ufanisi, na tunakwenda kwa wakandarasi wa sekta binafsi ambao wote wamepewa kazi halafu hawajafanya kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua kuna *trick* nyingine za kisheria lazima uende kwa tahadhari. Nataka niwaambieni Waheshimiwa Wabunge kwamba tunawafanyia uchambuzi na kwa yeyote yule ambaye *performance* yake haikufika viwango tunavyohitaji miradi inayokuja baadaye hatutawapa na badala yake tutawapa watu ambao wana uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tunachotaka, Waheshimiwa Wabunge wakisimama hapa Bungeni na ninamwomba Mungu iwe hivyo, kazi yao iwe kusema umeme umefika, tunataka ufike na mahali fulani. Hili nataka nilieleze na nadhani ni jambo la kueleweshana. Waheshimiwa Wabunge kuna watu wanasema kwamba umepeleka umeme kwenye kijiji fulani, ndiyo, lakini waliopata ni watu 20, ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kufikisha umeme, kwenye kijiji kuwe na *access*. Dar es Salaam unayoiona hapa 15% ya wakazi wake hawana umeme, haimaanishi kwamba Dar es

Salaam hakuna umeme. Jambo la kuwaunganisha wananchi na umeme ni jambo endelevu. Utafikisha umeme leo, kuna watu 20 wamejenga nyumba mpya, kesho nao watahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni *access*, umeme ufike, halafu baadaye utaendelea kuunganisha taratibu. Ni jambo ambalo tutaendelea nalo miaka yote, halitaisha. Muhimu umeme ufike kwanza, vijiji vyote 12,000 vipate umeme, tukimaliza vijiji, vitongoji 64,000 vipate umeme, baadaye *connectivity* itaendelea hatua kwa hatua, hatimaye Watanzania waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli niwashukuru tena, mnatuvumilia mno. Wakati fulani tukipata changamoto mnakuwa pamoja nasi pamoja na Watanzania. Naomba mtuvumilie, mtukubalie tufanye jambo moja. La kwanza, tuwaambie ukweli na ukweli ni huu kwamba ni lazima umeme ufike kwanza kijijini kabla haujakwenda kitongojini; na umeme ukifika kitongojini utatoka kwenye kitongoji utakwenda kwenye nyumba *(household)*.

Mheshimiwa Spika, haitatokea hata siku moja nyumba zote kwenye kitongoji hicho ziamke siku moja zina umeme zote. Atakayewaambia maneno haya, ni mwongo na Mbinguni hafiki. Tunakwenda hatua kwa hatua kwa utaratibu, na hiki ndicho tutakachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale walio nje ya Gridi ya Taifa, Mikoa ya Kagera, Katavi, Lindi na Mtwara nataka niwahakikishieni kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita imeweka *resource* ya kutosha ya kuji-*connect* sisi na mikoa yote hapa nchini. Siyo tu hivyo, tunataka tujiunge vilevile na mataifa ambayo ni jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, tayari tumekamilisha Mradi wa Lemguru, tunajiunga na Kenya, Rwanda na Burundi tumeshajiunga. Tunajenga mradi wetu wa Kwenda kujiunga na Zambia. Tukimaliza hiyo, kama tuna ziada kama sasa hivi, basi tuwe na *power exchange program* pamoja na majirani zetu kwa mujibu wa taratibu zetu za *Eastern African Power*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tunalifanya, sasa tunajenga mradi mkubwa wa kuwaunganisha watu wa Kagera na gridi kule Lindi na Mtwara. Kama tulivyoeleza, miradi inaendelea. Zipo changamoto za fidia za hapa na pale, na kwa upande wa Lindi, tunazifanyia kazi ili tuweze kukamilisha utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, limeelezwa jambo lingine hapa kuhusiana na habari ya *CSR* kwenye maeneo ambako kuna miradi ya mafuta na gesi. Naomba nikiri kwamba Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza jambo hili wamezungumza ukweli. Sisi Wizara ya Nishati tumepitia tukajiuliza, hivi kweli watu wa Lindi na Mtwara ambao ni wazalishaji wa gesi *CSR* yao ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeenda Madimba, tumeenda Songosongo. Watu wa Songosongo; kutoka Songosongo kwenda Makao Makuu ya Wilaya, mahali ambako gesi inatoka, hawana hata usafiri wa kuwafikisha kwenda Makao Makuu ya Wilaya. Unawakuta wananchi wanalalamika umeme unakatika kwenye maeneo yao na gesi inatoka pale; hili halikubaliki, ni lazima tuchukue hatua.

Mheshimiwa Spika, tumeamua sasa kwa pamoja, na kwenye hotuba yangu nimeeleza kwamba tunapitisha kanuni ya uwajibikaji kwa wananchi kwenye miradi yote ya mafuta na gesi ili tuwatoe wananchi kwenye malalamiko ya kuona kwamba gesi hii tunaitoa hapa tunaipeleka mahali fulani huku hali zao bado zipo mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nataka nikuhakikishie kwamba kwa Madimba na Songosongo tunao mpango maalum. Kwa sababu haiwezekani kwenye *plant* mle ndani wana umeme wa kutosha haukatiki, lakini wananchi nje ya *plant* umeme unakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwamba ni lazima tutengeneze utaratibu wa wao kuwa na *line* mbili; *line* ya *TANESCO* na *line* nyingine inayotoka kwenye *plant* ambako umeme haukatiki kwenda kwenye maisha ya watu

wanaozunguka maeneo hayo ili wakati umeme wa *TANESCO* ukikatika wawe wana-*backup* ya umeme mwingine unaotoka kwenye *plant*.

Mheshiiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba kwenye *plant* kule umeme wao haukatiki, kila siku upo, ila pale nje kwa wananchi unakatika; na wananchi bahati njema ni watu rahimu, mabomba yale yakipasuka ndio wanaopiga simu kusema kwamba mabomba yenu yamepasuka, njooni m-*fix*. Sasa kama wao wana wema mkubwa kwenye miradi hiyo, ni lazima na sisi Serikali tuwaoneshe wema kwa kuwapatia huduma bora kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, wakati tunazungumza hizi kampuni kubwa kufanya *CSR* kwenye miradi, tukubali kwamba zipo fedha zinalipwa, zinaitwa *service levy*. *Service levy* ikilipwa inalipwa kwenye halmashauri, lakini kwa bahati mbaya halmashauri wakati wa kusimamia zile fedha vipaumbele vyao haviangalii maeneo ambako miradi hii ndiyo imezalisha hii *service levy*.

Mheshimiwa Spika, jambo hili na sisi ni Madiwani, twende tukawaambie wakurugenzi. Hapa nataka niwaombe Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri wote, sasa hapa nazungumza kama Naibu Waziri Mkuu. Fedha za *service levy* zinazokwenda kwenye halmashauri kutoka kwenye miradi yote ya mafuta na gesi ni lazima sehemu ya fedha hizo irudi kwenye vijiji ambavyo kunachimbwa hiyo gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekwenda Songosongo, Waheshimiwa wa Kilwa mpo hapa, shilingi milioni 500 za *Service Levy* zimechukuliwa pale ndani, zipo kwenye halmashauri, lakini halmashauri hawajawarudishia fedha watu wa Songosongo. Haikubaliki na haiwezi kuwa sawa. Hili tutaanza kulisimamia kuanzia sasa. Katibu Mkuu Wizara ya Nishati wasiliana na Katibu Mkuu TAMISEMI tuje na mpango wa *Service Levy* zinazotolewa kwenye hayo maeneo ili zianze kurudi kwenye maeneo hayo ambako Serikali inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili wakati tunasaini mkataba wa kununua *shares* za *Wint Wealth* Mheshimiwa Rais alilieleza, tena kwa utulivu kabisa, akasema sitaki kuona malalamiko ya wananchi mahali ambapo gesi inachimbwa, wanaendelea kulalamika na maneno kwamba sisi hatuoni manufaa ya gesi. *Service Levy*, *CSR* sasa zitaanza kufanyiwa kazi kwa kasi kubwa, na Waheshimiwa Wabunge mtupe taarifa mahali mnapoona haya mambo hayaendi sawa.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie hili jambo la *CSR* kwenye *EACOP*. Mheshimiwa Mbunge amezungumza kwamba walifanya ziara kule, walipofika wakaambiwa *CSR* ni siri. Aliyesema hivyo ni mwongo, *CSR* siyo siri, *CSR* ni kitu cha wazi. Kama Serikali inakuja hapa kutangaza mapato na matumizi kwa Wabunge na mipango yake, *CSR* ni kitu gani kiwe siri kwa wananchi na Wabunge? Haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, habari ninayotaka kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba *EACOP* sisi kama wabia tena tuliochangia fedha nyingi, dola za kimarekani milioni 289.78 tunalisimamia. Ndiyo maana mtaona *CSR* kwenye *EACOP* tumeshatumia shilingi bilioni 27. Shilingi bilioni 3.7 zimekwenda kwenye miradi ya maji, shilingi bilioni 19.6 zimekwenda kwenye miradi ya barabara na shilingi milioni 710 kwenye elimu na afya. Hizi ni fedha ambazo zimetolewa kwenye maeneo ambako miradi inafanyika; Tanga, Tabora kwa maana ya Nzega pamoja na Misenyi, imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuna *local content issue* inazungumzwa. Nawaomba Watanzania kupitia Bunge lako tuache kuwa madalali wa kujinyima faida kama nchi. Hapa kwenye *EACOP* kanuni yetu ipo *clear,* kwamba kazi ambazo anaweza kufanya Mtanzania afanye Mtanzania na siyo mgeni.

Mheshimiwa Spika, vinatokea vikampuni vya kigeni vinamtafuta Mtanzania mmoja anaitwa Doto Biteko anatoa *NIDA* yake, anatoa *documents* zake; kinasajiliwa kikampuni *a shell company,* yule Mtanzania anapewa hela yake kidogo tu halafu huyu mtu anachukua. Mle ndani kuna Mtanzania, lakini nyuma

kuna watu wengine nje ya nchi. Mkienda ku-*compete* nyaraka zinaonekana ni Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, ukimtafuta huyo Mtanzania ukamwuliza, uliomba kazi gani? Anakwambia, kwani wapi? Maana naye hajui. Yeye kapewa hela yake, dola elfu 50, ameona Mbingu na dunia zimekutana zinamshangilia. Kumbe hiyo kazi unafanya, ni ya kuchukua mtaji ndani ya nchi na kuwapelekea watu nje ya nchi. Tumechukua hatua, tumewachambua wote kupitia *EWURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana *EWURA* na *TPDC,* wale wote ambao wamefanya *artificial company* kwa kutumia *document* za Watanzania wakati wao ni watu wa nje tumewaondoa kwenye utaratibu wa kazi na tutaendelea na kazi hizo. Haiwezekani eti kujenga barabara tena barabara ya vumbi inayotaka *excavator*, *compactor* na mitambo ambayo kila Mtanzania hapa anayo kazi hiyo, ichukuliwe na mtu kutoka nje ya nchi, haiwezekani. *It will never happen under my watch and under Dr. Samia Suluhu Hassan's watch*, kwa sababu tunataka Watanzania wanufaike na rasilimali walizonazo pamoja na miradi hii. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Deus kwamba hili tumelifanyia kazi na tutalimaliza na Mungu atusaidie tutalifikisha.

Mheshimiwa Spika, najua nina *constrain* ya muda na nimeshasikia hiyo kengele, nami nakuangalia; najua ukimwangalia mtu kwamba muda umeisha, una jicho la aina fulani, nimeshakuona, unikubalie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo yanayoitwa vijiji miji ambayo na yenyewe kuna mahali watu wanaambiwa kwamba sasa ni lazima nao walipe shilingi 320,000.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais akiwa ziara Mtwara na Lindi, alitupa kazi mahususi, akasema tuyachambue maeneo hayo. Tumefanya uchambuzi, tumepata maeneo 1,570 ambayo kwa kweli unaweza ukayataja ni miji, lakini kwa kweli ni vijijini, wanastahili kulipa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais amesikia kilio chenu, tunakwenda kuyafanyia kazi maeneo haya na utaratibu utaelezwa hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kusogeza huduma kwa wananchi, yapo maeneo ni makubwa sana, mahitaji yamekuwa makubwa, ni lazima tubadilishe maeneo ya utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wameeleza Waheshimiwa Wabunge, kwa mfano Kigamboni. Kigamboni ipo Temeke. Kigamboni peke yake ni eneo kubwa mno. Meneja wa Mkoa wa Temeke atoke huko aliko ndiko watu wengi waliko na watu wanajenga ndani ya Kigamboni kwenda mbali. Tumeamua kama Wizara, tutaongeza maeneo ya kiutawala ili tusogeze huduma zaidi Kigamboni ikiwepo na Kahama kwa sababu tunafahamu mahitaji yale yanahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la *CNG* tunalichukua kwa uzito mkubwa. Amesema hapa Mheshimiwa Musukuma, kwamba Serikali tuanze. Sisi pamoja na *GPSA* tumeanza kutafuta mshauri ili vyombo vyote vya Serikali tunavyotumia, basi viwe na *hybrid* ya kuwa na *CNG*. Tunasubiri uchambuzi huo ufanyike, ukishafanyika, kiu yetu ni kuona huko tuendako kwa ajili ya kupunguza matumizi ya Serikali, basi tuwe na magari ambayo yanatumia *CNG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepunguza masharti ya kufungua Vituo vya *CNG,* wapo watu wengine wameomba, wakishaomba bahati mbaya wanachelewa kurudi. Kwa mfano, Mheshimiwa Kilumbe amezungumza kwamba, kuna maombi 11. Namwomba Mheshimiwa Kilumbe, kama anawafahamu awaambie walete *documents* tulizowaomba. Kuna mwingine ameombwa tu alete

*EIA* haraka haraka anakwambia ngoja nije nitachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tunayo maombi zaidi ya 30 ya watu wanaoomba kufungua vituo vipya vya *CNG,* ninataka niwahakikishieni kwamba, akileta leo nyaraka zake zimekamilika, kesho yake asubuhi kunapokucha tutakuwa tumeshashughulikia hiyo kazi yake na nyaraka zote zimekamilika, na ndani ya siku tatu tutakuwa tumempa leseni ili aendelee kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la *call center,* amelieleza. Nimalizie la mwisho kabisa kuwaomba ndugu zetu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, watuvumilie, tuna kazi kubwa ya kufanya ndani ya *TANESCO* kwa sababu tunaamini kwamba, *TANESCO* ndio wamebeba moyo wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kila Meneja aliyefanya vizuri humu ndani mmempa maua yake. Mimi nikiona mnawapongeza ninyi ninapata nguvu kwamba nina watu sahihi wa kufanya nao kazi. Ninaomba mfanye nao kazi, mahali wanapokosea waambieni na kama mnaona ni kichwa ngumu niambieni mimi ndiyo kazi yangu niliyopewa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepeana utaratibu wa kupimana kila siku. Kila siku Mkurugenzi wetu wa usafirishaji wa umeme *wa distribution,* tunachukua tiketi, nani amefanya vizuri? Tunawapanga wa kwanza hadi wa mwisho. Tukimaliza kuwapanga wa kwanza hadi wa mwisho, kwa wiki tunatengeneza ripoti moja. Tunajua wiki hii Meneja wa Mkoa gani hajafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunapanga wiki nne kutengeneza ripoti ya mwezi. Tukimaliza tunachukua miezi mitatu tunatengeneza robo moja. Hiyo robo moja aliyefanya vizuri tunampa zawadi aliyekuwa wa mwisho kwa kushughulika na wateja, tunamshusha cheo. lazima tukubaliane, tuwe na mipango. Wananchi wanataka tuwe na kitu ambacho wakiwa na tatizo kwenye umeme wapate majibu. *(Makofi)*

Mhehimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge watupe muda, *TANESCO* wanafanya kazi kubwa. Wakati mwingine mkiona wanatoa taarifa ya katizo la umeme, jamani tuelewe siyo mgao, wanahitaji kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, kwa mfano, leo kule Kilimanjaro mafuriko yametokea, Meneja wetu wa *TANESCO* ameombwa azime umeme ili kunusuru hali iliyopo kule. Atafanyaje Meneja huyu akikata umeme? Tuwavumilie. Matangazo yale wanayoyatoa, basi tuyapokee tukiamini kwamba ni ya nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tangazo mtu anasema; "Tutazima umeme kwa ajili ya matengenezo ya kinga." Mtu wa *comment* ya kwanza anasema; "Ninyi nanyi tumewachoka." Sasa tufanyaje katika mazingira kama hayo? Ni lazima hii miundombinu iendelee kutengenezwa, kama ambavyo una gari Mheshimiwa Mbunge, utaiendesha kila baada ya muda fulani utaipeleka gereji kutengenezwa. Ukiipeleka gereji kutengenezwa, haimaanishi hauna gari, gari ipo unarekebisha na miundombinu ipo vilevile.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna mahali fulani kikombe kimepasuka, ni lazima turekebishe, na huwezi kurekebisha kukiwa na umeme, ni lazima utazima. Watukubalie wakati tunafanya marekebisho hayo, kwani tutakuwa tukiyafanya hapa na pale. Cha muhimu, wananchi wanapaswa kufahamu kwamba kuna jambo gani linakuja kukata umeme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, na ninaushukuru sana Uongozi wa Bunge. Kwa kweli tumesikiliza hoja zenu, tunakwenda kufanyia kazi. Kwa unyeyekevu mkubwa, wale ambao mmeahidi kushika shilingi yangu, naomba mnifanyie hisani moja, mnipe fedha pamoja na wasaidizi wangu tukatatue changamoto ya yale yote mliyoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi hatutakuja hapa; na moja ya jambo ambalo nimewaambia wenzangu ni kwamba, msiende kusema uwongo kwa ajili ya kutafuta makofi. Utapigiwa makofi leo, kesho

makofi hayo yatageuka kuwa kuzomewa. Tutafute heshima ya kusema ukweli na kuwa na matokeo kwa kazi yetu na kusema kidogo na kuwa na matokeo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba mtupitishie fedha hizi shilingi trilioni 1.8, tulizoomba. Ukweli ni kwamba, zitakwenda kutatua changamoto tulizonazo. Baada ya robo inayokuja, tutakuja kujipima kwenu, wapi tumefikia kupitia Kamati yenu?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba tena kutoa hoja na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kama ilivyo ada, tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

## KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 58 - Wizara ya Nishati

Kifungu1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................... Sh. 4,949,110,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndiyo chenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ameomba mumpitishie bila kushika shilingi na sina majina hapa mbele ya kushika shilingi. *(Makofi)*

Sawa, kwa kuutazama muda tulionao hapa, tutapitisha kwa mafungu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati**

Kifungu1001 - *Administration and Human Resources Management*...................................... Sh. 4,949,110,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…..............Sh.1,217,634,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.......................Sh.1,601,052,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 625,759,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*..................................Sh. 650,523,000
Kifungu 1006 - *Government Comm Unit*........................Sh. 591,880,000
Kifungu 1007 - *Procurement Management Unit*………………………...…………Sh. 600,143,000
Kifungu 1008 - *Environment Management Unit*............Sh. 386,128,000
Kifungu 1009 - *Management Info System Unit*..............Sh. 654,756,000
Kifungu 1010 - *Monitoring and Evaluation Unit*.............Sh. 741,084,000
Kifungu 3001- *Electricity and Renewable Energy*……....………………….......Sh.56,274,440,000
Kifungu 3002 - *Petroleum and Gas*............................Sh. 20,600,114,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*..........................................................Sh. 0
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*....................Sh. 1,020,274,000
Kifungu 3001 - *Electricity and Renewable Energy*…..................….Sh.1,726,459,058,000
Kifungu 3002 - *Petroleum and Gas*…....................……Sh. 67,387,500,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, kwa hiyo, imepita, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Watendaji wote chini ya Wizara hii na kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeahidi kuyafanya kupitia bajeti hii mliyoileta mbele ya Bunge. *(Makofi)*

Naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Nishati na Madini, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa kazi nzuri walivyoifanya mpaka tumefika hapa leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mawazo mliyoyatoa, mmemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, mmemsikia Mheshimiwa Waziri akieleza namna ambavyo watayafanyia kazi. Kwa kweli wamewasikiliza na hoja zenu wameweza kuzijibu na yale ambayo hawakujibu, kama walivyosema wameyasikiliza na yote watayafanyia kazi. Sote tunawatakia kila la heri katika kuyatekeleza hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja ambalo Mheshimiwa Waziri wa Nishati amelitolea ufafanuzi hapa, ninafikiri tunarudi

kwenye hoja yetu ile ile ya Waziri wa Mipango, ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais. Hoja ya *CSR* imefafanuliwa vizuri sana hapa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati pia amefafanua vizuri zaidi aliposema anazungumza, sasa kama fulani, kama Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hayo nayo yatatusaidia sana Waziri wa Mipango. Kwa sababu nimesikia kwenye *EACOP,* imetajwa Tanga kwamba imo, kule nako kwenye Rufiji imo, Tanga; sasa nawaza, mbona huko kwenye *EACOP* hawajatajwa kule watu wa Lindi, Mtwara na Morogoro? Sasa hao wengine mbona wanaingia kila mahali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hayo yote nafikiri mipango ikiwekwa vizuri mambo yatakaa sawa. Kwa hiyo, kwa kweli ninajaribu tu kusisitiza kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tunatarajia mambo mengi yanayolalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge tutafika mahali ambapo kwa kweli yatakuwa yamekaa sawa, pale ambapo tutakuwa tumeweka uwiano mzuri, kwa sababu ipo miradi mikubwa mingi tu inaendelea kubuniwa ambayo pengine *CSR* zake zitakuwa kubwa zaidi na pengine tutatakiwa kuweka uwiano, kwa sababu mwisho wa haya rasilimali ni zetu wote nchi hii.

Kwa Kweli tungetamani kila mwananchi aone naye ni sehemu ya nchi hii katika kufaidika na hayo yote. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nitumie fursa hii kuwatakia ninyi kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania, Maadhimisho mema ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Siku ya kesho, sote tutakuwa tukikumbuka mambo mazuri na mazito ambayo waanzilishi wa Muungano huu, kwa maana ya Baba yetu Mwalimu Nyerere na pia Baba yetu Mzee Karume, walivyoyafanya na mpaka sisi tumeweza kuendelea kufaidika na huu Muungano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.58 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 29 Aprili, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*